

16 APRILI, 2012

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Tano – Tarehe 16 Aprili, 2012

(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 52

**Ahadi ya Rais Kununua Gari la Wagonjwa
(Ambulance) - Kituo cha Afya Mlangali**

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE aliuliza:-

Mwaka 2008, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshim iwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, aliahidi kuwapatia wananchi wa Mlangali gari jipya la wagonjwa *Ambulance*:-

16 APRILI, 2012

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza ahadi hiyo?

(b) Je, gari hilo linaweza kupatikana leo baada ya Bunge kuahirishwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe Mbunge wa Ludewa lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mheshimiwa Rais mwaka 2008 aliahidi kutoa gari kwa ajili ya kituo cha afya Mlangali katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa. Kwa kuzingatia ahadi ya Mheshimiwa Rais na adha ya usafiri waliyo nayo wananchi wa Mlangali, tarehe 1 Aprili, 2011 Serikali ilipeleka gari la kubebea wagonjwa katika kituo cha Afya Mlangali kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wanaohitaji rufaa. Gari lililonunuliwa ni *Toyota Land Cruiser Hardtop* lenye Na. Za usajili SM 9192. Gari hili lilikabidhiwa kituo cha afya Mlangali tangu Septemba, 2011.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii na fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Deo Filikunjombe kwa jitihada kubwa alizofanya kwa wananchi wake wa Ludewa kwa kuamua kununua magari mawili (*hiace*) ambapo yanatumika kusafirishia wagonjwa wa rufaa katika Wilaya ya Ludewa.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Waziri kwa pongezi, lakini cha pili nina maswali mawili madogo:-

Kwanza hili gari ambalo lilikuja Mlangali, ambalo lilikuja Ludewa lililetwa mwaka mmoja kabla na lilipofika Ludewa halikuwa na maelekezo bayana. Lile gari lilipofika Ludewa, Baraza la Madiwani, tulika na kulipeleka sehemu nyingine ambako kuna shida kubwa zaidi ya usafari. Kwa hiyo, kwanza namwomba Waziri akiri kwamba gari lilikuja bila mawasiliano, mawasiliano yalikuwa ni duni. Lakini cha pili, sehemu ya pili Rais alipokuja Ludewa nilizungumza naye na alisikitika kwamba gari limepelekwa sehemu nyingine awali na baadaye limehamishiwa kwenda sehemu nyingine na akaahidi kwamba atatekeleza ahadi yake, ahadi yake bado iko pale pale gari bado linakuja. Sasa hivi tunavyozungumza kuna shida ya usafiri Ludewa. Je, ahadi ya Mheshimiwa Rais kutuletea gari

16 APRILI, 2012

wananchi wa Ludewa Mjini ambako gari hili limeondolewa, itatekelezwa lini? Ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Deo Filikunjombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama tumeambiwa kwamba gari limepotea, halikuonekana ndiyo ningepata shida hapa, lakini gari kama limekwenda kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, na limekwenda Mlangali, mimi sipati tabu sana na Mheshimiwa Filikunjombe kwa hicho anachokizungumza.

Kwa hiyo, inawezekana kabisa kama anavyosema kwamba mawasiliano hayakuwa bayana lakini anakiri kwamba gari limekwenda kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa na kama anavyosema hapa maombi yaliyopelekwa kwa Mheshimiwa Rais, yalikuwa ni maombi kwa ajili ya kile kituo cha afya cha Mlangali, kwa hiyo gari lilikwenda kule.

Sasa hili lingine ambalo Mheshimiwa amefanya mawasiliano, kwanza mimi nampongeza sana kwa sababu nimekwenda kule, mimi nilikuwa Ludewa, Mheshimiwa Spika, unakumbuka, nimeyaona haya

16 APRILI, 2012

magari ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyanunua na mimi siwezi kusimama hapa nikasema kwamba sizioni jitihada za Mheshimiwa Mbunge anazofanya katika Jimbo lake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shida yangu mimi, ni hapa sasa kutoka hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naahidi gari lingine litakwenda, sasa mimi nitakwenda kwenye records nikaangalie, lakini nataka nikudhibitishie hapa Mheshimiwa Spika, na nyumba hii niisibitishie kwamba gari, hili nililolitaja hapa hardtop namba SM 9192 lilikwenda katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa. Pale ndipo plan unit ilipo na wao ndiyo wanaelekeza, sasa maelekezo yalikuwa ipelekwe kule Mlangali sasa kama yalikuja at a later stage hivi ni vitu ambavyo tutawekana sawa na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kujua kwamba nini kinachoendelea.

SPIKA: Bado nakumbusha hamkusimama kabla. Kwa hiyo, naendelea, suala linalofuata, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga.

Na.53

**Ahadi ya Kuweka Lami Barabara za Mji wa
Makambako**

MHE. DEO K. SANGA aliuliza:-

16 APRILI, 2012

Tarehe 31 Oktoba, 2010, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Mji wa Makambako aliahidi kuweka lami km 5 za barabara za Mji wa Makambako. Lakini ahadi hiyo bado haijatekelezwa. Je ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Naomba maswali ya nyongeza yawe *brief to the point* kusudi tuwe na maswali mengi zaidi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Njombe Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Mji wa Makambako tarehe 31 Oktoba, 2010 aliahidi kujenga kilometa 5 za barabara ya lami katika Mji wa Makambako. Katika kutekeleza ahadi hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia mfuko wa barabara fungu la maendeleo kwa mwaka 2012/2013 imeomba shilingi milioni mia sita (600,000,000) kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa

16 APRILI, 2012

kiwango cha lami kwa jumla ya kilometa 2 kutoka tanki la maji- Afya (Mjimwema road) na Ubena-Sokoni katika eneo lile la (*Ubena road*)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imepanga kuanza ujenzi wa barabara za lami kwa awamu ambapo katika mwaka 2012/2013 jumla ya kilometa 5 zitajengwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mitaro ya maji kwa gharama ya shilingi bilioni 3.

Fedha hizi zimewekwa katika maombi maalum ya mpango wa Bajeti ya Halmashauri kwa mwaka wa 2012/2013. Azima ya Serikali ni kuhakikisha kuwa kilometa zote tano zinajengwa na kukamilika kwa wakati.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Serikali, labda niseme tu kwamba naishukuru Serikali, ninachoomba kwamba kilometa mbili ambazo Mheshimiwa Waziri ameonyesha hapa kwamba wataanza kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013 basi niseme naipongeza Serikali kwa namna ambavyo ina majibu mazuri, ahsante sana Mheshimiwa Spika.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu hayo mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa, ningependa

16 APRILI, 2012

kujua jukumu la *road board* ya Mkoa mpya wa Njombe kuhusiana na suala hili, ili sisi tutakao kuwa kule tuweze kuwasimamia vema. Kwa hiyo, labda Waziri angetueleza vyema jukumu la *road board* kuhusiana na ahadi hii nzuri ya Serikali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Njombe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jukumu la *road board* mpya kwa maana ya Mkoa mpya wa Njombe, halina tofauti na majukumu ya *road boards* hizi zilizoko sasa, katika kazi yake kubwa hapa ni kuhakikisha kwamba Bajeti ile inapita na Bajeti ile ikipita inajengewa hoja, hapa nimeeleza hapa kuna *issue* hapa kwamba haya ni maombi maalum. Unapozungumza habari ya bilioni 3, bilioni 3 haziingi moja kwa moja katika Halmashauri pale kwa sababu ita-*bust* na *ceiling* yetu ni kama 10% *sometimes* Serikali inaamua kwamba hakuna.

Kwa hiyo, jukumu lake kubwa litakuwa ni kujenga hoja kwa sababu tutakwenda kukutana sasa kama Mkoa mpya, tutakwenda kukutana na Wizara ya Fedha sasa ili tuzungumze sasa kuhusu

16 APRILI, 2012

haya maombi maalum na nataka nikuthibitishie kwamba kwa vile hili linatoka ofisini kwetu na ni Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi sisi tutashirikiana na hiyo road board mpya, kuhakikisha kwamba hela zinapatikana na barabara hii inajengwa. (*Makofi*)

MHE. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Swali hili linafanana kabisa na ahadi ambayo Mheshimiwa Rais aliitoa Karatu mwezi wa kumi na kwa kuwa Waziri mara zote amekuwa amesema ahadi ya Rais haina mjadala na kutekelezwa. Ni lini ahadi ya Rais ya kutengeneza lami kilometa mbili katika Mji wa Karatu itatekelezwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mchungaji Natse, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mchungaji anasema vizuri na ni kweli tumekuwa tunajibu hivyo, hapa hatuna tabia ya kukaa hapa tukaanza kubishana kuhusu ahadi za Rais na kama tulivyokuwa tumeeleza kule nyuma. Sisi tunachofanya ni kwamba tunaenda awamu kwa awamu. Sasa hivi tumemaliza Bajeti

16 APRILI, 2012

moja, kwanza hata hatujaimaliza, hatujafika, mpaka tufike kwenye mwezi wa sita, au mwezi wa saba.

Kwa hiyo, ni mwaka mmoja, mpaka miaka mitano itakapokuwa imekamilika, mimi nitakwenda kucheki sasa kwa vile ameni-*alert* hapa ili tuone kwamba hizo kilometa mbili na zinatengenezwa kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi.

Na. 54

Matatizo Sugu ya Maji-Kishapu

MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI (K.n.y. MHE. MASOUD S. NCHAMBI) aliuliza:-

Tatizo la maji Kishapu limekuwa sugu na linasababisha wananchi wake kutumia muda mwingi kutafuta maji kwa taabu sana hasa nyakati za ukame:-

Je, kwa nini Serikali isitoe fedha kwa ajili ya kuchimba visima katika vijiji vyote vya Jimbo la Kishapu?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman

16 APRILI, 2012

Masoud Nchambi Suleiman, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ni moja ya Wilaya zenye uhaba mkubwa wa maji chini ya ardhi. Tafiti mbalimbali zilizofanyika Wilayani humo zimeonesha kuwa maeneo mengi ya Wilaya hiyo hayafai kuchimba visima kwa sababu ya uhaba wa maji chini ya ardhi.

Tafiti ya karibuni ilifanyika katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 kupitia mtalaam mshauri *NETWAS (T) Ltd.* Utafiti huo ulifanyika chini ya programu ya kitaifa ya majisafi na usafi wa mazingira Vijijini inayoendelea kutekelezwa Wilaya zote nchini pamoja na hivi Vijiji kumi.

Tarehe 29 Agosti, 2011 Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ilitangaza zabuni ya kuajiri wakandarasi watakaojenga miundombinu ya maji kwa vijiji sita vya awali. Vijiji hivyo ni Mwamshimba, Mwigumbi, Bulekela, Iboja, Nyenze na Seke Iddi.

Kwa sasa Halmashauri ya Wilaya, Wizara ya Maji na Benki ya Dunia wanakamilisha tathmini ya zabuni hizo ili kupata wakandarasi. Jumla ya shilingi bilioni 1.4 zimetengwa katika mwaka wa fedha 2011/2012 kutekeleza kazi hiyo.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuvipatia Vijiji vingine huduma ya maji itaendelea kutekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Lengo ni kuvipatia vijiji vyote huduma ya maji ifikapo mwaka 2025. *(Makofi)*

MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Vijiji sita hivyo vilivyopatiwa maji ni kati ya Vijiji 114 vilivyoko katika Jimbo la Kishapu na ni dhahiri kwamba ni asilimi 4 tu ya wananchi ndiyo wataweza kufikiwa na huduma hiyo ya maji:-

(a)Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga miundombinu ya maji katika Vijiji 108 vilivyosalia ili wananchi wa Jimbo hilo waweze kunufaika na huduma ya maji hususani wanawake?

(b)Kwa kuwa katika Wilaya ya Kishapu, suluhisho pekee ya kupata maji ni kupitia mradi wa Ziwa Victoria. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na utekelezaji wa mradi mapema iwezekanavyo? Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante, wewe ndiyo mwaminifu kweli kweli naomba ujibu maswali, umeuliza exactly unavyotaka mwenzio. Haya Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

16 APRILI, 2012

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kairuki kama ifuatavyo:-

Kwanza kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba tumeanza na Vijiji 6 lakini lengo la Serikali ni Vijiji vyote tutavipatia maji ifikapo mwaka 2025. Kwa hiyo, kila mwaka tutakuwa tunakwenda kwa hatua na Vijiji vingi tutavifanya katika programu awamu ya pili, awamu ya kwanza tutaishia kwenye hivyo Vijiji 6, lakini usanifu umefanyika katika Vijiji vingi zaidi.

Katika swali lake la pili kuhusu kupata maji kutoka Ziwa *Victoria*, sasa hivi maji yamefika Shinyanga an Serikali imemwajiri mhandisi mshauri ambaye ameshafanya usanifu wa kina kupeleka maji katika Miji Midogo ya Ushirambo, Maswa pamoja na Kishapu. Kwa hiyo, mambo yote haya tutayafanya katika awamu ya pili ya programu ya maji safi.

SPIKA: Mheshimiwa *Lake Victoria* maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, maji ambayo yamefika Shinyanga yanatoka *Lake Victoria* kwa hiyo, tumefanya usanifu wa kuyatoa

16 APRILI, 2012

maji ya *Lake Victoria* yapelekwe kwenye hiyo Miji ya Ushilombo, Maswa pamoja na Kishapu.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa mradi huu wa maji Mheshimiwa Waziri wa Maji alishatujibu hapa Bungeni muda mrefu uliopita kwamba tayari usanifu wa kina umeshakamilika hadi kufika Kishapu na Maswa na tukakubaliana kuwa baada ya Maswa mradi huu wa maji utaenda Mwandoya Makao Makuu ya Jimbo la Kisesa.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kujua huu mradi wa Maswa na Kishapu unakamilika lini ili sasa usanifu uanze wa kutoka Maswa kwenda Kisesa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mpina kama ifuatavyo:-

Ni kwamba nimesema kwamba tumeshakamilisha usanifu wa kina katika Miji ya Ushirombo, Maswa pamoja na Kishapu. Sasa lini kazi itaanza, hiyo kazi imeshaanza kwa sababu tumeshafanya usanifu.

Sasa awamu ya pili ya kuanza kujenga miundombinu, hii tutaifanya katika awamu ya pili ya programu, ambayo tutaanza mwaka 2013 na

16 APRILI, 2012

baada ya hapo tutaona uwezekano wa kupeleka maji katika Miji mingine.

MHE. ZABEIN M. MUHITA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa hili tatizo la maji la Kishapu linafanana sana, sana, sana na tatizo sugu la maji katika Jimbo la Kondo la Kaskazini.

Je, Serikiali itatoa msaada gani kuwezesha uchimbaji wa visima virefu ili wananchi wa Jimbo la Kondo la Kaskazini nao wanufaike na wanawake wapunguziwe adha ya kutafuta maji? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Muhita kwa niaba ya Waziri wa Maji kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba niseme tu kwamba suala la kuchimba visima virefu au vifupi inategemeana na utafiti na yale maji kwamba yapo chini ya ardhi.

Kwa hiyo, katika awamu ya kwanza, tumeanza na Vijiji ambavyo Halmashauri ya Kondo iliamua ifanye, sasa kama kuna Vijiji katika Jimbo la Kondo la Kaskazini havikuwemo kwenye ile awamu ya kwanza, tutavifanya katika awamu ya pili. Sasa usanifu ukifanyika ndiyo tutaainisha kwamba tuchimbe visima virefu au vifupi. *(Makofi)*

16 APRILI, 2012

Na. 55

Hitaji la Maji – Dar es Salaam

MHE. IDDI M. AZZAN aliuliza:-

(a) Je, ni lini hasa wananchi wa Dar es Salaam watapata maji safi na salama?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga bomba la maji toka Mto Rufiji kuja Dar es Salaam?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Iddi Mohamed Azzan, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali imeanza kutekeleza mpango maalum wa kulipatia maji Jiji la Dar es Salaam. Chini ya mpango huo, vyanzo vya maji vya Ruvu Juu na Ruvu Chini vitapanuliwa, bwawa la Kidunda litajengwa na visima 20 vitachimbwa katika Bonde la Kimbiji na Mpera na kujenga miundombinu ya maji. Miradi hiyo itaongeza wingi wa maji yatakayosambazwa kutoka lita milioni 300 kwa siku za sasa hadi lita 710 kwa siku.

16 APRILI, 2012

Matarajio ni kwamba mpango huu utakamilika mwaka wa fedha 2013/2014.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kujenga bomba la maji kutoka mto Ruvu kwa sababu vyanzo vilivyodainishwa vya mto Rufiji na visima katika bonde la Mpera na Kimbiji vinakidhi mahitaji ya Jiji la Dar es Salaam hadi mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada mipango ya uboreshaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam kukamilika upatikanaji wa huduma ya maji utakuwa umeboreshwa na wananchi watapata maji ya uhakika. Hivyo suala ya matumizi ya maji ya Mto Rufiji kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam katika mipango yake ya muda mrefu zaidi zinaweza kufanyiwa utafiti.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa ahadi hizi za kutatua tatizo la maji Dar es Salaam zimekuwa zikitolewa mara nyingi na kila mara tunaambiwa tatizo hili litaisha, ilianza 2009 ikaja 2013 mpaka leo tatizo bado lipo. Je, Mheshimiwa Waziri unalihakikishaje Bunge hili kwamba hii ahadi ya mwaka 2013/2014 Jiji la Dar es Salaam litapata maji kama itakuwa sasa ni ya ukweli? *(Makofi)*

16 APRILI, 2012

Swali la pili, katika majibu yako umesema kwamba maji haya ambayo mnatarajia kuyapata hivi sasa baada ya kutengeneza Kidunda pamoja na visima vya Kimbiji, yatatosheleza hadi 2025 na kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam linaendelea kupanuka na itakapofika mwaka huo wa 2025 inakadiriwa kuwa watu takribani milioni 10.

Je, huoni kwamba Serikali haioni kwamba kuna umuhimu sasa wa kuanza kujenga angalau kwa awamu bomba la maji kutoka Mto Rufiji kuleta Dar es Salaam kama ilivyokuwa maji ya kutoka Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na Kahama? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nikuhakikishie kwamba ahadi ambayo tumekuwa tunaelezea kwamba maji kwa Dar es Salaam ifikapo December, 2013 inatekelezeka kwa sababu hatua mbalimbali tumeshazianza. Tumeshianza kujenga Ruvu Chini tayari mkandarasi yuko pale na asilimia 33 ya kazi imeshafanyika.

Kwa hiyo tunachoanza sasa hivi tunaanza kuajiri mkandarasi wa kujenga bomba kuu la kutoa maji kutoka Ruvu Chini mpaka Dar es Salaam. Upande wa Ruvu tayari usanifu umeshianza na tayari tumeshapata fedha kutoka Serikali ya India.

16 APRILI, 2012

Kwa hiyo nina uhakika na Kimbiji sasa hivi ndiyo tunataka kuajiri mkandarasi wa kuanza kuchimba. Kwa hiyo hatua mbalimbali zinaendelea.

Kwa hiyo kwa mipango yote hii na kama tulivyosema Serikali imeshji-*commit* imeweka mpango maalum karibu dola bilioni 653 Serikali imeshatenga kwa ajili ya kutatua matatizo ya Jiji la Dar es Salaam. Kwa hiyo fedha hizi ni nyingi na nina kwamba suala hili litakamilika.

Swali lako la pili kuhusu kuanza kujenga awamu kwa awamu. Naomba niombe Mheshimiwa Mbunge tukubaliane tu kwamba kwanza tufanye kazi moja hii ambayo tumeshalanza. Tutakapoimaliza hii sasa tunapoanza kufikiria namna Dar es Salaam inavyopanuka ndiyo tuanze kuangalia *option* mbalimbali. Tunaweza tukafikiria maji kutoa Rufiji tunaweza kufikiria mambo ya *desalination* na vitu vinawezekana.

Na. 56

Hitaji la benki ya Wanawake, Mkoa wa Mwanza

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA (K.n.y. MHE. MARIA I. HEWA) aliuliza:-

16 APRILI, 2012

Mkoa wa Mwanza ni miongoni mwa mikoa yenye watu wengi hususan wanawake:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni muda muafaka wa kuanzisha tawi la benki ya wanawake katika Mkoa wa Mwanza?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulijibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Benki hii ambayo ilifungua milango yake tarehe 28 Julai, 2009 bado inajiimarisha ili iweze kufungua matawi mengine mikoani ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Mwanza. Kwa kuzingatia hilo benki imejiwekea mikakati ya muda mfupi na muda mrefu. Mikakati hiyo inaonyesha jinsi benki itakavyojipanua na kukuza mtaji wake ili iweze kufungua matawi mengine mikoani. Kufuatana na kanuni za Benki Kuu inatakiwa kuwa na mtaji wa shilingi 18 bilioni ili iweze kufungua matawi mengine.

Hadi sasa benki hii ina mtaji wa shilingi 4.8 bilioni zikiwemo bilioni 2 zilizotolewa na Serikali. Ahadi ya Serikali ni kuendelea kuipatia benki hii shilingi bilioni 2 kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano. Hata hivyo mipango ya baadaye ya benki hiyo ni

16 APRILI, 2012

kufungua matawi mengine mikoani ili wananchi wengi zaidi waweze kufikiwa na huduma ya benki hii.

MHE. LOLENSIA J. M. BUKWIMBA: Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jibu lake zuri. Lakini vile vile ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ahadi ya Serikali ni kuipatia benki hii ya wanawake shilingi bilioni 2 kila mwaka na hata hivyo, mpango huu unasua sua kwa sababu ilifanikiwa kutoa bilioni mbili mwaka 2010 tu.

Ningependa kujua sasa ni nini mkakati wa Serikali kuweza kuipatia benki hii bilioni mbili mbili kila mwaka ili iweze kufanikisha azma yake ya kufungua matawi mengine katika mikoa mingine hata mkoa wa Mwanza na mikoa mingine?

Swali la pili, kwa vile katika mkoa wa Mwanza wanawake wengi wanajishughulisha sana na biashara ndogo ndogo lakini hawana mtaji wa kuwawezesha kuweza kufanya biashara hizi. Ningependa kujua sasa mkakati wa Serikali kwamba inajipanga vipi kuweza kuwasaidia wanawake hawa ili waweze kupata mitaji wakiwemo wanawake wa Geita na jimbo la Busanda kwa ujumla? *(Makofi)*

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, ni kweli ahadi ya

16 APRILI, 2012

Serikali tangu itolewe haijafanikisha kutoa bilioni mbili kila mwaka lakini ahadi bado iko pale pale kufuatana na vipaumbele ambavyo vinajitokeza katika Serikali ndiyo maana haikuwezekana. Lakini nia bado ipo nzuri na tunatarajia kabla ya mwaka huu kwisha tutapata bilioni mbili nyingine.

Swali lake la pili anaulizia kuhusu wanawake wa Mkoa wa Mwanza wajasiriamali ambao wangependa kupata mikopo. Ni kweli wanawake nchi nzima wakiwemo wanawake wa Mkoa wa Mwanza wanahitaji kupata mikopo. Kwanza niwapongeze sana kwa jinsi walivyohamasika kuingia kwenye ujasiriamali.

Lakini niseme tu kwamba benki ni moja ya taasisi inayotoa mikopo. Serikali imeweza taasisi mbalimbali nyingine kuanzisha mifuko mbalimbali ya kukopesha kama *Finca* na wengineo na kwamba pia tunawahamasisha sana waanzishe vikoba na waanzishe SACCOS ambazo zitawasaidia wao kupata mikopo kwa urahisi katika benki za kawaida.

Lakini ningependa pia nimpongeze sana Mheshimiwa Lolensia Bukwimba, pamoja na Mama Ibeshi Hewa kwa kazi kubwa ya kuhamasisha wanawake katika Mkoa wa Mwanza, katika

16 APRILI, 2012

kuhakikisha wanakuwa wajasiriamali wazuri.
(Makofi)

SPIKA: Ahsante. Mnihakikishie maswali yenu yatakuwa mafupi. Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mwaka huu katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake nilipata bahati ya kutembelea ile benki na kwa kweli kikwazo kikubwa ni mtaji na Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Serikali itakuwa ikiendelea kutoa bilioni mbili kila mwaka. Mtaji unaotakiwa ili kutimiza masharti ya kufungua matawi na kufikia wanawake wengi ni bilioni 18 kama utaratibu utakuwa ni huu itachukua miaka mingi sana kuwafikia wanawake wengi. Ni mkakati gani wa nyongeza ambao Serikali inao wa kuhakikisha hii benki inapanuka kimtaji mpaka kufikia bilioni 18 kwa haraka ili kuweza kuwafikia wanawake wengi zaidi? (Makofi)

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Waziri naomba majibu kwa kifupi sana.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, mkakati mkubwa ambao benki inayo wa kuhakikisha tunafikia mtaji huo ni kwamba tumeomba Benki Kuu na imeturuhusu tuanze kuuza hisa. Kwa hiyo, katika

16 APRILI, 2012

mkakati huo wa kuuza hiza tunategemea tutapata pesa nyingi na naomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge waendeleo kuamini benki hii kwa kufungua akaunti zao katika benki hii. Tunavyokuwa na wateja wengi maana yake na mtaji wetu unakuwa. Lakini wakati wa uuzaji wa hisa pia nitashukuru sana Waheshimiwa Wabunge watahamasisha jamii na wao wenyewe kununua hisa katika benki hii.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametuambia hapa kwamba benki hii iko kwenye *process* ya kuanzishwa mikoani. Kwa kuwa Zanzibar siyo mkoa, Zanzibar ni nchi, na kwa kuwa wanawake wa Zanzibar nao wana haki ya kupata huduma katika benki hii. Lakini kila siku Serikali tukiuliza hapa Bungeni inasema kwamba iko kwenye mchakato, kuanzisha benki hii Zanzibar.

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Zanzibar wakiwemo wanawake?

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu mafupi tu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, benki hii tayari ile

16 APRILI, 2012

mikakati imefikia mahali pazuri ya kufungua tawi lake katika Visiwani Zanzibar kwa sasa tayari tumeshapata nafasi ya eneo la kuweza kufungua hiyo benki. Tumepewa nafasi katika eneo la Hoteli ya Bwawani na *process* inaendelea. Aidha benki inatakiwa ilipe milioni 10 kwa ajili ya usajili kabla ya kuanza kazi. Kwa hiyo, bado tunatafuta hizo pesa ili tuendelee kumudu gharama ambazo tumetakiwa tulipe ili tufungue hilo Tawi la Benki. (*Makofi*)

Na. 57

**Malipo ya kodi (*Payee* na *Income Tax*) kwa
Watumishi Zanzibar**

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO

aliuliza:-

Malipo ya kodi ya *Payee* na *Income Tax* hulipwa kwa ajili ya kusaidia Serikali katika utoaji wa huduma mbalimbali kwa Watumishi wa Umma au sekta binafsi sehemu walipo:-

(a)Je, kwa nini watumishi wa Taasisi za Muungano na Makampuni kama vile ya simu wanaofanya kazi upande wa Zanzibar hulipa kodi hizo Tanzania Bara badala ya Zanzibar ambapo ndio wanapata huduma hizo zilizokusudiwa?

16 APRILI, 2012

(b)Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutoa huduma kwa watumishi hao ambao kodi zao hulipwa kupitia Serikali ya Muungano ni unyonyaji. Je, ni lini Serikali ya Muungano na ile ya Mapinduzi Zanzibar zitakaa na kumaliza tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos Nyimbo, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba watumishi wa Taasisi za Muungano na Makampuni wanaofanya kazi upande wa Zanzibar hulipa kodi ya mapato kwenye Hazina ya Serikali ya Muungano badala ya Zanzibar ambako ndiko wanakopata huduma.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977kodi ya mapato ni kodi ya Muungano.

Aidha, kifungu cha 81(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato kinamtaka mwajiri kuzuia kodi ya mapato ya wafanyakazi anaowalipa mishahara na mapato

16 APRILI, 2012

mengine yatokanayo na ajira kwa kiwango kilivyoainishwa na kuwasilishwa kwa Kamishna wa Kodi ya Mapato, Tanzania. Suala hili ni la kikatiba na kisheria na wala siyo la kinyonyaji.

(b)Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba muafaka wa kulirekebisha jambo hili umeshafikiwa kwenye Kamati ya pamoja ya Masuala ya Muungano na inapendekezwa kwamba Sheria ya Kodi ya Mapato (*PAYEE*) ifanyiwe marekebisho ili kodi za wafanyakazi wa Muungano waliopo Zanzibar walipe kodi pale wanapapata huduma.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha imeandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri ili litoe ridhaa ya mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332. Baada ya mapendekezo hayo kuridhiwa Muswada wa marekebisho hayo utawasilishwa Bungeni mapema iwezekanavyo. (*Makofi*)

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:
Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa ruksa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumwuliza maswali mawili.

16 APRILI, 2012

Je, uamuzi wa kurekebisha Sheria ya mapato ya PAYEE ya Muungano ni ya kudumu au ni ya muda mfupi?

Swali langu la pili, je marekebisho haya yanawalenga wafanyakazi wale wa Zanzibar kwa sasa pamoja na wale watakaopatiwa uhamisho kwa baadaye?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Spika, muafaka huo ukishafanywa kuwa Sheria utakuwa wa kudumu mpaka Sheria hii ifanyiwe marekebisho au kufutwa. Hata hivyo kwa sababu tunakwenda kwenye mchakato wa Katiba na masuala haya ya kodi yamo kwenye Katiba. Nafikiri tukipata mabadiliko katika Katiba mpya suala hili pia litabidi libadilike linavyoendeshwa hivi sasa.

La pili kuhusu suala je ni wafanyakazi wa sasa tu au na wa baadaye? Wakati Sheria hii itakuwa inafanya kazi basi ni budi itawahusisha wa sasa na wanaokuja baada ya kutolewa taarifa zinazohusika. *(Makofi)*

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Nakushukuru Mheshimiwa Spika hasa kwa safari yako ndefu na ukarejea bado una uwezo. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwa mujibu wa maelezo yake ni

16 APRILI, 2012

kwamba ni Katiba ya Muungano ndiyo iliyokuwa ikitudhalilisha siye Wazanzibar na ndiyo sababu kodi hii haiwezi kufutwa mpaka Katiba mpya itakavyotokea. Je, Serikali inakubali kama maonevu haya yalikuwa yanakuja upande mmoja tu kwa Zanzibar?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Spika, nilichokiri ni kwamba hili suala limepatiwā ufumbuzi na kurekebishwa na pia nilisema katika jibu langu la msingi kwamba katiba ni kitu ambacho tulikubaliana na kitu ambacho ukishakikubali hakiwezi kikageuka kikawa ni unyonyaji au vinginevyo.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kodi ya Mapato ya wafanyakazi ni moja tu ya kero za kikodi ndani ya Muungano. Je, kero nyingine zitapatiwa suluhisho lini?

SPIKA: Hilo swali lako jumla kabisa maana ziko nyingi. Hebu jibu Mheshimiwa kwa kifupi hizo zingine kwa ujumla wake. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA): Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba mambo mengi ambayo yameorodheshwa kwenye kero za Muungano yanahusu kodi pia. Hili ni moja

16 APRILI, 2012

tu. Lakini pia ni hatua katika safari ndefu ambayo inaendeshwa. Kwa hiyo, naamini majadiliano bado yanaendelea kwenye Tume hii, kwenye Kamati ya pamoja na itafikia mahali matatizo haya yatatoweka. Ahsante.

Na. 58

Hiza za Kampuni ya Zain Kutopelekwa Kwenye Soko la Hisa

MHE. SAID A. ARFI aliuliza:-

Je, kwa nini Hisa za Kampuni ya *Zain* hazikupelekwa kwenye Soko la Hisa la Dar-es-Salaam (*DSE*) na kuuzwa kwa Watanzania, badala yake zikauzwa kwa kampuni ya *Airtel* kinyume na Sheria inayotaka hisa hizo ziuzwe kupitia Soko la Hisa?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Airtel Tanzania Ltd.*, ambayo ilikuwa ni kampuni ya *Zain Tanzania* hisa zake zilichukuliwa na *Celtel Tanzania BV* ambayo ni kampuni tanzu ya *Zain Africa BV* ambao Novemba mwaka 2010 ilinunuliwa na hivi sasa imebadilishwa jina na kuitwa *Airtel Tanzania Limited* kuanzia Novemba 2010, ilikuwa ikimilikiwa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania na Kampuni ya *Celtel Tanzania BV* tangu mwaka 2004. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali ina hisa 40% katika Kampuni ya *Airtel Tanzania Limited* ambayo, awali ilikuwa Kampuni ya *Zain Tanzania* na Kampuni ya *Celtel Tanzania BV* inamiliki 60% ya hisa.

Celtel Tanzania BV ni Kampuni tanzu ya *Zain Africa BV* ambayo Novemba 2010 ilinunuliwa na *Bharti Airtel International (Netherlands) BV (Bharti)*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo niliyoyatoa hapo juu, utaona kwamba, Kampuni ya *Bharti* haikununua hisa za Serikali bali ilinunua hisa za Kampuni Mama ya *Celtel Tanzania BV* iitwayo *Zain Africa BV* iliyoandikishwa nchini Netherlands. Hisa za Serikali asilimia 40 katika Kampuni ya *Zain Tanzania Limited* ambayo hivi sasa inaitwa *Airtel Tanzania Limited*, zipo palepale hazijabadilika. Hivyo, wakati utakapowadia kwa Serikali ya Tanzania kuuza hisa zake kwa wananchi, ninaamini utaratibu utawekwa

16 APRILI, 2012

kulingana na Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo ili kuwapatia fursa Wananchi wa Tanzania kununua hisa hizo au hata nyingine zitakazokuwepo.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa maelezo ya utangulizi yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri ni tofauti na haya ambayo amenipa na sijui ni kwa nini hakutaka kuelezea historia ya kuwepo kwa Kampuni hii ya *Zain* na kuanzishwa kwa Sheria ya Mawasiliano?

Kwa kuwa Bunge hili Tukufu mwaka 2009 lilipitisha Sheria ya Mawasiliano na Posta, ambayo ilikuwa inazitaka Kampuni zote za Simu ziwe *listed* katika Soko la Hisa la Dar es Salaam ili Watanzania waweze kumiliki...

SPIKA: Naomba maswali yako yawe mafupi kusudi wengi waulize maswali, maana naona unasimulia historia hapo sasa. Haya, tuendeleo.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, ili waweze kumiliki kwa nini mpaka sasa hivi makampuni hayo hayaja-*list share* zao katika Soko la Hisa la Dar es Salaam?

Sheria hiyo pia inayataka Makampuni yawe na ubia na Watanzania; ni kwa nini Kampuni

16 APRILI, 2012

ya *TIGO* inamilikiwa na wageni kwa asilimia 100?
(*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba nijibu mwaswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Arfi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria inayotaka Makampuni yawe *listed* kwenye Soko la Hisa kama anavyosema, haipo hivyo. Sheria ya *EPOCA* ya mwaka 2010 iliyopitishwa hapa imetoa kibali kwa Mashirika ya Simu yaweze ku-*list* kama yataweza na imetoa kibali kwa Mheshimiwa Waziri, kuweza kukubaliana na Mashirika yenyewe kujua ni kiasi gani hisa ziwe za Watanzania na hisa nyingine ziwe za nje. Kwa hiyo, kuna utaratibu maalum ambao unatumika kuhakikisha kwamba, hisa zinakuwa zimewekwa katika Soko la Hisa. Kwa hivyo, ni lazima kwanza *Capital Market Authority* iwe imeridhia kwamba, Kampuni hii inastahili kuwa *listed* kwenye *Stock Exchange*. Haya ni mambo ya kitaalamu na huwezi kuweka kila Kampuni kwenye *Stock Exchange* kwa sababu watu wanaokwenda kununua hisa pale ni wananchi wa kawaida na ni lazima hela zao zilindwe.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba kwa nini *TIGO* inamilikiwa; ni kutokana na Sheria hiyo hiyo ya *EPOCA* ambayo tuliipitisha hapa Bungeni; inampa mamlaka Waziri kujadiliana na Makampuni husika, kuona ni kwa kiasi gani Watanzania wanunue katika hisa za *TIGO* au katika Kampuni nyingine.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, ninalirejea swali la Mheshimiwa Arfi.

SPIKA: Lakini haitakiwi kurejea.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, Kampuni zote za Simu Tanzania, kwa mujibu wa Sheria, zinapaswa kumilikiwa sehemu ya hisa zake na *local* Watanzania. *Vodacom* ina *locals*, *Airtel* ina *locals*, *Zantel* ina *locals*, *TIGO* asilimia 100 ya hisa zinamilikiwa na wageni. kabla ya hapo *TIGO* ilikuwa na hisa za Serikali. Mwaka 2005, wiki moja kati ya uchaguzi na kuapishwa kwa Rais Mpya, hisa zile zikauzwa kinyemela.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali imeiachia Kampuni ya *TIGO* iendelee ku-*operate* bila kufuata Sheria; na Sheria ya Mawasiliano inataka Kampuni zote, wawe *local share holders* au *foreign share holders*; ziwe *listed* kwenye Soko la Hisa; na kampuni zote zinapata faida isipokuwa baadhi ya

16 APRILI, 2012

makampuni hata hayaonekani katika orodha ya walipa kodi wakubwa?

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali hai-*enforce* Sheria ya Mawasiliano kuhakikisha kampuni za simu zinakuwa *listed* kwenye soko la hisa ili tuweze kupata thamani yake na walipe kodi inavyotakiwa?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda nimjibu Mheshimiwa Zitto Kabwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nirejee katika jibu langu la msingi na nimwombe Mheshimiwa Zitto, akaisome upya Sheria ya *EPOCA* ya Mwaka 2010 na Kanuni zake zote za Mwaka 2011. Akishasoma aje aulize hilo swali tena kama kweli ni lazima ziwe *listed*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kwamba, kuweza ku-*list* kampuni katika *Stock Exchange* kuna taratibu zake. Kwanza, kuna *Capital Market Authority* ambayo ni lazima ijiridhishe kwamba, Kampuni hiyo ikiwa *listed* kwenye *Stock Exchange* itakaa pale na kwamba, hela za wawekezaji watakaokwenda pale zitakuwa salama. Sasa huwezi kuweka kila kampuni kwenye *Stock Exchange* kama haijakidhi vigezo ambavyo vitawezesha wawekezaji

16 APRILI, 2012

pesa zao kuwa salama. Nimwombe Mheshimiwa Zitto, tukitoka hapa nikamwoneshe ile Sheria na anioneshe kama kuna sehemu inaposema kwamba ni lazima ziwe *listed* kwenye *Stock Exchange*.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia majibu mazuri tu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Ukilitazama hili suala, ndani yake kuna mambo ambayo wenzetu wanasema yanaweza yakawa na ukweli wa aina fulani na ni muhimu sana kwa Serikali yetu kufanya kazi kwa uwazi. Kwa hiyo, kwa niaba ya Serikali, tutalifuatilia vizuri na kutoa taarifa kamili itakayoondoa kabisa utata kuhusu suala hili. *(Makofi)*

Na. 59

Mpango wa Kilimo wa SAGCOT

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU aliuliza:-

Je, ni sababu zipi zilizofanya Mikoa ya Lindi na Mtwara kutokuwepo katika Mpango wa Kilimo wa SAGCOT ikiwa nayo ni Mikoa ya Kusini?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mpango wa *Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT)*, unalenga kuwa na ubia wa Kimataifa kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma (*International Public – Private Partnership*), unaolenga kuongeza tija ya uzalishaji katika kilimo. Ubia huu ulizinduliwa katika Kongamano la *World Economic Forum on Africa* lililofanyika Mjini Dar es Salaam, mwezi Mei 2010. Wabia wa *SAGCOT* ni pamoja na Serikali, Wafanyabiashara, Sekta Binafsi, Wakulima na Washirika wetu katika maendeleo.

Mheshimiwa Spika, *SAGCOT* ni Mradi ambao umeandaliwa kwa misingi ya KILIMO KWANZA ambao unalenga kubadilisha kilimo kutoka kilimo cha kujikimu na kukifanya kuwa kilimo cha kibiashara, ambapo sekta binafsi itawekeza takriban *USD billion 2.1* wakati Sekta ya Umma nayo itawekeza *USD billion 1.3* katika kipindi cha miaka 20.

Mheshimiwa Spika, matarajio ya utekelezaji wa *SAGCOT* ni pamoja na yafuatayo: Hekta 350,000 zitaendelezwa kwa kilimo cha kisasa na kuzalisha mazao yatakayouzwa ndani na nje ya nchi; zaidi ya

16 APRILI, 2012

wakulima 10,000 watalima kilimo cha kibiashara na kutumia miundombinu ya umwagiliaji; ajira mpya 420,000 zitatengenezwa na kuondoa umaskini kwa watu 2,000,000; na usalama wa chakula utaongezeka.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kutekeleza *SAGCOT* unazingatia upatikanaji wa miundombinu katika Ukanda huo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, punguzeni mazungumzo ndani ya Bunge.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, punguzeni itaunganisha Bandari ya Dar es Salaam, Malawi, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Aidha, wakati wa kuanzisha punguzeni ilionekana kwamba, Awamu ya Kwanza ijikite katika maeneo yanayounganishwa na Reli ya *TAZARA*, Barabara ya Kusini na upatikanaji wa umeme. Utekelezaji wa Mpango huu unafanyika katika Kongani (*Clusters*) za Rufiji, Kilombero, Ihemi, Mbarali, Ludewa na Sumbawanga. Kwa sasa, tumeanza na Kongani ya Kilombero na baadaye Kongani nyingine zitakazojumuisha Mikoa ya Mtwara na Lindi zitafuata.

16 APRILI, 2012

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri, kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Waziri haoni kwamba Mpango huu ni muhimu ukashirikisha Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma kwa sababu huwezi kuitaja *Southern Corridor* bila ya Mikoa hiyo? (*Makofi*)

(ii) Katika majibu yake ameanisha kwamba, baadaye; sisi hatutaki baadaye, atuambie ni lini tutashirikishwa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mangungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mpango huu kama nilivyoeleza, unatekeleza KILIMO KWANZA; ni *selective approach*, tumeanza na Ukanda huo. Huwezi kuchukua fedha zote ukagawanya katika nchi nzima, zitakuwa *very thinly distributed*. Kwa hiyo, kwa sababu hiyo tumeanza na Ukanda huu na kwa sababu kupanga ni kuchagua, baada ya Ukanda huu ambao tunaona tayari sasa una miundombinu inayoweza ku-*support* kilimo pamoja na barabara na hii ndiyo dhana pana ya KILIMO KWANZA,

16 APRILI, 2012

tumeamua kuanza na Mikoa hiyo halafu baadaye tutaweka pia Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, pia hata katika Mikoa sita ambayo imepewa dhana ya kuwa Kapu la Taifa la Chakula, mbona Mikoa mitano imeunganishwa na Kigoma haimo katika *SAGCOT*. Kwa hiyo, ni kupanga tu kwamba tuanze na hapa, halafu baadaye tutakapofanya *evaluation*, tutaingiza pia Mikoa hii ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa, Mtwara na Lindi pia inatekeleza *Mtwara Development Corridor*. Kwa kifupi, huo ndiyo utaratibu tutakaoufuata ili Mikoa hiyo nayo baadaye iingizwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ni lini; mimi siwezi kumwambia ni lini, Mpango huu sasa ndiyo unianza. Kila kitu kinapoanza ni lazima kifanyiwe tathmini baadaye matokeo ya utekelezaji yatasaidia pia kupanga kongani nyingine inayofuata.

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nina swali dogo tu kwa Mheshimiwa Waziri.

Katika Mipango mingi ya Kimaendeleo Mkoa wa Lindi unaonekana kuwa wa mwisho na ndiyo

16 APRILI, 2012

maana unaitwa Mikoa ya pembezoni. Sasa hiyo Mipango ni kwa nini haianzii Lindi na kwenda maeneo mengine kwa sababu Mipango mingi ya Kimaendeleo haijafika kwenye Mkoa wa Lindi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtanda, kama ifuatavyo:-

Kuhusu kwa nini tusianzie Lindi; labda nirejee tu hapa kwenye *SAGCOT*; nimesema unapopanga Mipango, unaangalia pia hali iliyofikiwa ya miundombinu au *support services* zingine ili iweze ku-*support* Mpango unaoanzishwa. Hivi sasa Lindi na Mtwara vile vikwazo ambavyo huko nyuma vilikuwa vimedumaza maendeleo mfano, barabara na simu, mambo yale sasa yameanza kubadilika. Kwa hiyo, sasa hivi tutaanza kuona Mipango mingine inaanizishwa hata kwa Mikoa ile kwa sababu vile vikwazo vinaondoka taratibu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge, awe na subira kidogo sasa kwa sababu tunaona vikwazo vile vinaanza kuondolewa na Lindi na Mtwara nao kama ilivyo na Kigoma na Tabora, nako tutaanza kuwa tunaanzia huko.

16 APRILI, 2012

Na. 60

Kujenga Miundombinu ya Mifereji katika Bwawa la Kahama

MHE. SELEMANI J. ZEDI aliuliza:-

Serikali imekamilisha Awamu ya Kwanza ya Ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji la Kahama Nhalanga, lakini Bwawa hilo halitaweza kutumika mpaka litakapojengewa miundombinu ya mifereji ya kupeleka maji mashambani:-

- (a) Je, ni lini Serikali itajenga mifereji hiyo ili kufanikisha Kilimo cha Umwagiliaji?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa kutojenga mifereji hiyo ni sawa na kupoteza fedha zilizotumika kujenga Bwawa hilo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, lenye sehemu (a) na (b), yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipanga kujenga Bwawa la Kahama Nhalanga kwa ajili, ya kuvuna maji kwa matumizi ya kilimo cha umwagiliaji na matumizi mengine. Kutokana na ukubwa wa gharama za ujenzi wa Miradi ya aina hiyo, utekelezaji wake ulipangwa kufanyika kwa awamu. Awamu ya kwanza ilihusisha ujenzi wa bwawa lenye uwezo wa kuhifadhi maji mita za ujazo 2,356,825 ambalo sasa limekamilika.

Mheshimiwa Spika, Serikali itatenga fedha katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi huo inayohusisha ujenzi wa miundombinu ya skimu ya umwagiliaji. Aidha, tayari usanifu wa mifereji na miundombinu mingine ya shambani umekamilika kwa eneo la hekta 400 zitakazonufaisha kaya 300.

Mheshimiwa Spika, faida nyingine za bwawa hilo ni pamoja na ufugaji wa samaki, upatikanaji wa maji ya binadamu na mifugo.

Mheshimiwa Spika, namshauri Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri ya Wilaya, kuweka ujenzi wa mifereji katika mpango wao wa Maendeleo ya kilimo kama hawajaweka ili Serikali iendelee kutenga fedha za kukamilisha kazi.

16 APRILI, 2012

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri, nina swali la nyongeza.

Miaka miwili iliyopita Serikali ilitumia hela nyingi sana kujenga Bwawa hili la Kahama Nhalanga, lenye uwezo wa kumwagilia hekari 500. Kwa kipindi chote hicho umwagiliaji haujaweza kufanyika kwa sababu ya kukosa miundombinu ya mifereji ambayo ndiyo inapeleka maji mashambani. Majibu ya Naibu Waziri, yameishauri Halmashauri kuweka mipango ya ujenzi wa mifereji katika mipango yake. Nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega...

SPIKA: Mheshimiwa Susan, endelea; Mheshimiwa Mbunge huyu alikuwa anakuvuka wewe na mimi.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda nimpe taarifa Mheshimiwa Naibu Waziri...

SPIKA: Aah, uliza swali bwana!

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba, kwa kuwa sasa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, imeweka katika mpango wake utekelezaji wa ujenzi wa mifereji ya umwagiliaji na

16 APRILI, 2012

imeomba shilingi milioni 800 kutoka Mfuko wa *District Irrigation Fund – DIDF*. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anaweza kulihakikishia Bunge hili na Wananchi wa Kahama Nhalanga na Mogwa kwamba mwaka huu wa fedha, fedha hizi sasa zitapatikana, mifereji ya umwagiliaji itajengwa na wananchi wataanza kutumia bwawa hilo kwa umwagiliaji?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zedi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Kahama Nhalanga, limejengwa kwa awamu kulingana na gharama yake. Bwawa lenyewe lina gharama ya shilingi bilioni 1.14 na ndiyo maana tunalijenga kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Habari njema ni kwamba, Kikao cha *DIDF* kilichoketi mwezi mmoja uliopita au wiki tatu zilizopita, tayari kimeidhinisha shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa mifereji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitoa tu kwamba, tuendeleo kuweka katika mipango ya maendeleo ili baadaye katika miaka mingine, kama kuna viporo visije vikasahauliwa, lakini tayari tumetenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya Mradi huo.

16 APRILI, 2012

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa tatizo la Nhalanga linalingana kabisa na Korogwe Vijijini hasa katika Bonde la Mkomazi. Je, Serikali imetenga kiasi gani cha pesa cha kukarabati miundombinu ya Mkomazi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwamba, Korogwe ni sehemu ambayo tumeiwekea maanani na kwa bahati nzuri, pamoja na upatikanaji wa fedha za Serikali kuwa siyo mkubwa sana, nilimshauri Mheshimiwa Ngonyani baada ya kuwasiliana na mimi tukauweka Mradi ule katika Mpango wa *Tanzania Japan Food Counterpart Fund*. Napenda niwaarifu kwamba, Serikali ya Japani imeshatuidhinishia sasa shilingi bilioni 8.9 kwa ajili ya Miradi ya Umwagiliaji, Kilimo cha Kawaida, Miradi ya Barabara za Mashambani na kati ya hizo shilingi milioni 300 zimetengwa kwa ajili ya Mradi huo wa Mkomazi ambao alikuwa anaufuatilia Mheshimiwa Ngonyani.

SPIKA: Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Naomba pia nitumie nafasi hii, kwa sababu fedha hizi ni nyingi na Miradi ni 30...

16 APRILI, 2012

SPIKA: Nafasi hapana utapata nyingine, wewe umejibu swali wamepata 300 basi, naomba tuendelee na maswali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Nasema kwa faida ya Bunge lakini.

SPIKA: Hapana nafasi haitoshi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Haya.

Na. 61

Rasilimali Zilizoko Hifadhi ya Kigosi

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI aliuliza:-

Wananchi wa Bukombe wanaoishi katika vijiji vinavyopakana na Hifadhi ya Kigosi hawanufaiki na rasilimali hizo:-

Je, Serikali itahakikishaje kuwa wananchi wananufaika na rasilimali hizo?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la kaka yangu, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela

16 APRILI, 2012

Kanalwanda Kahigi, Mbunge wa Bukombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Wilaya ya Bukombe wananufaika kutokana na rasilimali zilipo katika Pori la Akiba la Kigosi kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori ya 2009. Shughuli zinazoweza kufanyika ndani ya Pori hilo na kuingiza mapato Serikalini ni pamoja na uwindaji wa kitalii na utalii wa picha, japo wenyewe bado upo kwa kiwango kidogo sana.

Pori la Akiba la Kigosi lina Vitalu; *Kigosi Game Central* na *Kigosi Game Reserve North* ambavyo vyote vinamilikiwa na Kampuni ya *Malagarasi Hunting Safaris*. Vitalu hivi vimekuwa vikinufaisha Wananchi wa Halmashairi ya Wilaya ya Bukombe kwa kutoa gawio la asilimia 25 ya mapato yanayotokana na uwindaji wa kitalii. Hata hivyo, kuanzia mwaka 2008, Kampuni ya *Malagarasi Hunting Safaris* haikuweza kutumia vitalu hivyo kwa kiwango kinachostahili kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mtikisiko wa uchumi duniani na uvamizi wa mifugo. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2007 – 2012, Wilaya ya Bukombe ilipata kiasi cha shilingi 8,917,140 ambazo kwa mujibu wa mwongozo uliotolewa na Wizara yangu, asilimia 60 zilitumika kwa Miradi ya Maendeleo na asilimia 40 kwa ajili ya kuendeleza hifadhi.

16 APRILI, 2012

Shughuli nyingine zinazochangia mapato ya wananchi kutokana na Pori la Kigosi ni ufugaji wa nyuki. Shughuli hizi huzalisha asali na nta ambazo huchangia kwenye mapato ya wananchi na vikundi vya wananchi. Hadi sasa jumla ya vikundi 11 vya wafugaji nyuki vyenye wanachama wapato 961 katika Wilaya ya Bukombe, vinaruhusiwa kuendesha shughuli za ufugaji nyuki kwenye Pori hili. Aidha, uhifadhi wa pori hili umewezesha kuendelea kuwepo kwa uoto wa asili ambao unachangia kupatikana kwa mvua, vyanzo vya maji, kupunguza kwa hewa ukaa na hivyo kupunguza madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Wananchi wananufaika kutokana na mvua ambazo ni muhimu kwa shughuli zao za kilimo.

MHE. PROF. KALIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nina maswali mawili, lakini kwanza ningependa kueleza masikitiko yangu kwamba....

SPIKA: Uliza swali bwana masikitiko baadaye.
(Kicheko)

MHE. PROF. KALIKOYELA K. KAHIGI: Kwamba, jibu halikuridhisha kwa sababu hatujui kwa nini wananchi wanapata tu shilingi 8,900,000 kwa kipindi cha miaka mitano.

16 APRILI, 2012

SPIKA: La kwanza tayari; kwa nini wanapata milioni nane tu. La pili?

MHE. PROF. KALIKOYELA K. KAHIGI: Naomba niulize.

SPIKA: La pili sasa uliza. La kwanza kwa nini wanapata milioni nane kila wakati? Naomba uulize swali la pili Mheshimiwa ndiyo utaratibu.

MHE. PROF. KALIKOYELA K. KAHIGI: Swali la pili ni kwamba; Serikali itaandaa lini mpango mkakati wa kukuzwa uwindaji wa kitalii ambao utawanufaisha Wananchi wa Bukombe, Kahama na Urambo kikweli kweli badala ya milioni nane na laki tisa kwa miaka mitano? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu wewe huna Naibu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kwamba, kiasi ambacho wanapata wananchi kutokana na uwindaji wa utalii ni kidogo sana kama nilivyosema. Pia kama nilivyosema kwenye jibu hilo hilo kwamba, shughuli za uwindaji kwa kiasi kikubwa hazikuweza kufanyika toka mwaka 2008 kutokana na sababu mbalimbali ambazo nimekwisha kuzieleza. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Bukombe,

16 APRILI, 2012

tushirikiane katika kuhifadhi pori kwani kwa sasa uvamizi hasa wa mifugo upo kwa kiwango cha juu sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la mkakati wa kukuzwa uwindaji wa kitalii, mwaka 2009 Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria na sasa tumekwisha kumaliza utaratibu wa ugawaji vitalu katika mfumo mpya, ambao pamoja na mambo mengine; kwa mfano, umeelekeza kwamba kila kampuni ya uwindaji lazima ichangie shughuli za maendeleo za wananchi wanaozunguka kitalu kwa kiasi kisichopungua dola elfu tano kwa mwaka. Kwa hiyo, tunategemea kwamba katika kipindi Fulani, Wilaya ya Bukombe itakuwa inapata dola elfu ishirini na tano katika kipindi cha miaka mitano cha mkataba.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa hivi vitalu pia vipo Longalembogo, Maswale na Mwamtani sehemu ya Itirima; na kwa kuwa hivi vitalu vinachukua ardhi kubwa sana; ukilinganisha vitu viwili, kwanza huku una-*conserve* yaani unahifadhi na huku unaua na hupati mapato ya kutosha:-

Huoni Mheshimiwa Waziri labda tungeachana kabisa na mtindo huu wa vitalu vya kuua wanyama

16 APRILI, 2012

ili tuweze kutoa hiyo ardhi kwa matumizi mengine kama vile kuchunga ng'ombe? *(Kicheko)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, hifadhi hizi kwa kweli hazipo kwa ajili ya uwindaji peke yake na uwindaji wa kitalii unaofanyika lengo lake hasa ni kuondoa wanyama ambao wameshazeeeka na ndiyo maana tunawaruhusu kufanya hivyo. Tatizo la uhaba wa ardhi, ikiwemo maeneo ya malisho, sidhani kama jibu lake linaweza likatokana na kuondoa hifadhi au kufanya kitu kingine. Mimi nafikiri suala la matatizo ya malisho tuwe na mjadala mpana zaidi na kuangalia maeneo mengine badala ya kuangalia maeneo ya hifadhi, ambayo faida zake ni kubwa zaidi ya uwindaji.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Pori hili la Kigosi Moyosi lenye ukubwa wa zaidi ya kilomita elfu ishirini, linapakana na Kata za Idahina, Ulungwa, Ushetu na Ulowa na wananchi wa kata hizi hawanufaiki chochote na Pori hili la akiba ambalo biashara ya uwindaji haifai:-

Je, ni kwa nini Serikali inapata kigugumizi cha ombi la wananchi wa eneo hili kupandishwa hadhi Pori hili kuwa Hifadhi ya Taifa na baadaye na wao

16 APRILI, 2012

waweze kunufaika kama wenzao wa Kaskazini?
(Makofi)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kama nilivyomjibu Mheshimiwa Prof. Kahigi na ndugu yangu Mzee Cheyo kwamba, faida za hifadhi hizi siyo uwindaji peke yake; ukiangalia kwa Wilaya ya Kahama, eneo linalopata mvua vizuri ni hayo maeneo ya Magharibi ya Wilaya kwa sababu ya Pori hili. Kwa hiyo, faida zake siyo uwindaji peke yake.

La pili, Mheshimiwa Mbunge ameliuliza kwamba wananchi wanahitaji Pori.

SPIKA: Unajibu moja tu siyo mawili.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Kuhusu kupandishwa Pori kufanya iwe Hifadhi ya Taifa, utaratibu ni kwamba, mjadala unatakiwa kuanzia kwenye mkoa, yaani mkoa wanapitisha kwenye RCC, halafu yanakuja kama mapendekezo Wizarani. Wizarani ipo tayari na tunatamani kufanya hivyo ili kuimarisha ulinzi. Kwa hiyo, nimwombe tushirikiane katika kufanya huo mchakato ili tupandishe hadhi ya Pori hili.

16 APRILI, 2012

Na. 62

Mapato ya Hifadhi ya SELOUS

MHE. DKT. SEIF SELEMAN RASHID aliuliza:-

(a) Je, Serikali imepata mapato kiasi gani kutokana na utalii kupitia Hifadhi ya Selous katika Kata za Ruwaseni, Kipungira, Ngorongo na Ngarambe kwa mwaka?

(b) Je, Serikali imewekeza kiasi gani katika kuboresha barabara za vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashid, Mbunge Rufiji, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Tangu mwaka 2005/2006 hadi 2011/2012, Wizara ilikusanya takriban shilingi 1,992,472,000 kutokana na wanyamapori waliowindwa au kujeruhiwa katika vitalu vitano vilivyo ndani ya Pori la Akiba la Selous ambavyo ni MS1, U4, LL3, RU1, LL1 na kitalu cha eneo la wazi Tapika Ngarambe kilichopo kando ya Pori la Akiba la Selous. Kati ya fedha hizo,

16 APRILI, 2012

Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ilipata shilingi 83,359,052 zikiwa ni mgao wa asilimia 25 ya uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, katika kutambua umuhimu wa kuchangia maendeleo ya vijiji vya kata zinazozunguka vitalu vya uwindaji wa kitalii, Wizara yangu iliweka Kanuni ya Uwindaji wa Kitalii ambayo inazitaka kampuni za uwindaji wa kitalii kuchangia katika shughuli za uzuiaji ujangili, uendelezaji wa vitalu na Miradi ya Maendeleo ya Wananchi wanaoishi karibu na vitalu hivyo. Tangu mwaka 2006/2007 hadi 2010/2011, kampuni hizo zilichangia jumla ya shilingi 166,163,575 kwa ajili ya maendeleo ya wananchi Wilayani Rufiji.

MHE. DKT. SEIF SELEMAN RASHID: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Swali linasema kutaka kufahamu mapato ya Serikali kwa mwaka, jumla iliyotolewa ni miaka mitano. Vilevile swali la pili lilikuwa linazungumzia uwekezaji wa Serikali katika kuboresha barabara, jibu lililotolewa ni kuzungumzia maendeleo yote kwa ujumla.

(i) Ninaomba nimwulize Waziri katika fedha hizi zilizopatikana katika miaka yote hiyo mitano kuna eneo la wazi la Tapika na Ngarambe ambalo asilimia 25 yake inakuwa tofauti ile ya jumla ya maeneo ambayo yapo ndani ya Hifadhi ya Saleous

16 APRILI, 2012

na hivyo kufanya kiwango cha asilimia 25 kisiwe kinagawanyika, ambacho hapa Mheshimiwa Waziri hajakionesha kwa ajili ya eneo la wazi la Tapika, Ngarambe, kwa ajili ya Rufiji. Je, yupo tayari kutuambia ni kiasi gani?

(ii) Kutokana ukweli kwamba wawekezaji hawa au wawindaji na waliowekeza katika hifadhi hizi wamechangia kiasi cha shilingi milioni 166 kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya wilaya. Je, Serikali ipo tayari kuwasaidia wale watu wa Ngarambe kwenda Kingupira ambako watumishi wa hifadhi wa maliasili ambao wanakaa pale, barabara yao na daraja likiwa bovu wanashindwa kuvuka wakati wa mvua?

SPIKA: Unajibu maswali mawili.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwa kifupi sana mchangano wa miaka nitampatia Mheshimiwa Mbunge. La pili, maeneo ya wazi yalichangiwa shilingi 19,750,000 zilizotolewa na Kampuni ya M-Frontiers, inayofanya uwindaji kwenye eneo hilo. Kuhusu kutengeneza Barabara ya Ngarambe kwenda Kingupila; ni moja ya maeneo ambayo tumeyaweka katika mipango yetu ya mwaka huu wa fedha tunaoendelea nao, lakini hii itategemea na upatikanaji wa fedha kwa sababu

16 APRILI, 2012

wakati mwingine mnaweza mkapanga lakini msifikie malengo mliyoweka.

Na. 63

***Postmortem* kwa Marehemu**

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA aliuliza:-

Je, ni sheria ipi inayoruhusu mwili wa marehemu kufanyiwa *postmortem* bila idhini ya wafiwa?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(b) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, Toleo la Marejesho la Mwaka 2002, mtu yeyote ambaye ana taarifa kuhusu kifo cha ghafla au kisicho cha kawaida au kifo cha kikatili au kifo kilichotokea katika mazingira yanayotia mashaka au aliyeuona mwili wa mtu aliyekufa lakini hajui kilichosababisha kifo cha marehemu huyo, mtu huyo anatakiwa kutoa taarifa kwa ofisa wa polisi au mtu yeyote mwenye mamlaka, ambaye naye

16 APRILI, 2012

atatakiwa kutoa taarifa ya tukio hilo kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi kilicho jirani na tukio hilo.

Taarifa hiyo inayotolewa ndiyo inayoanzisha uchunguzi wa kifo cha marehemu chini ya Sheria ya Utafiti wa Vifo, Sura ya 24. Polisi kwa kutumia fomu maalum, humtaka Daktari wa Serikali aliye katika eneo husika, kuufanyia uchunguzi mwili wa marehemu ili kujua sababu za kifo hicho. Matokeo ya uchunguzi wa kifo cha marehemu hupelekwa polisi na huwa ni sehemu muhimu ya upelelezi wa chanzo cha kifo hicho hasa pale inapobainika kuwa kifo hicho siyo cha kawaida.

Mheshimiwa Spika, katika hali isiyokuwa ya kawaida, marehemu anaweza kuwa amekufa kutokana na sababu isiyofahamika lakini ndugu wa marehemu wakawa na wasiwasi kuwa kifo cha ndugu yao kimesabishwa na watu wenye nia mbaya. Hivyo, ili kuondoa utata unaoweza kujitokeza, mwili wa marehemu hutakiwa kufanyiwa uchunguzi wa kitaalamu na daktari kwa mujibu wa sheria. Katika mazingira haya, ndugu wa marehemu huruhusiwa kuwepo wakati mwili huo unapofanyiwa uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Utafiti wa Vifo, haimzui Afisa Utafiti wa Vifo, yaani *Coroner*, katika mazingira ya aina fulani ikiwa ataona ni vyema

16 APRILI, 2012

kujua sababu ya kifo cha marehemu na bila kupata idhini ya wafiwa au ndugu, kumwelekeza daktari yeyote wa Serikali kuufanyia uchunguzi mwili wa marehemu ili kubaini chanzo cha kifuo chake. Mazingira hayo husababishwa na mambo mengi kama vile kutopatikana kwa ndugu wa marehemu katika muda mwafaka. Aidha, kuharibika kwa mwili wa marehemu ni moja ya sababu inayoweza kumfanya Afisa Mtafiti wa Vifo, kuamuru uchunguzi wa mwili wa Marehemu, yaani *postmortem*, bila kupata idhini ya wafiwa.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa mwili wa marehemu hufanywa kwa nia njema kwa minajili ya kubaini chanzo cha kifo na hatimaye sheria iweze kuchukua mkondo wake ikiwa kifo hicho kimesababishwa na mtu yeyote.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

(i) Je, iwapo mtu anaacha wosia wa kwamba kwa namna yoyote na kifo chochote kitakachohusika asifanyiwe *postmortem* nikiwemo mimi Sanya; inaruhusiwa asifanyiwe hilo?

(ii) Kwa kuwa maiti ina haki zake za msingi kama mtu alivyo hai na kuna heshima ya kidini

16 APRILI, 2012

katika maiti kulingana na imani za kidini. Je, tunao madaktari wa kutosha Tanzania au Serikali imejipangaje kupata madaktari ambao watakuwa wakiwafanyia *postmortem* wanawake, wawafanyie madaktari wanawake kwa heshima yake ya mwanamke na mwanaume kufanyiwa *postmortem* yake na mwanaume kwa heshima ya uanaume wake? Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu tafadhali.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Sanya, kama ifuatavyo:-

La kwanza, kwa mtu aliyeacha wosia; wosia wa mtu huwa unaheshimiwa ilimradi unafuata sheria. Wosia mara nyingi unakuwa wa maandishi au wa maneno, lakini lazima kuwe na mashahidi wawili ambao watausimamia wosia huo; uwe wa maandishi au usiwe wa maandishi.

Swali la pili kuhusu madaktari; hakuna sheria yoyote inayotamka wazi kwamba, daktari wa kike amfanyie *postmortem* marehemu wa kike, ni kama kwa *gynaecologists* wanakuwa wanaume na wanawake. Watu wanafanyiwa uchunguzi ilimradi anapofanyiwa uchunguzi mara nyingi kunakuwa na *nurse* ambaye anasimamia uchunguzi huo na

16 APRILI, 2012

manesi wengi huteuliwa wanawake. Kwa hiyo, hilo analolisema kwa kuwa ni ombi, sisi tutalifanyia utafiti lakini kwa sasa hivi hakuna ubaguzi wa aina hiyo.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wakati mwingine mtu anafanyiwa *postmortem* hata kama ndugu wa marehemu hawapo na hata kama wanakuwepo inakuwa taarifa sahihi za uchunguzi ambao umefanywa wa *postmortem* hawapewi. Je, ni kwa sababu gani hawapaswi kujua taarifa za matokeo ya kifo cha marehemu wao au ndugu yao mpendwa? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu, lakini hata Madaktari kama wapo wanatakiwa kujibu.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Riziki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema kwamba, wakati mwingine ndugu wa marehemu wanakuwepo wakati *postmortem* inafanyika. *Postmortem* inafanyika kuwezesha upelelezi kukamilika ili Sheria ichukue mkondo wake. Mara

16 APRILI, 2012

nyingi taarifa sahihi hazitolewi kwa wale ndugu wa marehemu ili ushahidi usije ukavuja, kwani mara nyingi huwa unaharibu ushahidi. Wakipewa ushahidi wakishavujisha ina maana upelekezi hautafanyika vizuri.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; Mheshimiwa Felix Mkosamali, atauliza swali hilo.

Na. 64

Huduma za Afya kwa Mama Wajawazito na Watoto

MHE. FELIX F. MKOSAMALI aliuliza:-

Sera ya Serikali ni kutoa huduma za afya bure kwa akina mama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mtano (5):-

(a) Je, ni kwa nini Hospitali ya Wilaya, Zahanati na Vituo vya Afya Wilayani Kibondo bado vinatoza pesa kwa watu hao?

(b) Je, ni kwa nini wananchi wanaochangia Mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*) wanapokwenda kupata huduma huambiwa dawa hakuna na kuelekezwa wakanunue katika maduka ya madawa?

16 APRILI, 2012

(c) Je, fedha hizo zinapelekwa wapi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA
ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) - (K.n.y.
WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Sera ya Afya inaekeleza kutoa huduma za afya bure kwa wanawake wajawazito na watoto walio chini ya miaka mitano katika Vituo vya Afya vya Umma na Hospitali. Kuwatoza fedha makundi yao ni kwenda kinyume na Sera ya Afya inayotekelezwa na Serikali nchi nzima. Serikali inaipokea taarifa hii kwamba, upo utozaji wa fedha kwa makundi hayo katika Wilaya ya Kibondo na kuahidi kuifanyia kazi kwa kufanya ufuatiliaji kuona ni kwa nini Wilaya hiyo inakiuka utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa Sera na Sheria za Nchi. Hatua stahiki zitachukuliwa kwa mujibu wa Sheria zilizopo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF), kwa lengo la kuhakikisha

16 APRILI, 2012

mwananchi wa kipato cha chini anapata huduma za afya bila malipo pale anapohitaji na kuongeza rasilimali fedha kwa ajili ya kugharimia huduma za afya ikiwemo dawa. Hata hivyo, Wizara inakiri kwamba, bado kumekuwa na upungufu mkubwa wa dawa kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za afya ikilinganishwa na mahitaji halisi ya jamii. Hivyo, Serikali inakiri kuwepo kwa changamoto hii na ili kukabiliana nayo, imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kuongeza bajeti ya dawa mwaka hadi mwaka.

(c) Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya Wilaya kumekuwepo na taarifa zinazoeleza matumizi yasiyokusudiwa kama kununua mafuta ya gari, posho za kujikimu, ukarabati wa majengo na kadhalika. Kuna upungufu mkubwa wa dawa kutokana na kwamba, fedha za *CHF* zimekuwa hazitumiki kwa lengo lililokusudiwa la kununulia dawa na vitendanishi.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mkosamali, swali la nyongeza.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Waziri ni kwamba nilishaleta taarifa kwamba kumekuwa na wizi unaoendelea

16 APRILI, 2012

Wilayani Kibondo. Mwaka jana wametafuna pesa za CHF milioni 76 nikaleta taarifa na hukuchukua hatua yoyote. Mwaka huu zimeliwa milioni 42 na hakuna madawa kwenye Wilaya yangu ya Kibondo. Sasa nataka majibu Serikali inachukua hatua gani na lini?

(2) Ninataka kujua kama hii Sera ya CHF ni ya utapeli au ya nini kwa sababu wamekuwa wanatoza pesa nchi nzima na tunaambiwa ni sera ya kweli na kadhalika lakini hakuna madawa? Sasa leo hii tunataka majibu sahihi.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Felix Mkosamali, wala asitumie nguvu kubwa hapa, mimi nataka nimthibitishie ni kweli anachosema na ninataka niliambie Bunge hili kwamba, tumezunguka Tanzania nzima, Mfuko huu hautumiki kama inavyotakiwa.

16 APRILI, 2012

Sasa ameniuliza ni hatua gani tunazochukua lakini amesema ni milioni 76, nimemwagiza Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma asiende Kibondo tu, bali aende Mkoa mzima, afanye utafiti, apitie, aangalie Mfuko wote Mkoa mzima na baada ya hapo tutatuma watu watakwenda Kigoma na tutachukua hatua. Hilo la kwanza.

La pili, kuna akina mama wajawazito ambao wanaendelea kulipa fedha kwa ajili ya kujifungua. Nataka kupitia Bunge hili na kupitia kwako Mheshimiwa Spika, kutoa maelekezo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, ni marufuku kwa kituo chochote cha afya au hospitali, kumtoza fedha mama mjamzito anayekwenda kujifungua katika kituo. Mfuko huu, ninaheshimu taarifa aliyoileta hapa na mimi nasubiri ikishindikana nitakwenda mwenyewe Kigoma.

Na. 65

Ujenzi wa Kiwanda cha Maboti ya Uvuvi – Mbamba Bay

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA aliuliza:-

Katika Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 Serikali iliahidi kujenga Kiwanda cha

16 APRILI, 2012

Maboti ya Uvuvi huko Mbamba Bay ili kuinua hali ya uvuvi na uchumi katika Wilaya mpya ya Nyasa:-

Je, ni lini kiwanda hicho kitajengwa na kwa thamani gani?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kapt. John D. Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali imedhamiria kujenga karakana ya ujenzi wa maboti ya uvuvi huko Mbamba Bay kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga. Karakana hii itaanza kwa ujenzi wa maboti ya mbao na hatimaye itaweza kutengeneza maboti mepesi ya plastiki, yaani *fibreglass boats*. Gharama za ujenzi wa karakana hiyo zimekadiriwa kuwa shilingi 240,000,000.00. Katika mwaka 2011/2012, Serikali imetenga shilingi 51,000,000.00 ambapo hadi sasa jumla ya shilingi 30,000,000.00 zimetolewa. Fedha hizi zitatumika kukarabati majengo ya watumishi yaliyopo kituoni hapo, kukarabati jengo la ghala lililopo ili liweze kutumika katika kuanza ujenzi wa maboti na kukarabati ofisi ili watumishi wa karakana

16 APRILI, 2012

wapate eneo la kufanyia kazi na kutunza vifaa. Hadi sasa, Wizara kwa kushirikiana na Halmashasuri ya Mbinga, zimefanya ukarabati wa jengo la ofisi na stoo kwa kuweka milango, madirisha na kupaka rangi jengo la ofisi. Aidha, hivi sasa Halmashauri ya Mbinga imekwisha kuandaa makadiri ya ujenzi (*Bills of Quantity – BoQ*), kwa ajili ya kukarabati jengo lililopo ili liwe karakana ya ujenzi wa maboti ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa karakana hii na kujenga karakana nyingine nchini hatua kwa hatua ili kuwawezesha wavuvi kuwa na vyombo bora vya uvuvi.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ambayo nimepewa sasa hivi, nina maswali mawil ya nyongeza.

Ikiwa gharama yenyewe ni ya shilingi milioni 240 kujenga ...

SPIKA: Mheshimiwa Blandes; kwa nini unakata kati yangu ya msemaji? Mheshimiwa Komba endelea!

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Ikiwa gharama yenyewe ni milioni 240 kujenga karakana na hadi

16 APRILI, 2012

sasa zimetoka milioni 30 tu tena kwa ajili ya kukarabati Ofisi:-

(i) Hivi ni lini karakana yenyewe itakuja kujengwa ikiwa mtindo wenyewe wa kutoa fedha ni huo wa milioni 30 tu? Je, hii si danganya toto?

(ii) Mradi huu ulikuwa uanze tangu mwaka jana, kwa mwenendo huu hatuoni kwamba wananchi watakuwa wanakata tamaa kwa Serikali yao wenyewe?

SPIKA: Lakini ondoa neno danganya toto kwani siyo maneno ya humu. Ninaomba uondoe yale maneno ya danganya toto.

MHE. CAPT. JOHN M. KOMBA: Nimeyaondoa!

SPIKA: Mheshimiwa Naibu, Waziri majibu. (Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Capt. John Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Moja; ni kweli kazi imeshafanyika kubainisha kiasi cha fedha kinachotakiwa kujenga kituo hicho

16 APRILI, 2012

kwa ujumla. Tunarudi palepale kwamba, tatizo linakuja kwamba uhaba ama ufinyu wa bajeti hauruhusu kupata kwa wakati mmoja jumla ya fedha zinazotakiwa; na kwa sababu hiyo nimesema kwamba, watu walioandaa mpango huu wamejaribu kuelekeza kwamba awamu za kufuata ni zipi na tushukuru tu kwamba imewezekana kwa awamu hii ya kwanza kupata hizo milioni 50 ambazo milioni 30 ndiyo zimeshatoka.

Kweli kama anavyosema kwamba, ilipaswa kuwa imeanza mwaka jana lakini nadhani upatikanaji kwa uhakika wa fedha haukuruhusu hilo lifanyike. Kwa kupitia Bunge lako hili Tukufu, nawaambia Wananchi wa Mbinga kwamba, kituo hicho kitajengwa na kitakamilika kwa sababu nia ipo palepale, tatizo linakuja katika kiasi cha fedha kinachoweza kupatikana kwa awamu. Roma haikujengwa kwa siku moja na hivyo, kuna siku kituo hicho kitakamilika na kufanya kazi iliyokusudiwa.

Na. 66

Kuandaa Sensa ya Mifugo Nchini

MHE. OMARY A. BADWEL aliuliza:-

Tanzania ni nchi inayoaminika kushika nafasi ya tatu kwa wingi wa mifugo kwa nchi za Afrika lakini

16 APRILI, 2012

hadi sasa nchi haina takwimu za uhakika juu ya mifugo yake na hivyo kushindwa kupanga mipango sahihi ya kuiendeleza sekta hii:-

(a) Je, ni lini Serikali itaandaa Sensa ya Mifugo nchini ili kuwa na takwimu sahihi za mifugo?

(b) Je, kuna mpango gani endelevu wa kuhakikisha kuwa Sensa ya Mifugo sasa inafanyika angalau kila baada ya miaka kumi?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel, Mbunge wa Bahi, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara yangu, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka za Serikali za Mitaa, imeanza maandalizi ya kufanya sensa kamili ya mifugo kwa kujumuisha kipengele kuhusu masuala ya mifugo katika Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika mwezi Agosti, 2012. Lengo la kuweka kipengele kuhusu mifugo katika Sensa ya Watu na Makazi ni kujenga msingi wa kufanya sensa

16 APRILI, 2012

kamili ya mifugo mwaka 2012/2013, kulingana na upatikanaji wa fedha.

(b) Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni mojawapo ya nchi Wanachama wa Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa, ambapo Shirika hili limetoa ushauri na maelekezo kwa nchi Wanachama kufanya Sensa ya Mifugo kila baada ya miaka kumi. Serikali yetu inajitahidi kuzingatia ushauri huu. Pamoja na kwamba, hatujaweza kufanya sensa kamili kila baada ya miaka kumi, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, imekuwa ikifanya Sensa ya Sampuli ya Kilimo inayojumuisha mifugo kila baada ya miaka mitano. Sensa ya sampuli ya mwisho ilifanyika mwaka 2007/2008, ambapo takwimu za mifugo kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu iliyotolewa mwaka 2011 inaonesha kwa sasa idadi ya mifugo nchini ni ng'ombe milioni 21.3, mbuzi milioni 15.2 na kondoo milioni 6.4. Pia, wapo kuku wa asili milioni 35, wa kisasa milioni 23 na nguruwe milioni 1.9.

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Serikali imekiri kufanya Sensa ya Mifugo kwa muda mrefu na hiyo imepelekea pia

16 APRILI, 2012

Serikali kushindwa kutoa huduma kikamilifu kwa mifugo yetu hapa nchini ikiwa ni pamoja na suala la mbegu bora, tiba na utaalamu:-

Sasa Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuliambia Bunge hili mipango yake mipya, endelevu na mizuri ya kusaidia utoaji wa huduma hizo kwa mifugo yetu hapa nchini?

(ii) Kwa kuwa Wizara hii ya Mifugo imekuwa ikihamahama kila wakati ama kwenda Wizara ya Kilimo, Uvuvi na Maji. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuliambia Bunge hili kwamba hiyo ni sababu mojawapo ya kuifanya Wizara hii kushindwa kutekeleza mipango yake mbalimbali ikiwemo suala la Sensa ya Mifugo kwa muda mrefu?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omary Badwel, kama ifuatavyo:-

Moja, ni kweli kwamba, imeshindikana kufanya Sensa ya Mifugo kwa maana ya kuhesabu kila kichwa cha ng'ombe ama mbuzi au kondoo. Kama nilivyosema, kumekuwepo na Sensa za Sampuli na Kisayansi, hizi pia zinatoa takwimu na dira inayoweza kuruhusu Serikali kupata taarifa muhimu inayohitajika

16 APRILI, 2012

kwa kupanga. Pia niseme tu kama tulivyolieleza Bunge lako Tukufu, tayari kwa sasa tuna mpango endelevu wa kuendeleza Sekta ya Mifugo na kwenye mpango huo ambao tumeshaanza utekelezaji wake, kwa awamu hii ya miaka mitano, mambo haya ya mifugo na huduma nyingine zote zinazotakiwa zipo mle. Rasilimali zitakapokuwa zinapatikana kwa uhakika, mifugo ina programu kabambe kwa sasa ya kuendeleza na kujibu changamoto zote ambazo wadau wote na wafugaji nchini wamekuwa wanakabiliana nazo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya jibu niseme tu ni kweli kwamba, kule nyuma kumekuwepo na kubebwa kwa Wizara ya Mifugo na Wizara nyingine, lakini kwa sasa pamoja na kwamba Wizara ya Mifugo ipo pamoja na Sekta ya Uvuvi, kila Sekta ina *focus* ya kutosha na ina Programu yake.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wapiga kura wake wa Bahi na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla na Taifa kwamba, mipango hii ipo, imekamilika na hatua kwa hatua kila kinachowakera wafugaji na kila kinachohitajika kufanyika hivi vyote vitaanza kufanyika iwe ni katika eneo la ugani, mafunzo na eneo la utafiti kama tulivyofanya wiki iliyopita, lakini pia katika suala zima la masoko. Kwa uhakika, kutakuwepo na msukumo

16 APRILI, 2012

wa kutosha na raslimali za kutosha kwa ajili ya changamoto hizi za wafugaji.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge ...

MWONGOZO WA SPIKA

MJUMBE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Nimesimama naomba ukae. Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na shughuli zote zimekwisha, sasa ninachopenda kusema ni kwamba; leo mmejitahidi sana kuuliza maswali mafupi mafupi, sasa mkifanya hivyo mnakuta wengi wanapata nafasi. Ninaomba muendelee hivyo. Pia Waheshimiwa Mawaziri, majibu ya nyongeza mjitahidi yawe mafupi, kwa sababu tunapata muda wa kuuliza maswali mengi. Tuendeleo kujitahidi ili kusudi tuweze kufanya kazi yetu vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, wageni tulionao na waliopo Ukumbini leo, kwanza kabisa ni Balozi wa Finland Nchini, Mheshimiwa Sinika Antilla. Huyu ni Balozi wa Finland Nchini na ameambatana na Maafisa wa Ubalizi huo hapa nchini akiwepo Mheshimiwa Eila Tiainen, huyu ni Mwenyekiti wa *Demo Finland and Left Alliance*; ambao wamekuwepo hapa na Waheshimiwa Wabunge

16 APRILI, 2012

Wanawake, kuongelea mambo yanayohusu *gender* na *violence against women*. Karibuni sana.

I hope madam Ambassador we shall meet at 11.30 in my office. (Makofi)

Halafu tunaye Mwenyekiti wa Chama cha NCCR Mageuzi Mheshimiwa James Mbatia akiambatana na Katibu Mkuu wa chama hicho Ndugu Samweli Luhuzza. Mheshimiwa Mwenyekiti, yuko wapi? Naona amechelewa kuingia, lakini yupo. *(Makofi)*

WABUNGE: Yupo! Yupo!

SPIKA: Aah, yupo! Ahsante, karibu sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

Halafu nina wageni wengine waliofika kwa ajili ya mafunzo hapa Bungeni ambao ni wanafunzi 33 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Pale mlipo msimame. Wanafunzi wa kutoka *UDOM!* Aha, ahsante sana. Karibuni tunaomba msome kwa bidii zote kwa sababu tunawategemea. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi wengine 30 kutoka Chuo Kikuu cha Tumaini, Iringa na wenyewe pia wasimame walipo. Ahsanteni sana na karibuni sana.

16 APRILI, 2012

Ninyi pia tunaomba mkazane kusoma, ndiyo matumaini ya nchi yetu. (*Makofi*)

Tunaye Katibu Mstaafu wa CCM, ambaye alikuwa Mkoa wa Arusha na nafikiri alikuwa na Mkoa mwingine, Ndugu Mohamed Mbonde, sijui amekaa wapi. Eeh, karibu sana. Huyu ni mgeni wa Mheshimiwa Mohamed Seif Khatibu. (*Makofi*)

Sasa ni matangazo ya shughuli za kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo hii Saa 7.00 mchana katika Ukumbi Na. 219 watakuwa na kikao chao.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa January Makamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo hii Saa 7.00 mchana watakuwa na kikao chao katika Ukumbi Na. 231.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Mussa Zungu anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo hii Saa 7.00 mchana watakuwa na kikao cha Kamati yao kitakachofanyika katika Ukumbi wa Msekwa C.

16 APRILI, 2012

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 7.00 mchana watakuwa na kikao chao katika Ukumbi wa Msekwa A.

Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, siku nyingine ni Mnyika, leo mwingine, Mheshimiwa Silinde David anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kuwa leo tarehe 16 watakuwa na kikao chao. Wao wanakutana Saa 8.00. Kweli iwe saa 8.00 usiku haiwekezekani! Nafikiri...

MJUMBE FULANI: Saa Mbili usiku.

SPIKA: Aah, saa mbili usiku, nilifikiri saa nane usiku. Haya mmeandika Kiingereza na Kiswahili, haya saa mbili usiku mara baada ya kuahirisha kikao cha Bunge, watakuwa katika Ukumbi Na. 219. Hawa watakaa baada ya kuahirisha kikao cha jioni katika ukumbi huo Na. 219.

Katibu wa Wabunge wa CUF Mheshimiwa Magdalena Sakaya anaomba niwatangazie Wabunge wote wa CUF kuwa wanatakiwa kuhudhuria kikao kitakachofanyika leo saa 10.00 jioni katika Ukumbi wa *Basement* hapo chini. Sasa hawa ni Wabunge wa CUF, anasema mfike bila kukosa.

16 APRILI, 2012

Pia mimi mwenyewe Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni za Bunge, nawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Kanuni leo saa. 7.00 mchana kutakuwa na kikao katika Ukumbi wa Spika.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, kuhusu Mwongozo!

SPIKA: Kuhusu Mwongozo Mheshimiwa Mpina!

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 68(7) hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa hapo hapo au baadaye kadri anavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, tumepokea ratiba ya Mkutano wa Saba wa Bunge hili linaloendelea na katika ratiba hiyo tarehe 17 mwezi wa Nne ndiyo siku ambapo taarifa ya Kamati za Bunge zinazosimamia fedha za umma inasomwa.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukikaa hapa Bungeni kwa siku 55 kujadili bajeti ya Serikali na kisha tunaletewa Taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ili tuweze kuichambua na kuona undani wa fedha tulizoziidhinisha. Kamati zetu za fedha kwa maana ya Kamati ya Fedha za Mashirika ya Umma, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa pamoja na Kamati ya Hesabu za Serikali, zote zinakwenda kuifanyia kazi ripoti hii.

Mheshimiwa Spika, lakini cha kushangaza ripoti hii ya *CAG* pamoja na ripoti za *LAAC*, *POAC* na *PAC* zinaletwa hapa Bungeni ili Bunge lako lijadili kwa siku moja kuona mapato na matumizi ya fedha zao zilivyotumika kwa niaba ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kama hili linaruhusiwa na kama haliruhusiwi ni lini Bunge hili litapewa nafasi ili liwe linajadili kwa kina fedha za Watanzania? (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kupanga ni kuchagua kwanza, lakini pili anayepanga ratiba ni Kamati ya Uongozi na wakati inapanga ratiba inaangalia mambo mengi sana, tena ilivyokuwa awali ilikuwa karibu Kamati zote twende nazo siku mbili pamoja na hizo ulizosema, lakini ikabidi tufanye mawasiliano na Serikali kwamba kipindi kile ambacho tunapaswa kujadili Mpango wa Serikali

16 APRILI, 2012

tumeongeza siku zingine kule mbele kati ya tarehe 23 – 24 Aprili.

Kwa hiyo, hivyo ndivyo tulivyopanga na uzuri kama watajipanga vizuri wakaweka mambo yale kuwa bayana na kwamba mmeweka taarifa zenu kabla ya wakati na ilikuwa muweke leo hapa mezani lakini hakuna Mwenyekiti aliyekuwa tayari ku-*table* taarifa yake. Nategemea kesho mtafanya hivyo, tunaweza kuu- *manage* muda wetu vizuri na tukafanya kazi zote kadri inavyostahili. Nakubali kwamba muda hautoshi na hilo ndilo tatizo tulilionalo katika kuangalia mfumo mzima wa Bunge, muda hautoshi. Kwa hiyo, kwa sasa ndivyo ambavyo tumepanga.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa tuna wageni halafu pia tuna kikao cha Kamati ya Kanuni, namwomba Mwenyekiti Mheshimiwa Jenista anipokee kikao hiki cha asubuhi.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama)
Alikalia Kiti*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyomsikia Mheshimiwa Spika anakwenda kuendelea na shughuli nyingine kule ofisini kwake kwa ajili ya masuala mbalimbali ya kiutendaji, basi

16 APRILI, 2012

naomba sasa tuendelee. Nitamwita Katibu atuongoze tunaendelea na hatua gani.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria
Mbalimbali wa Mwaka 2011
(*The Written Laws (Miscellaneous amendments) (No. 2) Act 2012*))**

(Kusomwa Mara ya Pili)

MWENYEKITI: Ahsante Katibu. Waheshimiwa Wabunge sasa tunaendelea na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2011 (*The written Laws (Miscellaneous amendments) (No. 2) Act 2011*)

Naomba nimwite Mwanasheria Mkuu. Mwanasheria Mkuu, mtoa hoja, naomba utoe hoja yako.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kutoa hoja kwamba Muswada uitwao Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2011 (*The written Laws (Miscellaneous amendments) (No. 2) Act 2011*), sasa usomwe kwa

16 APRILI, 2012

mara ya pili na Bunge lako Tukufu liujadili na hatimaye liupitisha kuwa Sheria kama itakavyofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawasilisha maelezo mafupi ya Muswada huu, nakuomba na ningependa kwanza kufanya zaidi ya jambo moja au mawili hivi; kwanza, ni kutoa rambirambi kwa familia zote za Watanzania wenzetu waliofiwa na wapendwa wao tangu tulipomaliza Kikao cha Tatu cha Mkutano wa Sita wa Bunge hili. Kwa namna ya pekee natoa rambirambi kwa familia ya Jenerali Mstaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Ernest Mwita Kyaro, Inspekta Jenerali wa Polisi, Haruni Guido Mahundi, Wabunge wenzetu Mheshimiwa Daktari Mary Nagu aliyefiwa na baba yake mzazi na Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, aliyefiwa na mama yake mzazi jana. Mwenyezi Mungu azipokee roho za marehemu na kikubwa zaidi atujalie sisi waja wake ufahamu wa kutosha kuhusu maisha na kifo. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine muhimu linahusu Sheria ya Mabadiliko ya Katiba iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu ambayo ni moja ya Sheria muhimu zinazowagusa wananchi moja kwa moja. Namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kufikia muafaka wa kuwa na sheria hii na kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa

16 APRILI, 2012

busara zao za kuachana na ushabiki wa kisiasa na kukubali kutungwa kwa sheria hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali kwenye jambo hili ni thabiti, nayo ni kuhakikisha tunayo Katiba Mpya, wala si marekebisho ya Katiba. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kutuongoza katika jambo hili kwa namna alivyotumia busara na hatimaye kuunda Tume itakayoratibu maoni ya Watanzania juu ya Katiba ya nchi yetu itakayoliongoza Taifa hili kwa siku za usoni. Si kazi sana kukosoa. Kukosoa ni kazi rahisi kama ilivyo kufanya kazi inayokosolewa. Kukosoa ni kazi iliyo rahisi kwa kila mtu na pengine wengi wetu tungependa kuifanya kazi hiyo rahisi kuliko kufanya ile kazi ya kukosolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba kwa kukubali kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume hii na Mheshimiwa Jaji Augustine Ramadhani na Wajumbe wote wa Tume kwa kuteuliwa na kukubali kwao kuwa Wajumbe wa Tume. Ingewezekana wao kumwambia Rais kwamba, watahiriki katika kutoa maoni kuliko kazi waliyopewa. Kazi iliyo mbele yao ni muhimu na inayohitaji matumizi ya akili na busara zao na muda wao mwingi na wakati mwingine watakatishwa tamaa kwa kauli za baadhi ya wenzetu ambao wataona kwamba mawazo yao

16 APRILI, 2012

hayapati kipaumbele au kwa matusi na kebehi zisizo na maana. Huu ni wakati tunapohitaji uvumilivu sana na wakati wa kusikiliza zaidi ili kuelewa hoja zinazotolewa hata kama hoja hizo zina vionjo vya kebehi au matusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo muhimu ni kuhakikisha kwamba tunachukua maoni yote bila kujali kama maoni hayo yanapingana na maoni yaliyozoeleka au la! Kwa nafasi ya utaalum wa sheria na mifumo ya uongozi au Katiba, nawahakikishia kwamba ofisi yangu itafuatilia kwa karibu sana hoja zitakazoibuliwa kwa kuzitolea maoni bila kujali zimetolewa na nani na sisi wenyewe kutoa maoni juu ya mambo tunayoona yana faida au yanakwamisha demokrasia ya maendeleo ya nchi yetu. Tutakuwa tayari kuisaidia Tume na kwa wakati muafaka Bunge la Katiba, ili kuhakikisha tunapata Katiba ya Jamhuri ya Muungano inayobeba utashi wa Watanzania bila kuzingatia itikadi au elimu miongoni mwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakuwa nimetenda haki ya msingi kama sitatumia nafasi hii kuitakia Tume fanaka na ufanisi katika kazi yao inayoanza tarehe 1 Mei, 2012 na itakayomalizika kwa kipindi cha miezi 18 tangu hapo. Nawataki kila la heri, afya njema, ustahimilifu na uvumilivu kwa kipindi

16 APRILI, 2012

hicho chote na nina uhakika tutapata muafaka katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada ulio mbele ya Bunge lako kama inavyoonekana katika Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) ya Kikao cha tatu cha tarehe 2 Februari, 2012 katika Ukurasa wa 88 – 97 uliwasilishwa katika Mkutano wa Sita. Hoja ilitolewa kwa kufuata Kanuni ya 69(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007 kwamba mjadala uahirishwe hadi mwezi wa Nne ili kupata fursa ya kutosha kwa Waheshimiwa Wabunge kufanya majadiliano baina yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imezingatia ushauri wa Wabunge kuhusu marekebisho yanayohusu Sheria ya Bodi ya Mikopo (*The Higher Education Students' Loans Funds, Act (CAP. 178)*). Sehemu hiyo imeondolewa katika Muswada kama inavyooneshwa katika jedwali lililowasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 84(10)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Katika sehemu (a) ya jedwali hilo sehemu za (i) – (viii) zimeondolewa katika Muswada. Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, inaendelea kuifanyia kazi Sheria ya Mikopo kwa kuwahusisha wadau wote na katika wakati muafaka tutaleta

16 APRILI, 2012

mapendekezo ya kuirekebisha sheria hiyo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ambazo zimeondolewa kwa kufuata maoni hayo ni Sheria ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma, Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Mashirika ya Umma, Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Serikali za Mitaa, Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sheria ya Mamlaka ya Mapato ya Tanzania, Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara na Sheria ya Korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria zote hizo ukiacha ile ya Korosho zinashabihiana kwa msingi kwamba zinamlenga mwanafunzi ambaye anatakiwa kurudisha mkopo wake wa elimu kwenye Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uamuzi huo sheria zilizo mbele ya Bunge lako Tukufu ni zile zinazoanzia sehemu ya IX yaani Sheria ya Uendeshaji wa Mashtaka (*The National Prosecution Service Act, (CAP. 430)*). Sehemu ya X inayohusu Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma za Kipolisi, Sura ya 322 (*The Police Force and Auxiliary Service Act, (CAP. 322)*)

Sehemu ya XI inayohusu mabadiliko katika Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168 (*The*

16 APRILI, 2012

Road Traffic Act, (CAP. 168)). Sehemu ya XII inayohusu Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Sura 96 (*The Constituencies Development Catalyst Fund, Act, (CAP. 96)*). Sehemu ya XII kuhusu Sheria ya Mapato kwa njia ya Uhalifu, Sura ya 256 (*The Proceeds of Crime Act, (CAP. 256)*), sehemu ya XIV inayohusu Sheria ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19 (*The Prevention of Terrorism Act, (CAP. 19)*), sehemu ya XV inayohusu Uhujumu Uchumi, Sura ya 200 (*The Economic and Organized Crime Control, Act (CAP. 200)*), Sehemu ya XVI inayohusu Sheria ya Kuzuia Biashara ya Dawa za Kulevya, Sura ya 95 (*The Drugs and Prevention of Illicit Traffic in Drugs Act, (CAP.95)*) na mwisho ni sehemu ya XVII inayohusu Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 (*The Evidence Act, (CAP 6)*). Marekebisho ya kwenye jedwali yanahusu Sheria hizo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza iliyopo katika ukurasa wa Saba wa Muswada inabeba Jina refu la Muswada ambalo ni Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali. Sehemu ya pili ya Muswada huu, ni ile iliyokuwa sehemu ya Tisa ya Muswada. Sehemu hii inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 18 cha Sheria ya Uendeshaji wa Mashitaka kwa lengo la kumwezesha Mkurugenzi wa Mashtaka kutoa amri, miongozo na maelekezo hayo kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa kifungu hicho kimempa tu Mkurugenzi wa Mashtaka mamlaka ya kutoa amri, miongozo na maelekezo ambayo Maafisa Waendesha Mashtaka wanapaswa kuyafuata. Hata hivyo, kifungu hicho hakielekezi kwamba, amri, miongozo na maelekezo hayo yachapishwe katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ya Muswada huu ni iliyokuwa Sehemu ya X ya Muswada. Sehemu hii inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha saba (7) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma za Polisi yaani Sura ya 322 ambacho kinampa mamlaka Inspekta Jenerali wa Polisi kutoa amri mbalimbali na jumla kwa lengo la kusimamia Jeshi la Polisi katika kutekeleza majukumu yake. Kwa sasa sheria haiweki masharti yanayoelekeza kuwa amri hizo zitangazwe kwenye gazeti la Serikali, hivyo basi, lengo la marekebisho hayo ni kuweka masharti yanayoelekeza kutangazwa katika gazeti la Serikali kwa amri hizo ili kuleta ufanisi na pia *transparency*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne ya Muswada ni ile ambayo ilikuwa ni sehemu ya XI ya Muswada, sehemu hii inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 25 cha Sheria ya Usalama Barabarani yaani Sura 168.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna ongezeko la ajali za barabarani zinazotokana pamoja na sababu zingine madereva kutokuwa makini na kuheshimu alama za barabarani. Madhumuni ya marekebisho haya yanalenga kuingiza kifungu kipya ndani ya sheria hii kinachohusu usimamizi wa leseni za udereva. Kifungu kinapendekeza kuweka utaratibu wa leseni za udereva kupewa alama maalum kwa namba na pale mwenye leseni anapotenda kosa au anapohukumikiwa kwa kosa lolote linalohusiana na uvunjifu wa Sheria ya Usalama Barabarani, basi namba hizo zitakuwa zikipunguzwa. Kuingizwa kwa kifungu hiki kipya kunalenga kuwawajibisha wenye leseni za udereva na kuwafanya wawe makini na kufuata masharti yaliyopo katika leseni zao za udereva kwa lengo la kupunguza ajali za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano ya Muswada ni ile iliyokuwa sehemu ya XII ya Muswada na sehemu hii inapendekeza marekebisho katika vifungu vya 3, 4, 21 na 22 vya Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Sura ya 99, ni Mfuko ambao unaohusu ninyi Waheshimiwa Wabunge. Marekebisho kwenye kifungu cha tatu yanalenga kupanua tafsiri ya neno "Waziri" ili kumhusisha pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa

16 APRILI, 2012

Rais masuala ya Muungano. Marekebisho hayo pia yanafanywa katika kifungu cha 4 ili kumtambua Afisa Kiongozi au Afisa aliyeteuliwa na Katibu wa Bunge kuwa Msimamizi wa Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Sehemu hii inapendekeza pia marekebisho katika kifungu cha 21 ili kuwezesha Ofisa Mfawidhi kuwa Msimamizi Mkuu wa Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo.

Mwisho, marekebisho yanapendekezwa katika kifungu cha 22 ili Afisa Mipango wa Wilaya na mmoja kati ya Madiwani waliotajwa katika kifungu cha 10(c) kuwa ndio watia saini wateule wa kundi la (a) na (b) kwa pamoja kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita ya Muswada ni iliyokuwa sehemu ya XIII ya Muswada. Sehemu hii inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Mapato kwa Njia ya Uhalifu yaani Sura ya 256. Marekebisho yanayokusudiwa yanalenga vifungu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kifungu cha tatu kinachohusiana na tafsiri ya baadhi ya maneno, mapendekezo yanayotarajiwa kurekebishwa tafsiri ya neno "*Tainted Property*" na "*Trustee*". Lengo la marekebisho haya ni kutoa tafsiri pana zaidi ili iweze kukidhi matakwa yaliyokusudiwa katika sheria.

16 APRILI, 2012

Kifungu cha tano kinafanyiwa marekebisho ili maneno “*except section 4*” yaondolewe kwa kuwa kuwepo kwa maneno hayo kunaondoa maana ya kifungu cha 4(1)(c).

Marekebisho haya yatasababisha masharti ya kifungu cha tano (5) kutumika pia katika kifungu cha 4. Marekebisho yanapendekezwa pia katika kifungu cha 12 ili kuongeza sharti lililopo kwenye kifungu cha 4(1)(c). Kwa sasa ilivyo endapo mtuhumiwa anayechunguzwa akitoroka Mahakama haina uwezo wa kutoa amri ya kufilisi mali ya mtuhumiwa inayohusika na mashtaka hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii inapendekeza marekebisho kwa kuongeza kifungu kipyua cha 13(a) ili kushughulikia watuhumiwa ambao wanafariki wakati wa uchunguzi wa uhalifu huo au baada ya kutiwa hatiani. Sharti lililopo ni kwamba katika hali hiyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kwenda Mahakamani kuomba amri ya kutwaa mali zilizotokana na uhalifu. Marekebisho ambayo yanapendekezwa yanakusudia kuipa Mahakama mamlaka ya kutoa amri ya kufilisi mali inayohusika na uhalifu ambao mtuhumiwa anayefariki au kutoroka wakati akichunguzwa au baada ya kushtakiwa Mahakamani anahusika nayo.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, inapendekezwa kufanya marekebisho katika kifungu cha 38 ili kumpa mamlaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuiomba Mahakama kutoa amri ya kuzuia mali ya mtuhumiwa wakati uchunguzi unafanyika dhidi yake kwa lengo la kumzuia kuhamisha au kugawa mali aliyopata kwa njia isiyo halali. Kifungu cha 39 kinafanyiwa marekebisho ili kiweze kutoa mwongozo ambao Mahakama itautumia katika kumteua msimamizi wa mali iliyozuiliwa wakati tuhuma zikipelelezwa yaani *trustee*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la mapendekezo haya ni mahitaji ya mikataba ya Kimataifa inayohusiana na madawa ya kulevya. Kwa mfano, *United Nations Convention Against Prevention of Illicit Traffic in drugs and psychotropic substance* wa mwaka 1978. Mkataba wa *United Nations Convention Against National Organized Crime* wa mwaka 2000, Mkataba dhidi ya Makosa ya Rushwa, *United Convention Against Corruption, 2003*. Mikataba yote hii inataka mwanachama kuchukua hatua kuhakikisha kwamba hakuna mtu yoyote atakayenufaika na vitendo vya ufisadi na kutunga sheria za kuchukua mali zinazotokana na vitendo hivyo vya ufisadi. Nchi nyingine kama Zambia, Kenya, Afrika ya Kusini zimekwishatunga sheria hizo.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya saba ya Muswada ni iliyokuwa sehemu ya XIV na sehemu hii inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19. Mapendekezo hayo yanalenga kurekebisha tafsiri ya maneno *property* na *fund* yaliyotumika katika sheria hiyo ili kutoa tafsiri inayorandana na tafsiri iliyo katika Sheria ya Mapato kwa Njia ya Uhalifu yaani Sura ya 256.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nane ya Muswada iliyokuwa sehemu ya XV ambayo inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Uhujumu Uchumi yaani Sura ya 200 ya sheria zetu. Mapendekezo hayo yanalenga kurekebisha kifungu cha 23 kinachohusu kutaifisha mali au kifaa kilichohusika au kusaidia kutendeka kwa kosa la jinai kwa mujibu wa sheria hii. Kifungu hiki kinamtambua mwenye mali aliyekutwa nayo bila kujali kuwa mali hiyo inaweza kuwa ya mtu mwingine. Marekebisho haya yanalenga kutoa tafsiri ya neno *Owner* lililotumika katika sheria ili lihusishe hata yule mtu mwingine au mmiliki, lakini asiyehusika na utendaji wa kosa la jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tisa ya Muswada iliyokuwa sehemu ya XVI. Sehemu hii inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kuzuia na Kusafirisha Madawa ya Kulevya, Sura ya 95. Marekebisho ya mapendekezo yafanyike katika

16 APRILI, 2012

kifungu cha pili, ili kutoa tafsiri sahihi ya neno *court* lililotumika katika sheria hiyo na kuonesha aina ya makosa yatakayofunguliwa katika Mahakama za Mahakimu Mkazi na Mahakama Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 12 kinahusu makosa ya kulima mmea wowote wa madawa ya kulevya ambapo maneno "*manufactured drugs*" na kifungu cha maneno "*or any preparations containing any manufactured drugs*" yanayoonekana kwenye kipengele cha (d) yako kimakosa. Hivyo, yafutwe ili kuondoa utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 16 kinahusu makosa ya usafirishaji wa madawa ya kulevya. Kifungu hiki kinarekebishwa ili kuondoa utata wa kiasi cha madawa mtu atakachopatikana nacho bila kujali uwingi. Inapendekezwa pia kuongezwa kifungu kipyua cha 17(a) kinachotoa adhabu kwa mtu anayepatikana akitumia madawa ya kulevya au umiliki wa eneo na kuruhusu eneo lake litumike kutayarisha au kuzalisha madawa ya kulevya. Kifungu hicho kinaainisha kosa la kupatikana na vifaa au zana za kuzalisha madawa ya kulevya au kushawishi mtu kutumia madawa ya kulevya au kushawishi mtu mwingine kujiingiza katika kundi na kuvuta au kutumia madawa ya kulevya.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kumi ya Muswada iliyokuwa ni sehemu ya XVII ya Muswada, sehemu hii inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 34(b) cha Sheria ya Ushahidi yaani Sura ya 16 ya sheria zetu. Kifungu hicho kinaelekeza utaratibu wa kutoa ushahidi Mahakamani kwa mtu ambaye hakuweza kupatikana na kutoa ushahidi wake ili maelezo yake yatumike kama ushahidi Mahakamani. Katika kutoa maelezo hayo yako masharti ambayo endapo yatatekelezwa basi maelezo hayo yanaweza kupokelewa Mahakamani. Miongoni mwa masharti hayo ni kwamba, kusiwepo pingamizi la kupokea maelezo ndani ya siku kumi kutoka upande mwingine tangu gusio la kutoa maelezo hayo kutolewa. Sheria kama ilivyo hivi sasa haitoi fursa kwa Mahakama kupima uzito wa pingamizi hilo linapotolewa. Lengo la marekebisho haya ni kuipa Mahakama fursa ya kupima uzito wa pingamizi linaloweza kutolewa na kisha kutoa uamuzi ama kukubali au kukataa pingamizi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, napenda kwa heshima na taadhima kupitia kwako kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuujadili Muswada huu na kuupitisha katika hatua mbili, yaani kusomwa kwa mara ya pili na kusomwa kwa mara ya tatu.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(*Makofi*)

WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali baada ya kutoa hoja na naona hoja yako imeungwa mkono kwa mujibu wa utaratibu wa kikanuni. Waheshimiwa Wabunge baada ya hoja hiyo kutolewa na kuungwa mkono kwa mujibu wa kanuni naomba sasa kwa heshima yote nimwite Mwenyekiti wa Kamati aliyefanya kazi ya kuchambua Muswada huu. Naona kwa niaba yake anakuja Mheshimiwa Lwanji kusoma taarifa ya Kamati kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

MHE. JOHN P. LWANJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Marekebisho wa Sheria Mbalimbali namba 2 wa Mwaka 2011 yaani (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 2 Act, 2011*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakavyokumbuka, Muswada wa Marekebisho ya

16 APRILI, 2012

Sheria Mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2011 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments), No. 2 Act, 2011*) uliletwa hapa Bungeni katika Mkutano wa Sita mwezi Januari/Februari, 2012 na Kamati yangu ikaweza kutoa maoni kuhusiana na Muswada huo. Hata hivyo, Bunge letu lilishauri Muswada huo ufanyiwe marekebisho na baadhi ya Vifungu hasa vinavyohusiana na Mikopo ya Wanafunzi wanaosoma katika Vyuo vya Elimu ya Juu na marejesho ya mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuipelekea Kamati yangu kazi ya kushughulikia Muswada huu kwa mujibu wa kanuni 84(1) tarehe 12 Aprili, 2012 Kamati ilikutana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Jaji Frederick Werema, Mbunge pamoja na wataalam wengine wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupata maelezo ya awali kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao hicho mtoa hoja alieleza Kamati kuwa Muswada wa Sheria ya Marekebisho wa mwaka 2011, unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria nane (8) ambazo ni Sheria ya Uendeshaji wa Mashtaka, Sura ya 430; Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma za Kipolisi, Sura 322; Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168; Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Sura 256; Sheria

16 APRILI, 2012

ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19; Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200; Sheria ya Kuzuia Biashara ya Dawa za Kulevya, Sura ya 95 na Sheria ya Ushahidi, Sura ya 16 kwa lengo la kuondoa mapungufu yaliyobainika wakati wa matumizi ya sheria hizo. Pia kuongeza masharti mbalimbali ili kuleta uwiano katika sheria zilizorekebisha pamoja na kusaidia utekelezaji madhubuti wa sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hali hiyo, Muswada huo uliondolewa Bungeni na kurejeshwa Serikalini ili kufanyiwa maboresho zaidi. Aidha, kama tulivyofahamishwa awali na mtoa hoja, hivi sasa Muswada huu umerudishwa tena ili uwasilishwe kwenye Bunge lako ikiwa vifungu vinavyohusiana na Mikopo ya Elimu ya Juu na marejesho ya mikopo hiyo vimeondolewa. Vifungu hivyo vinapatikana katika sehemu ya II hadi VIII ya Muswada yaani, Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178; Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Mashirika ya Umma, Sura ya 372; Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Serikali za Mitaa, Sura 407; Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50; Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399 na Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara, Sura ya 208.

Hivyo basi Muswada huu sasa unabakiwa na sehemu ya (I), (IX), (X), (XI), (XII), (XIII), (XIV), (XV) na

16 APRILI, 2012

(XVI) (isipokuwa XII) ambazo zina uhusiano wa karibu na Sheria ya *Anti-Money Laundering (Amendments) Act, 2012* iliyotungwa na Bunge lako Tukufu hivi karibuni ili kukabiliana na kosa la kutakatisha fedha inayopatikana kwa njia ya uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitumia uwezo wake wa kufanya marekebisho katika Muswada huu na kumshauri mtoa hoja kufanya mabadiliko hayo kama inavyoelezwa kwenye kanuni ya 84(3) ya kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nitoe maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Marekebisho Mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Kamati inashauri kuwa neno:-

- (i) Neno "may" katika Vifungu vya 24(a)(1) na 27(3) vibadilishwe na kuwa "shall". *"The orders, guidelines and instructions issued under this section may be published in the Gazette"*. Vile vile pamoja na kuwekwa kwenye Gazeti la Serikali kama inavyooneshwa kwenye Kifungu cha 24(b), ni vema taarifa hizo zikawekwa kwenye vyombo

16 APRILI, 2012

vingine vya habari kama Magazeti ili hata watu wanaokaa Vijijini na sehemu ambako Gazeti la Serikali halifiki waweze kupata taarifa hizo.

- (ii) Kamati inashauri maneno "*any Lawyer*" kama yalivyotumika kwenye Kifungu cha 25(1) yabadilishwe na kuwa "*any Legal Officer*" ili kuleta maana ya Kisheria.
- (iii) Kamati inakubaliana na Mapendekezo ya Serikali kama yalivyotolewa kwenye sehemu ya Kumi kwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma za Polisi, Sura ya 322. Kamati inaamini marekebisho yaliyofanywa ya kumpa sharti Inspekta Generali wa Polisi kutangaza na kuchapa kwenye Gazeti la Serikali amri mbalimbali anazotoa katika kulisimamia Jeshi la Polisi yataongeza ufanisi na uwajibikaji ndani ya chombo hicho muhimu cha Serikali.
- (iv) Pamoja na Kamati kukubaliana na mapendekezo ya Serikali kama

16 APRILI, 2012

yalivyooneshwa kwenye sehemu ya kumi na moja ya Muswada huu ambapo inapendekezwa kuweka utaratibu wa leseni za Udereva kupewa alama maalum kwa namba na pale mwenye Leseni anapotenda kosa, basi alama hizo zitakuwa zikipunguzwa, ni vema Serikali iangalie kwa makini suala hili kwani linaweza kuchochea rushwa kati ya Madereva na waliopewa dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Sheria hii.

Kamati inashauri kuwa, suala la kupunguza alama lifanyike Mahakamani na siyo kwa Watendaji moja kwa moja ambao hata hivyo hadi sasa ni eneo mojawapo linalolalamikiwa kwa vitendo vya rushwa. Aidha, Kamati inashauri kuwa Waziri mwenye dhamana aweke Kanuni na Taratibu za wazi zinazoeleza aina ya makosa yatakayopelekea alama kupunguzwa kwenye leseni ya Dereva.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali yaliyofanywa kwenye sehemu ya kumi na mbili ili kurekebisha Sheria ya Mfumo wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Sura ya 96. Kamati inaamini mapendekezo haya ya kupanua tafsiri ya neno Waziri ili kumhusisha Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) na marekebisho yanayofanywa katika kifungu cha (4), kwa kumtambua Afisa Kiongozi kuwa msimamizi wa Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa upande wa Tanzania Zanzibar yamelenga kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria hii kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imechambua kwa makini sehemu ya Kumi na Tatu ya Muswada huu inayopendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Mapato kwa Njia ya Uhalifu, Sura ya 256. Marekebisho yanapendekezwa kufanywa katika kifungu cha 12 ili kuondoa utata uliopo kwani ilivyo kwa sasa mtuhumiwa anapotoroka, Mahakama haina uwezo wa kutoa amri ya kufilisi mali ya mtuhumiwa huyo. Hivyo, mapendekezo ya marekebisho ni kuipa mahakama mamlaka ya kutaifisha mali iwapo mtuhumiwa anayepelelezwatafariki au kutoroka huku hukumu haijatolewa.

Aidha kwa kutumia utaalum wa Kisheria miongoni mwa Wajumbe wa Kamati, na kwa

16 APRILI, 2012

kuzingatia Ibara ya 13(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977, inayotoa misingi ya Haki na kupiga marufuku kwa mtu aliyeshtakiwa na kosa la jinai kuhesabika mkosaji kabla ya kutiwa hatiani na Mahakama. Kamati inashauri mapendekezo hayo ya Serikali yaondolewe na Sheria hii iweze kuangaliwa upya kwani mapendekezo haya yanakiuka misingi ya haki kwani kwa mujibu wa Sheria, Ushahidi kwenye Masuala ya Jinai ni kwa anayeshtaki kuthibitisha pasipo shaka (*he who alleges should prove beyond reasonable doubts*) na haiwezi kulegezwa kuwa "*balance of probabilities*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya kuipa Mahakama mamlaka ya kutoa amri ya kufilisi mali ya mtuhumiwa aliyefariki wakati akiwa anafanyiwa uchunguzi au hata baada ya kushitakiwa Mahakamani yanakiuka misingi ya haki kwa sababu mtu yeyote anapaswa kuonekana hana hatia hadi ithibitishwe hivyo pasipo shaka yeyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaaafiki mapendekezo ya Serikali kama yalivyotolewa kwenye sehemu ya Kumi na Nne inayohusu marekebisho katika Sheria ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19 ili kurekebisha tafsiri ya baadhi ya maneno kama vile "*Property*" na "*fund*" na hivyo kutoa tafsiri

16 APRILI, 2012

inayofanana na Sheria ya Mapato kwa Njia ya Uhalifu, Sura ya 256.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati inakubaliana na sehemu ya Kumi na Tano inayohusu marekebisho ya Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200 ambayo inalenga kurekebisha kifungu cha 23 kinachohusu kutaifisha mali au kifaa kilichohusika au kusaidia kutendeka kwa kosa la jinai kwa mujibu wa sheria hii. Kamati inaamini marekebisho haya yataongeza ufanisi wa Sheria hizi, katika maeneo yaliyotajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali yaliyofanywa katika Sura ya Kumi na Sita ya Muswada kwenye Sheria ya Kuzuia na Kusafirisha Madawa ya Kulevya, Sura ya 95. Mapendekezo haya yanalenga kufanya marekebisho katika kifungu cha pili (2) ili kutoa tafsiri ya neno *court* na kuonesha aina gani ya makosa yatafunguliwa Mahakama za kawaida na makosa gani yatafunguliwa Mahakama Kuu. Hata hivyo, Kamati inashauri mapendekezo yaliyofanywa kwenye kifungu cha 51 yaangaliwe upya na hasa kwenye hukumu ya kifungu cha maisha kwa mtuhumiwa aliyepatikana na hatia ya kukutwa na kiasi cha madawa ya kulevya bila kujali wingi. Kamati inashauri kwamba ili kuondoa matumizi mabaya ya Sheria hii, ni vema kuweka adhabu

16 APRILI, 2012

ndogo (*minimum sentence*) kwa baadhi ya makosa kwenye vifungu hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri maneno "*without parole remove*" yaondolewe kwenye kifungu cha 51(a) na 51(b) kwa sababu ni marudio yasiyo ya lazima kwani kwa mujibu wa Sheria ya "*The Parole Boards Act (Cap 400, R.E. 2009)*". Kifungu cha nne (4) Sehemu ya Tatu kinasema: "Mfungwa yeyote anayetumikia Kifungo cha Maisha hastaili Msamaha wa *Parole*". Aidha, Kamati inashauri kosa la "*ommission*" kama lilivyoielezwa kwenye Kifungu 51(a) liondolewe kwenye kifungu hicho na kuwekewa adhabu yake peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Sheria ya Kuzuia na Kusafirisha Madawa ya Kulevya, Sura ya 95, Kamati inashauri neno "*owner*" kama lilivyotumika kwenye Kifungu cha 52(c) libadilishwe kwani linaweza kutowatendea haki watu wengi. Hii ni kutokana na sababu kwamba si lazima mmiliki wa jengo ajue au ahusike na mambo yanayotendeka ndani ya Jengo lake iwapo yeye haishi mle ndani na huenda kapangisha jengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kama yalivyotolewa kwenye sehemu ya kumi na saba katika Sheria ya

16 APRILI, 2012

Ushahidi, Sura ya 16, ambayo yamelenga kifungu cha 34B ambacho kinaelezea utaratibu wa kutoa maelezo ya shahidi Mahakamani ambaye hakuweza kupatikana na kutoa ushahidi wake ili yatumike kama ushahidi Mahakamani. Miongoni mwa masharti hayo ni kwamba, kusiwepo na pingamizi la kupokea maelezo hayo ndani ya siku kumi kutoka upande mwingine kuanzia tarehe ya kusudio la kutoa maelezo hayo. Kamati inaungana na Serikali ili kuipa Mahakama Mamlaka na fursa ya kupima uzito wa pingamizi linaloweza kutolewa kabla ya kukubali au kukataa pingamizi lililotolewa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha Maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu, napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa kutuamini na kutupa kazi ya kufanya uchambuzi wa Muswada huu. Aidha, Kamati yangu imetafakari kwa makini na kuona umuhimu wa marekebisho yanayokusudiwa kufanyika katika Sheria hizo na hivyo kuomba Bunge lako Tukufu kwa sasa likubali kuupitisha Muswada huu ili kusomwa mara ya pili na hatua zake zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Fredrick Mwita Werema; Naibu Mwanasheria Mkuu

16 APRILI, 2012

wa Serikali, Ndugu George Masaju; Wataalam wote wa Serikali na Wadau wote waliotoa maoni yao, ambao kwa ujumla wao wameisaidia Kamati katika kufanya uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii ambao bila kuchoka na kwa kutumia utaalam wao katika Mambo mbalimbali ya Sheria na Utawala walifanya kazi hii kwa ufanisi, umakini na uvumilivu mkubwa. Naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pindi Chana, Mwenyekiti; Mheshimiwa Angellah Kairuki, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Tundu Lissu, Mjumbe; Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mjumbe; Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mjumbe; Mheshimiwa Rashidi Ali Abdallah, Mjumbe; Mheshimiwa Halima Mdee, Mjumbe; Mheshimiwa Azza Hilary, Mjumbe; Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mjumbe; Mheshimiwa Fakharia K. Shomari, Mjumbe; Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mjumbe; Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mjumbe; Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mjumbe; Mheshimiwa John Lwanji, Mjumbe; Mheshimiwa Jason Rweikiza, Mjumbe; Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mjumbe; Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mjumbe; Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mjumbe na Mheshimiwa Mohamed Said Mohamed, Mjumbe.

16 APRILI, 2012

Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Daktari Thomas D. Kasilillah, Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndugu Charles J. Mloka na Katibu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Ndugu Peter Magati na Msaidizi wa Kamati Ndugu Catherine Kitutu kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu, naomba nimshukuru sana Msemaji wa Kamati iliyochambua Muswada huo Mheshimiwa John P. Lwanji, lakini kwa mujibu wa Kanuni naomba mniruhusu nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani atakayewasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani. Namwona Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis.

MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS (K.n.y. MSEMaji MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Tundu A.M. Lissu, kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Namba 2 wa mwaka 2011 kwa

16 APRILI, 2012

mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa wanachama na wananchi wote ambao kwa moyo mmoja waliamua kufanya mabadiliko na kukichagua chama changu CHADEMA katika chaguzi ndogo zilizomalizika hivi karibuni. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani chini ya uongozi wa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman A. Mbowe kwa ushauri na ushirikiano uliowezesha maandalizi ya hoja hii. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, kwa michango yao mbalimbali wakati wa kujadili Muswada huu.

Vilevile nichukue fursa hii kumshukuru Msaidizi wa Masuala ya Kibunge, Oliver Mwikila, kwa msaada na ushauri wa kitaalam uliofanikisha maandalizi ya hoja hii. Mwisho, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru viongozi, wanachama na wapenzi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wananchi wote wa Tanzania ambao wameendelea kutuunga mkono na kututia nguvu katika kipindi hiki muhimu katika historia ya nchi yetu.

16 APRILI, 2012

Msimamo wetu ni ule ule, hakuna kulala mpaka kieleweke!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini kwa umuhimu, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao kwa nafasi zao walisimama imara hapa Bungeni na kuhakikisha marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ambayo yalikuwa yameletwa yanafutwa hadi hapo utaratibu muafaka utakapofanyika. Hongereni sana waheshimiwa wote!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kujadili mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali yaliyoko katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Inapendekezwa kwamba Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Madawa ya Kulevya, Sura ya 95 ya Sheria za Tanzania irekebishwe ili kuongeza adhabu kwa makosa kadhaa yanayohusiana na madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 51 cha Muswada kinachofanya marekebisho kwenye kifungu cha 16 cha Sheria mama, inapendekezwa kwamba, adhabu ya kosa la kupatikana na madawa ya kulevya au mchanganyiko wa

16 APRILI, 2012

madawa hayo, au la kufanya au kushindwa kufanya tendo au kitu chochote kuhusiana na madawa ya kulevya iwe ni kifungo cha maisha. Adhabu ya sasa kwa makosa hayo, kwa mujibu wa kifungo cha 16(1)(a) cha Sheria ya Kuzuia Madawa ya Kulevya, ni faini ya shilingi milioni kumi au mara tatu ya thamani ya madawa au mchanganyiko wa madawa hayo katika soko au yoyote iliyo kubwa zaidi katika faini hizo, au kifungo cha maisha au vyote viwili, yaani kifungo cha maisha na faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapendekezwa pia kuongeza adhabu ya kosa la kufanya biashara ya madawa ya kulevya kuwa kifungo cha maisha. Adhabu ya kosa hilo, kwa mujibu wa kifungo cha 16(1)(b) cha Sheria ya sasa, ni faini ya shilingi milioni kumi au mara tatu ya thamani ya madawa hayo katika soko au yoyote iliyo kubwa zaidi katika faini hizo na kifungo kisichopungua miaka ishirini hadi kifungo cha maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungo cha 52 cha Muswada kinaongeza kifungo kipya cha 17A kinachowekwa chini ya kifungo cha 17 cha sheria mama. Kifungu hiki kipya kinataja makosa na faini kwa watakaopatikana na hatia ya kutenda makosa hayo. Makosa mengine ambayo yanapendekezwa kuongezewa adhabu ni pamoja na kuvuta, kunusa au kutumia madawa ya kulevya kwa namna

16 APRILI, 2012

nyingine; kuvuta, kunusa au kutumia madawa hayo ndani ya nyumba, chumba au mahali pengine; kukutwa na kiko au vifaa vingine vinavyotumika kuvutia, kunusia au kutumia madawa hayo. Endapo mapendekezo ya Muswada huu yatapitishwa na kuwa Sheria, adhabu ya makosa hayo itakuwa faini ya shilingi milioni moja au kifungo cha miaka kumi au vyote viwili, yaani kifungo na faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu hii ni sawa na adhabu ya makosa hayo chini ya kifungo cha 16(2)(a) na (b) cha Sheria ya sasa ambacho kinapendekezwa kufutwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haifahamu hasara au matatizo yaliyokuwa yanatokana na makosa hayo kuwekwa katika kifungo cha Sheria. Vivyo hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haijafahamishwa juu ya faida, kama ipo, ya kuyahamisha makosa hayo na adhabu zake kutoka kifungo cha 16(2)(a) na (b) kwenda kifungo cha 17A kinachopendekezwa na Muswada huu. Inaelekea pendekezo la marekebisho ya kifungo hiki yameletwa Bungeni bila kuzingatia ufinyu wa muda wa Bunge hili Tukufu na kwa hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza mapendekezo haya yasikubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unapendekeza pia kuongeza adhabu ya makosa ya wamiliki, watumiaji au wasimamizi wa majengo au

16 APRILI, 2012

vyombo vya usafiri wanaoruhusu majengo au vyombo vyao kutumiwa kuandaa au kuzalisha madawa ya kulevya; au wanaokutwa na vyombo au vifaa vya kutengenezea madawa ya kulevya. Adhabu ya sasa ya makosa hayo ni faini ya shilingi milioni moja au kifungo cha miaka kumi au vyote viwili, yaani kifungo na faini. Adhabu inayopendekezwa katika kifungu kipyua cha 17B ni kifungo cha maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri na ni busara kwa Bunge lako Tukufu kuhoji sababu halisi za mapendekezo ya kuongeza adhabu za makosa haya. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi kwamba "matumizi na upatikanaji wa dawa za kulevya bado ni tatizo kubwa hapa nchini." Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu hatari kwa nchi yetu na madhara kwa jamii yetu kutokana na matumizi ya madawa ya kulevya na hivyo umuhimu wa kuendelea kupiga vita biashara na matumizi haramu na hatari ya madawa ya kulevya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchambuzi wa Muswada huu, Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala ya Bunge lako Tukufu ilipata ushuhuda kutoka kwa Kamishna Christopher J. Shekiondo wa

16 APRILI, 2012

Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya nchini. Katika ushuhuda wake, Kamishna Shekiondo aliieleza Kamati kwamba ni muhimu kwa adhabu za makosa ya madawa ya kulevya zikaongezwa kama inavyopendekezwa kwa sababu tatizo la biashara hii haramu na matumizi ya dawa hizi limekuwa likiongezeka hapa nchini. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haitakuwa inakosea kwa kuamini kwamba hii ndiyo sababu au *rationale* pekee ya mapendekezo ya kuongeza adhabu hizi kama inavyopendekezwa na Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu na *rationale* ya kuongeza adhabu kwa makosa ya madawa ya kulevya kama inavyopendekezwa haiendani na hali halisi ya tatizo la biashara na matumizi ya madawa ya kulevya nchini. Aidha, maelezo aliyoyatoa Kamishna Shekiondo kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala hayalingani na ushahidi uliopo katika taarifa mbalimbali rasmi zilizoandaliwa na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya na kuwasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu kwa mujibu wa kifungu cha sita (6) cha Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya. Kwa mfano, katika Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2010, Tume hiyo imeonesha kwamba kiasi cha bangi kilichokamatwa mwaka 2010 ni tani 4.03 ikilinganishwa na tani 964.1 zilizokamatwa mwaka 2004. Vile vile, wastani wa kiasi cha bangi

16 APRILI, 2012

kilichokamatwa kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano kufikia mwaka 2010 ulikuwa ni tani 80.4 ukilinganishwa na wastani wa tani 441.8 zilizokamatwa kwa mwaka kati ya 2001 na 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa za Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Dawa za Kulevya zinaonesha pia kupungua kwa biashara ya *mandrax*, *morphine*, bangi iliyosindikwa na bangi kavu katika kipindi cha miaka kumi kati ya mwaka 2000 na 2010. Ni kweli kwamba takwimu za Tume zinaonesha kuongezeka kwa biashara ya madawa ya *heroin* na *cocaine*. Kwa mfano, kiasi cha *heroin* kilichokamatwa kimeongezeka kutoka kilo 5.3 mwaka 2000 hadi kilo 185.8 mwaka 2010. Vilevile, kiasi cha *cocaine* kilichokamatwa katika kipindi hicho kimeongezeka kutoka kilo 2.104 mwaka 2000 hadi kilo 62.966 mwaka 2010, ikiwa "... ni takriban mara mbili zaidi ya kiasi chote kilichowahi kukamatwa katika kipindi cha miaka kumi iliyotangulia." Aidha, idadi ya kesi zinazotokana na madawa ya *heroin* imeongezeka kutoka kesi 160 mwaka 2000 hadi kesi 317 mwaka 2009 na ile ya *cocaine* imeongezeka kutoka kesi 36 mwaka 2000 hadi kesi 336 mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, takwimu za Tume zinaonyesha kwamba idadi ya watuhumiwa wa makosa ya biashara ya *heroin* imepungua kutoka watuhumiwa 412 mwaka 2001

16 APRILI, 2012

hadi watuhimiwa 15 mwaka 2010, na wale wa biashara ya *cocaine* wamepungua kutoka watuhumiwa 251 mwaka 2008 hadi watuhumiwa nane katika mwaka 2010. Hii ni picha ya kuongezeka kwa kiwango cha dawa hizo zinazokamatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kimoja ambacho hakionyeshwi na taarifa pamoja na takwimu zote za Tume ya Kuratibu Udhhibiti wa Biashara ya Dawa za Kulevya ni idadi ya watuhumiwa waliopatikana na hatia ya makosa haya Mahakamani. Kamishna Shekiondo alipoulizwa juu ya jambo hili kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala alijibu kwamba ni mtu mmoja tu ambaye amepatikana na hatia ya makosa haya katika kipindi chote cha taarifa za Tume. Kamishna Shekiondo alieleza sababu ya hali ya kustajabisha kuwa ni rushwa iliyokithiri katika Mahakama zetu ambapo alisema watuhumiwa wengi wamekuwa wakiachiliwa huru kwa sababu ya kutoa rushwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kauli ya Kamishna Shekiondo kuhusiana na sababu za watuhumiwa wa biashara haramu ya dawa za kulevya kutopatikana na hatia Mahakamani ni ya kuaminiwa, basi ni wazi kwamba tatizo la kuendelea kushamiri kwa biashara haramu ya dawa za kulevya nchini halitokani na udogo wa adhabu zilizowekwa na sheria ya sasa kwa makosa hayo, bali ni rushwa

16 APRILI, 2012

na uozo ulioko Mahakamani na kwenye mamlaka za uandaaji na uendeshaji mashitaka ya makosa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba dawa ya tatizo la rushwa na ufisadi katika taasisi hizo haiwezi kuwa kwa kuongeza adhabu za makosa hayo, bali kuzisafisha Mahakama na Taasisi za Uandaaji na Uendeshaji Mashitaka ili kuondokana na rushwa na ufisadi huo. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiwezi kuunga mkono mapendekezo ya marekebisho ya sheria ya kuzuia biashara haramu ya dawa za kulevya yaliyoko kwenye Muswada huu, kwani hayalengi kuondoa kiini cha tatizo ambacho ni rushwa na ufisadi.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaridhika na maoni na ushauri wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusiana na mapendekezo ya marekebisho mengine ya sheria yaliyoko kwenye Muswada huu na haioni haja ya kurudia maoni na ushauri huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.
(Makofi)

16 APRILI, 2012

MWENYEKITI: Ahsante. Nakushukuru sana Mheshimiwa Raya kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, moja kwa moja tunakwenda kuanza na wachangiaji. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, Zanzibar, atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Zanzibar.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi ni vyema nianze moja kwa moja katika sehemu ya 11 katika kifungu cha 25A.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii inahusu zaidi *license point system*. Kifungu hiki kimeletwa baada ya kuona ongezeko kubwa la ajali barabarani na kwa maana hiyo kusababisha Watanzania wengi kupoteza maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maisha ya Watanzania yanapotea kwa sababu tu ya uzembe wa madereva. Maisha ya Watanzania yanapotea kwa sababu madereva wanashindwa kufuata taratibu za barabara. Kwa maana hiyo, naipongeza tu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Mheshimiwa Waziri

16 APRILI, 2012

kwa kuleta kifungu hiki ambacho kitasaidia zaidi kupunguza vifo vya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu mataifa mengi ambayo wameendelea, huu ndiyo utaratibu wao wa kisheria. Kwa hiyo, siyo jambo geni kwa Tanzania kuweka utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiingia katika kifungu cha 25A(2) ambacho kinampa mamlaka Waziri kufanya *regulations* ambazo zitaratibu utaratibu mzima wa leseni hizi za udereva, kifungu hiki nadhani kimempa mamlaka mapana Mheshimiwa Waziri kwa sababu kifungu cha 25A(1) hakionyeshi ni idadi gani ya *points* za *driving license* zitakuwepo. Kwa hiyo, ni vyema katika kifungu hiki cha (1)A kieleze ni idadi gani ya *points* zitakazokuwepo katika *driving license* ili kitoe nafasi nzuri kwa Mheshimiwa Waziri kuweza kuandaa mchakato mzima wa *operation* kwa *license* hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uwezo aliopewa Mheshimiwa Waziri katika kifungu cha 25A(2) wa kuweka utaratibu, nina maoni kidogo kwamba ni vyema izingatie makosa maalum, ambayo yanayosababisha ajali kwa wingi barabarani. Kwa mfano, kuendesha gari kwa mwendo kasi, hii hakuna ambaye anapinga kwamba inachangia kwa kiasi kikubwa kusababisha

16 APRILI, 2012

ajali barabarni na hivyo kusababisha vifo vya Watanzania. Pia kuendesha gari wakati dereva huyo amelewa inaua Watanzania kila siku; pia kuendesha gari ambalo halina viwango; lakini pia kufanya kitendo ambacho kinasababisha ajali barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vyema kuwepo na jedwali ambalo linaandaa makosa maalum ambayo yanasababisha ajali kwa wingi ili kuweka jedwali lile pamoja na *points deductions* katika leseni ya udereva. Hii itarahisisha utendaji wa haki katika Mahakama zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea na kifungu cha 39 katika mabadiliko ya kifungu cha 13. Namshukuru tena Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwa kuweka utaratibu huo wa kisheria wa kutaifisha mali zile ambazo zinapatikana kwa njia isiyo halali, lakini mtu yule ambaye amepata mali kwa njia isiyo halali amekimbia au kabla ya kusikilizwa kesi ile amefariki au amefariki wakati wa upelelezi. Wabunge wengi wana hofu na suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hakuna nchi ambayo haina makosa haya. Nchi nyingi zina mafisadi ambao wanajipatia mali kwa njia isiyokuwa ya halali. Kama mtu yule anafanyiwa uchunguzi au amekimbia au amefariki kabla ya hukumu, ile mali

16 APRILI, 2012

ya ufisadi ambayo amepata iende wapi? Si halali mali ile kutumika kwa familia yake hata kama angekuwa hai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu cha msingi hapa naona ni kuhakikisha kuna ushahidi wa kutosha (*strong evidence*) ya kuonyesha hata kama yule mtu angekuwa hai, basi utafishaji ule ungefanyika. Hicho ndiyo cha msingi. Tusiwe na hofu, tusiwalinde mafisadi, tusiwalinde wezi ambao wanajipatia mali kwa njia isiyokuwa ya halali. Mali ambayo imepatikana kwa njia isiyokuwa ya halali ni sawa kutaifishwa kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linanisikitisha, pamoja na kwamba Mwanasheria Mkuu ameelezea kwa kina, ni kuondolewa kwa Muswada *Part II* mpaka ile *Part VIII* na haukuletwa hapa Bungeni kwa sababu kipindi kilichopita tulielekeza uletwe. Mwanasheria Mkuu alisema kwamba utaletwa baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi masikikitiko yangu kwa niaba ya wanafunzi wa Vyuho Vikuu Tanzania ni kwamba *Higher Education Students' Loan Board* kama ingeletwa leo na tukaupitisha Muswada ule, ungeleta ufanisi mzuri kwa wanafunzi wa Vyuho Vikuu. Leo tunaambiwa Wizara zinajipanga wakati *Higher Education Students' Loan Board* ina

16 APRILI, 2012

watalaam wa kutosha wa kuweza kufanya michakato na wakaipelekea Wizara na sehemu nyingine zote.

Kwa hiyo, nadhani Wizara haikuwajibika vizuri na itaendelea kuleta usumbufu mkubwa kwa wanafunzi ambao wanastahili kupata mikopo Vyuho Vikuu. Sioni kama wataleta baadaye kwa sababu kipindi kijacho ni kipindi cha bajeti na bajeti hiyo inakuwa miezi mitatu. Baadaye ipi? Muda wote huo wanafunzi wana-*suffer* kwa mazingira magumu, hawapati fedha za kuendesha masomo yao, leo tunaambiwa utakuja baadaye! Hii kwa kweli haiteti maantiki. Je, *are serious* kweli kuwatetea wanafunzi ambao wanahitaji mikopo kwa wakati? Leo tunasema tutaleta baadaye. Kwa kweli hii inasikitisha sana. Nasema nasikitika kwa niaba ya wanafunzi wa Vyuho Vikuu Tanzania kwamba hawakutendewa haki na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah. Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, atafuatiwa na Mheshimiwa John Mnyika.

16 APRILI, 2012

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo na leo kunipatia nafasi hii ya kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na vipengele vifupi tu nataka kuvizungumzia ili niweze kujua hali halisi ya marekebisho haya. Nitaanzia katika Sheria ya Mapato kwa Njia ya Uhalifu Sura ya 256, Sehemu ya 13 ya Muswada huu inayopendekeza marekebisho ya Sheria ya Kujipatia Mapato kwa Njia ya Uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na sheria hiyo, sina matatizo. Lakini, kuna vipengele ambavyo vinaweza vikatoa dhuluma wakati unaweza ukamtia adhabu mhusika ambaye siye. Mfano, kesi imekwenda Mahakamani, mhusika anahukumwa au yuko kwenye taratibu za kesi. Lakini kabla hukumu yake haijathibitishwa, tuseme kesi ile ilikuwa ni ya jinai ambapo huwa ndiyo anashitakiwa, lakini kabla hukumu haijathibitishwa na anasema huwezi mtu kumtia hatiani mpaka upate uthibitisho pasipokuwa na shaka. Sasa mtu huyu amefariki.

Baada ya kufariki, sheria inasema kwamba mali yake ifilisiwe ikiwa yu hai, kathibitika au hajathibitika, kafa, kesi iko Mahakamani, ile sheria isimame pale pale kwamba yule mtu afilisiwe mali yake. Hapo

16 APRILI, 2012

nimeona kwamba warithi hatutowatendea haki. Kwa sababu mtu akishafariki, kilichokuwepo siyo cha kwake ni cha watu wengine. Wale warithi, ikiwa mke, watoto, au warithi wa aina yoyote, wao hawajui kwamba mali ile ilipatikana kwa njia ya uhalifu au kwa njia mbaya, wao wanajua hii ni mali ya baba yetu au ya mama yetu, na huyu mzee ameshafariki, utaratibu ni kuingia katika mirathi. Sasa, nadhani suala hili liangaliwe zaidi kwa sababu itakuwa ile sheria haijadhhibiti. Kwa sababu sheria inasema mtu umtie hatiani na uthibitisho pasina shaka. Sasa huyu mtu hukumtia hatiani na amefariki, sasa vipi mali yake ifilisiwe? Sasa nilikuwa nataka hapo paangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja sehemu nyingine ya pili ambayo nataka kuzungumzia: Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Sura ya 96. Mimi hii sina matatizo nayo, maana marekebisho hayo yaliyofanywa ni kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Utaratibu uliokuja sasa hivi ni mzuri kwa sababu inakwenda kwa Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa hakika Ofisi ya Zanzibar wanayo, haina matatizo. Baadaye unapitia katika Ofisi ya Bunge, Ofisi ya Bunge Zanzibar wanayo ofisi, watendaji wa kufanya shughuli hii wapo. Hapa nampongeza Mheshimiwa Waziri, nampongeza Mwanasheria

16 APRILI, 2012

Mkuu kwa suala hili walilolifanya, ni zuri na linatoa sura nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapo hapo nina kilio. Sisi Wabunge wa Viti Maalum tunaomba tuwe wadau katika Mfuko huo, kwa sababu unapokiona kitu kizuri kinakwenda kwa mwenzio, unakimezea mate. Sasa taarifa niliyonayo ni kwamba wakati unaundwa Mfuko huu, kulikuwa bado, sheria yake ilipopita Viti Maalum vilikuwa havija-*function*. Sasa kama ni kweli iko hivyo, sasa vimeshakuwa vina-*function*, basi tunaomba na sisi angalau mkono wetu uingie humo kusaidia maendeleo ya Majimbo yetu ambayo sisi itakuwa Mkoa tuko *all round* na Majimbo yote. Ningeomba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na hili alipokee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja na suala lingine ambalo ni Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura namba 200. Nakubaliana na mapendekezo ya Serikali, sina matatizo nayo. Lakini kuna hii inaelezea Sheria ya Kuzuia na Kusafirisha Dawa za Kulevya, sura ya 95. Sasa hapa kidogo nimekuwa na mashaka napo kwa sababu tunao mateja wetu wa mitaani, hawa watoto wetu, anaweza akakutwa na pipi moja tu akafungwa maisha na wakati *super dealers* wanatembea mitaani. Sasa kwa vyovyote sheria hii iangaliwe, ipangiwe kwa mujibu wa hatia ya mtu. Mtuhumiwa kwa kosa lake, ukubwa wake

16 APRILI, 2012

na udogo wake. Sasa lazima kitu kama hicho kiwepo. Lakini ukisema atakayepatikana na dawa za kulevya afungwe maisha, tutawafunga vijana wetu na *super dealers* wako mitaani wanatamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwa hayo machache niliyochangia, natoa pongezi kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Fakharia, sasa naomba nimwite Mheshimiwa John Mnyika na Mheshimiwa Pindi Chana ajiandae.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu una sheria nyingi ambazo tunazifanyia marekebisho, sheria takriban tisa. Kwanza, niunge mkono uamuzi wa Serikali wa kuondoa mapendekezo ya marekebisho yote yaliyokuwa yanahusu Bodi ya Mikopo katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa sababu yale mapendekezo yaliyokuwepo hapa

16 APRILI, 2012

Mezani yalikuwa kwa kweli hayaendi kusaidia uboreshaji wa utoaji wa mikopo kwenye elimu ya juu, yalikuwa yanakwenda kuongeza ubaguzi na migogoro kinyume na matakwa halisi na dhamira ya wanafunzi wa Vyuu Vikuu. Nitoe wito tu kwa Serikali kwamba kuyaondoa haya marekebisho ni jambo moja, kurudisha Muswada ukiwa umezingatia matakwa ya wadau, ambao ni wanafunzi wa Vyuu Vikuu, wahitimu wa Vyuu Vikuu ni jambo lingine tofauti sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kwenda vizuri ni vizuri Serikali kwanza kwenye Mkutano wa Bunge ama hili linaloendelea, au mwanzoni mwa Mkutano wa Bunge la Bajeti, ikaileta kwanza Bungeni Ripoti ya Tume ya Rais iliyokuwa imeundwa kuchunguza vyanzo vya migogoro katika elimu ya juu na migongano iliyopo katika Sera ya Mikopo ili mapendekezo yoyote ya marekebisho ya sheria yakaenda kutatua vyanzo vya matatizo badala ya kushughulikia matokeo ya matatizo. Kwa hiyo, kama Muswada huu ungeletwa kwenye Mkutano huu wa Bunge tungeujadili bila kwanza kupatiwa ile ripoti ya Tume ya Rais ambayo mpaka sasa imefanywa kuwa siri. Ukweli ni kwamba tusingeshughulikia tatizo la msingi na migogoro kwenye elimu ya juu ingeendelea.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, rai yangu kuhusu hili na vile vile wigo mpana upanuliwe kuhusisha Kamati za kisekta za kibunge, siyo Kamati ya Katiba na Sheria peke yake kwenye suala hili, kwa kuwa hili ni jambo linalogusa sekta nyingi kwenye nchi yetu na inagusa watu wengi kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine inahusu Sheria ya Jeshi la Polisi. Niliwahi kuuliza swali la nyongeza hapa Bungeni la kuomba sheria hii ya Jeshi ifanyiwe marekebisho makubwa kwa kuwa kimsingi imepitwa na wakati na haiendani na mikataba ya kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia. Wakati ule Wizara inayohusika ikaahidi hapa Bungeni kwamba utafiti unaendelea na Serikali italeti marekebisho makubwa ya sheria. Lakini kwenye Muswada huu wa marekebisho ya sheria kimeguswa kipengele kidogo sana kwenye sheria ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali wakati wa kuhitimisha hoja, ituambie ni lini marekebisho makubwa ya Sheria ya Jeshi la Polisi yatafanyika ili kulinda haki za raia wanaonyanyaswa na Jeshi la Polisi, lakini vile vile sheria hii ifanyiwe marekebisho kuendana na mikataba ya kimataifa ambayo imesainiwa na nchi yetu. Kwa hiyo, marekebisho haya ambayo yameletwa ni kidogo

16 APRILI, 2012

sana, ni kipengele kimoja tu na hayajagusa wigo mpana kama ambavyo Serikali iliahidi Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ya sheria ni kuhusiana na sheria ya usalama barabarani. Dhana inayoingizwa hapa ni dhana ambayo inakubalika kimataifa ya kuweka *point* katika leseni kutegemea na makosa. Lakini naungana na mchangiaji mwingine aliyemaliza kwamba moja ya mamlaka aliyopewa Waziri kwa mujibu wa kifungu hiki cha sheria ni makubwa sana pamoja na kuwa anasema kwamba ataweka viwango na utaratibu kwa mujibu wa kanuni, bado mamlaka ni mapana sana, misingi ile ya viwango ilipaswa iwekwe kama sehemu ya jedwali, kama sehemu ya marekebisho ya sheria hii ili mipaka ya Waziri isiwe mikubwa sana kwenye kuamua ni mfumo gani utumike kuweka pointi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa napitia hapa ripoti hii maalum ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuhusiana na ufanisi wa *traffic* na ufanisi wa ukaguzi barabarani, ukiipitia na ukaangalia mapendekezo ya marekebisho ya sheria yaliyopendekezwa, inaoneshwa kwamba tunarekebisha sheria, leo lakini hatuendi kutibu mzizi wa tatizo la ajali barabarani ambazo sasa hivi zinasababisha mauaji ya raia wengi kuliko wakati wowote kwenye historia ya nchi yetu.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ripoti ya ufanisi wa ukaguzi wa barabarani, suala la historia ya makosa ya barabarani ambayo hili suala la uwekaji wa pointi kwenye leseni linakwenda kulitatua ni sehemu ndogo sana ya mapendekezo ambayo Mkaguzi Mkuu baada ya kuwahoji *traffic*, madereva na wananchi, ameona kwamba ndiyo chanzo cha kuongezeka kwa ajali barabarani. Asilimia 74 ya ajali za barabarani hivi sasa zinasababishwa na makosa ya kibinadamu, wakati asilimia 14 pekee ndiyo ambayo inasababishwa na makosa ambayo sasa hivi barabarani Jeshi la Polisi limewekeza nguvu kubwa sana kuyakagua, kuangalia *triangle*, kuangalia *mechanical effects* ambazo kwa maana ya ukaguzi huu yanachangia sehemu ndogo sana ya idadi ya ajali barabarani. Sasa kwa msingi wa ripoti hii, vile vile imeeleza bayana kwamba tatizo la msingi lililopo kwenye Taifa letu kwa sasa ni rushwa barabarani.

Kwa hiyo, unaweza ukatoa leseni mpya, ukaweka mfumo wa pointi, sana sana unaongeza tu njia nyingine ya mkondo mwingine wa rushwa kule barabarani, kwa sababu *Traffic* atakapomfuata yule mtu akimwona ametenda kosa, atapaswa amwekee pointi, wataendelea kujadiliana tu, kwamba nikuwekee pointi au nisikuwekee pointi? Una elfu tano au una elfu kumi? Uzo huu wa ajali

16 APRILI, 2012

barabarani utaendelea, kwa sababu hatushughuliki na msingi wa tatizo, tunaangalia matokeo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wetu waliopo barabarani kwa kweli wana hali mbaya sana. Tumepiga kelele huku Bungeni kuhusu *rationing allowance*, Serikali ikatoa kauli hapa Bungeni kwamba *rationing allowance* kwa Jeshi la Polisi imepandishwa kutoka Sh. 100,000/= mpaka Sh. 150,000/=, wakati ukweli ni kwamba Askari wanalipwa Sh. 100,000/= mpaka hivi leo, na Askari akidai Sh. 150,000/= anachukuliwa hatua. Ni vizuri Serikali ikaenda kushughulikia vyanzo vya matatizo badala ya matokeo ya matatizo ili marekebisho ya sheria yanayoletwa yajikite kwenye vipengele vinavyokwenda kushughulikia tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti hii ya Mkaguzi imeeleza vile vile kwamba tatizo la msingi la Jeshi la Polisi, Usalama Barabarani ni vifaa vinavyohusika, na mgawanyo wa Askari kwa kuangalia ni maeneo yapi yanasababisha ajali zaidi. Kwa hiyo, tatizo letu hasa siyo tatizo la kisheria, ni tatizo la kiutawala, ni tatizo la kiutendaji, ni tatizo la kimfumo. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali pamoja na marekebisho haya ya sheria yaliyoletwa, ikaelekeza nguvu zaidi kwenye kusafisha mifumo badala ya kutunga sheria na sheria zikakaa kwenye makabati.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kugusia sehemu ya 7 (12) ya sheria yanayohusu Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Katika hili, sitazungumza kwa kirefu kwa sababu naelewa kuna kesi Mahakamani ya kupinga huu mfuko kwa ujumla wake. Lakini naungana na mchangiaji aliyemaliza, kuhusiana na umuhimu wa Wabunge wa Viti Maalum kuingizwa kwenye sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia jedwali la marekebisho ambalo limeletwa na Serikali, hapa Bungeni Waziri Mkuu aliahidi kwamba kupitia marekebisho haya ya sheria, sasa Wabunge wa Viti Maalum wataingizwa kama sehemu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Kama hiyo ahadi kweli ni ya kutekelezwa, natarajia Serikali ilete nyongeza nyingine ya jedwali la marekebisho ili kuwaingiza Wabunge wa Viti Maalum kama ambavyo Waziri Mkuu (Serikali) alitoa ahadi Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sehemu ya 13 *Proceeds of crime Act*, naunga mkono dhana ya watuhumiwa ambao tuhuma zao zitakuwa zinaonekana zina uthibitisho wa hali ya juu, pale wanapofariki, mchakato wa mali kufilisiwa ukafanyika. Lakini nitapenda Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa kuhitimisha hoja atueleze ni kinga gani na uhakika gani wa kisheria unawekwa kwa Marehemu na mali zake, kwa sababu huyu ni

16 APRILI, 2012

mtuhumiwa ambaye bado alikuwa hajafikia hatua ya kuhukumiwa, lakini mali yake inachukuliwa. Pamoja na kuwa ni jambo jema kuwa na vifungu vya namna hii, lakini ni lazima tuhakikishiwe kwamba mwisho wa siku haki za pande zote zitalindwa.

Haki za umma zitalindwa, lakini wakati huo huo haki za Marehemu zitalindwa. Isije ikafikia hatua ambayo watu wakiwa wanabandikwa tuhuma, akishabandikwa anauawa, halafu mali zake zinafilisiwa. Kwa hiyo, tuangalie pande zote mbili. Wakati ambapo vyama vingine, sisi wengine viongozi wetu waliwataja baadhi ya watuhumiwa wa ufiisadi Septemba 15 pale Mwembeyanga mwaka 2007 na wengine wakatangazwa kwamba wameaga dunia kama Marehemu Balali, Mungu amlaze mahali pema, sheria hii haikuwepo wakati huo. Lakini kwa sheria hii ni vizuri ikatumika, lakini nasisitiza tu kwamba ile mipaka ya haki ilindwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia sehemu ya 16 ambayo inahusu marekebisho ya Muswada wa Sheria ya Kudhibiti madawa ya Kulevya. Nasikitika sana kuhusiana na haya marekebisho, kwa sababu haya marekebisho maeneo mengine yanakwenda kuongeza kifungo na kuwa kifungo cha maisha. Kwa wale watumiaji wadogo wadogo, sheria inakwenda kuwawekea faini ya Sh. 1,000,000/= na kifungo cha miaka kumi.

16 APRILI, 2012

Lakini tatizo letu la msingi kwenye masuala ya madawa ya kulevya siyo sheria. Kwa sababu kwa sheria ya sasa ilivyo, tayari ilikuwa inatamka *option* za adhabu, miaka 10 au 20 au faini inayoendana na mara tatu ya thamani ya madawa yaliyokamatwa au kifungo cha maisha kwa sheria ya sasa. Kwa hiyo, kusema kwamba madawa ya kulevya kasi inaongezeka kwa sababu eti sheria ni dhaifu siyo hoja sahihi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiona ni Serikali ije kutueleza wakati inahitimisha hoja, ni kwanini pamoja na kuwa kiwango cha madawa ya kulevya yanayokamatwa kinaongezeka, kiwango cha watuhumiwa kinashuka? Ni kwanini kiwango cha madawa yanayokamatwa kinaongezeka kiwango cha watuhumiwa kinashuka? Ni kwanini katika kipindi cha miaka kumi zaidi ya watu 2000 wametuhumiwa kwenye masuala ya madawa ya kulevya, lakini mpaka sasa waliohukumwiwa hawafiki hata asilimia 0.1 ya watu ambayo wamehukumwiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo zito kwa sababu ukishakuwa na takwimu za namna hii za Serikali yenyewe halafu ukapata kauli za viongozi wa kiserikali, nami nakumbuka kauli ya Mheshimiwa Rais, aliwahi kutamka kwamba anayo orodha ya wauza madawa ya kulevya, sasa kama kuna takwimu za namna hii, halafu watu hawafungwi, kutunga sheria

16 APRILI, 2012

peke yake hata uongeze kifungo cha maisha na maisha na maisha, kama watu hawafungwi, hakuna atakayeogopa.

Kwa hiyo, tuelezwe kwa takwimu hasa kati ya watu 2000 waliokamatwa zaidi ya miaka kumi sasa kwa kipindi hiki cha miaka kumi, ni wangapi wamefungwa na tutajua na majina yao pengine ili tuone kama ni wale mateja wadogo wadogo pale Manzese au pale Sinza au pale Ubungo au ni wao wenyewe wanaoingiza? Kwa sababu tukizuia wanaoingiza hatuwezi kuwa na hao mateja wa barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni jambo ambalo kwa kweli Serikali itoe kauli thabiti sana kuhusiana na namna ambavyo itachukua hatua. La sivyo, tutakuwa tunaona kwamba hukumu zinakwenda kuongezwa kwa watu wadogo wadogo, lakini mwisho wa siku, watu wakubwa ambao hukumu tayari zilishakuwepo, wanapita kwenye mikono ya sheria na hawafungwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili sasa ni kubwa sana na lina athari kwa vijana wengi sana. Dar es Salaam sasa hivi kadri siku zinavyozidi kwenda ndiyo kadri ambavyo vijana wanazidi kuathirika na madawa ya kulevya. Sasa tunaweza tukajiuliza, kama Serikali inakuja Bungeni inasema mipaka ya

16 APRILI, 2012

nchi yetu ipo salama, nchi inalindwa vizuri, hivi haya madawa kwa wingi namna hii yanaingiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tujikite kwenye kushughulikia mzizi wa tatizo. Kwanini *cocaine* na *heroin* inaongezeka kwa kasi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naomba majibu kutoka kwa Serikali. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa John Mnyika kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na orodha ya wachangiaji, na sasa namwita Mheshimiwa Pindi Hazara Chana ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua Muswada huu na Mheshimiwa Mariam Kasembe ajiandaye.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa ku-*declare interest*, kwanza naunga mkono hoja. Naanza kwanza kabisa kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Daktari Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiapisha hivi karibuni Tume yetu ambayo itakusanya maoni ya Katiba. Nampongeza na Mwenyekiti ambaye ameteuliwa kuiongoza Tume ile na Wajumbe wote ambao wameteuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nawapongeza Wajumbe wa Kamati ya Katiba,

16 APRILI, 2012

Sheria na Utawala kwa umahiri wao waliochambua ile sheria na kuipitisha na Wabunge wote ambao mliipitisha sheria hiyo humu ndani Bungeni. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba pia niungane na Watanzania wenzangu kutoa pole kwa wale waliofariki hivi karibuni kwa familia zao ikiwa ni pamoja na familia ya msanii maarufu Tanzania, pamoja na Diwani wa Kata ya Mlangali ambaye amefariki hivi karibuni, na wengine wote ambao nimeshindwa kuwataja kwa majina, nasema Mungu azilaze Roho za Marehemu mahali pema. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi wangu huo, sasa naomba nitoe maelezo *general*. Maelezo yangu yapo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naanza na suala zima la marekebicho ya sheria mbalimbali. Naomba kushauri kwako nikimaanisha Bunge, lakini pia nitashauri kwa Mwanasheria Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na utamaduni wa kuletewa sheria mbalimbali, zinakuja sheria 16, sheria 20 katika Muswada mmoja. Mle ndani kuna sheria ambazo zinahusiana na Kamati

16 APRILI, 2012

mbalimbali, na mara nyingi sana hupelekewa Kamati moja kuzipitia sheria zote, na inapopelekewa Kamati moja, unakuta ile Kamati wakati mwingine haikujadili sheria mama inayoletea yale marekebisho.

Kwa mfano, kipindi kilichopita, tuliona upande wa *Loans Board* Kamati inayohusika na masuala ya *Loans Board* haikushirikishwa, ilikuwa ni Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Nadhani ni muda muafaka umefika, utaratibu huu unatakiwa kuwa *reformed*. Marekebisho ya sheria mbalimbali, sheria ndogo unakuta ni kifungu kidogo, kuongeza hiki kupunguza hiki, yapelekwe kwenye Kamati husika ili wale waliojadili ile sheria mama wanafahamu fika kwamba mambo gani yalikuwemo na hivyo inapokuwa na marekebisho madogo madogo inakuwa ni rahisi. Kuliko zinakuja sheria 16, kwa mfano, masuala ya Ulinzi, masuala ya Mambo ya Ndani, masuala ya *Traffic* na kila kitu mnafanya kazi vizuri sana, vema sana, lakini mnahitaji muda wa kutosha ku-*research*, mnahitaji muda mwingi sana na kadhalika.

Kwa hiyo, hizo ni *reform* ambazo ni lazima twende na wakati. Kwa hiyo, huo ni ushauri wangu kwa Bunge na huo ni ushauri wangu pia kwa Mwanasheria Mkuu.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naendelea kuchangia vifungu viwili tu vidogo. Kifungu cha kwanza kinazungumzia kuhusu Sheria ya Usalama Barabarani - *The Road Traffic Act*. Mimi nimekuwa nina kilio sana cha ajali barabarani. Nimewahi kuleta maswali Bungeni humu mara mbili na mara ya mwisho nikasema nataka kujua kampuni zinazoongoza za mabasi yanayopata ajali kwa wingi nchini.

Kwanini kampuni hizo tunaziruhusu kusafirisha watu wakati wameshindwa, watu wanakufa, sisi tunashuhudia, Wabunge hatufanyi lolote, tunakuwa hatujawatendea haki Watanzania, maana sisi ndio tunaotunga sheria. Ni wajibu wetu kutunga sheria ambazo zitapunguza ajali za barabarani kadri iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kushuhudia basi moja linapata ajali Watanzania 20 wanafariki, Watanzania 40 majeruhi, ile nguvukazi tunafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa na kilio sana na ninakotokea mimi ni barabara kubwa nchini. Mimi natokea Mkoa mpya wa Njombe na Iringa, pale tunashuhudia mabasi yanakwenda Zambia, yanakwenda Congo na Malawi, barabara ile yanapita mabasi mengi sana na mara nyingi *public transport* imekuwa ni changamoto na

16 APRILI, 2012

Watanzania wengi tunatumia *public transport*. Kwa hiyo, hizi ajali kadri iwezekanavyo tunatakiwa tuzipunguze zisiwepo. Kwanini safari imekuwa kama *one leg is on the grave, the other leg is on life*. Yaani ukisafiri unaanza Mungu wangu sijui nitafika salama! Hebu mniombe wapendwa, mguu mmoja kaburini, mguu mmoja upo kwenye *life*, haiwezekani. Ukisafiri ni lazima uwe na *guarantee*, nitafika tu. Lakini unasafiri, ukipita Kitonga unasema ooh, ahsante Mungu. Ukipandisha mlima fulani ooh, nashukuru sana. Ukifika, ooh, yaani kwa kweli... Tutafika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tuweke namna zozote za kupunguza ajali ili watu wakiwa wanasafiri wawe na amani. Kwa hiyo, naungana na suala la pointi, asilimia 50 ya ajali za nchi yetu ni uzembe. Zipo za bahati mbaya, mtu ana-*overtake* kwenye kona, ana-*overtake* mbele haoni inakuwaje? Mtu anaambiwa *speed* 50 anakwenda 120 na sisi wote ni mashahidi. Kwa hiyo, ndugu zangu nadhani wakati umefika sasa tutafakari mbinu zozote za kupunguza ajali barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naungana na hili suala la kuweka pointi kwenye leseni ili madreva wanaosafirisha hasa watu kwenye mabasi, basi linabeba watu 80, fikisha roho za watu 80

16 APRILI, 2012

salama. Usiwe mtu anapata kinywaji, ana-*overtake* kiuzembe uzembe, hii siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba utaratibu huu wa kupunguza pointi kwa wale wanaofanya makosa ya barabarani, kwanza ni vyema zikawepo *category* za makosa, isije ikawa hana *reflector*, hana *triangle* pointi zimepungua, maana yake tairi kipara, sijui nini, yapo mambo mengi. Tuangalie ni makosa gani yanapelekea kupunguza pointi, lakini kwanza naunga mkono, nazungumzia namna ya ku-*operationalize*, lakini pia *machinery* gani zinatumiwa kupunguza pointi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu wa kupunguza *point*, tusipunguziane pale barabarani, kule tunapokwenda kutenda haki vipo vyombo kwa mujibu wa Katiba kinachotafsiri sheria, kinachojua sheria inasema nini ambacho ni Mahakamani. Waende, kwa sababu mtu ataona kwamba nikipunguziwa *point*, nitakapofika hatua fulani, nitanyang'anywa leseni na nitazuiliwa kuendesha. Utaratibu huu uko nchi zote. Kama mtu anaendesha amekunywa, ni kosa. Watu tufuate maadili, Watanzania wapone kwenye usafiri wa barabarani.

Kwa hiyo, naunga mkono, lakini naomba *regulations* na taratibu ziwekwe vizuri kabisa ili ajali za barabarani zipungue. Watu wanapata ajali

16 APRILI, 2012

maskini, unamwona vipi? Mimi nilikatika mguu kwenye basi, mimi mkono; hapana, hapana. Hatuwezi tukabariki mambo hayo. Haiwezekani! Lazima tuweke utaratibu wa kuzuia ujali za barabarani. Kwa hiyo, utaratibu huu wa *point* kwa madereva wote, gari ndogo, gari kubwa uweke matatizo yale, *category* za ajali zionyeshwe waziwazi na vyombo vinavyohusika vishirikishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine dogo sana la mwisho ni sehemu ya 13 kuhusiana na mtuhumiwa ambaye amefanya kosa, ametoroka au amefariki, mali yake inataifishwa. Ninaunga mkono hoja hiyo. Mtuhumiwa aliyefanya kosa la jinai akatoroka, kwa nini ametoroka? Kutaifisha mali ile, pale ni halali. Naomba sasa sheria zinazohusu dhamana ziboreshwe, maana mtu ana haki ya dhamana. Yako makosa ambayo hayaruhusiwi dhamana, mada, *armed robbery*, haturuhusu dhamana. Yako makosa ya dhamana. Wakati mtu anapeana dhamana, kiwepo kifungu kwamba endapo utatoroka kwa sababu kosa lenyewe ni masuala ya mali na kadhalika, basi mali hiyo itataifishwa barabara.

Sasa tunakwenda *point* ya pili, amefariki. Hapo inakuwaje na hatujathibitisha kwamba ana hatia? Hapa naomba niwasemee akina mama, asilimia 50 ya Watanzania, nami nikiwa kama Mbunge wa Viti

16 APRILI, 2012

Maalum. Sasa hivi mtu akifariki hata kama hajatuhumiwa, ile mali kugawana na watoto ni changamoto. Mali ya baba bado ni changamoto kwenye jamii za leo. Sasa huyu, ni kweli mali imepatikana kwa njia ndivyo sivyo, amefariki, ametuhumiwa. Kwanza, uta-*define* vipi kwamba ile mali iliyopatikana kwa njia za uhalifu inaishia hapa na wala siyo hapa? Yamkini zinaishia eneo gani, hakuna *witness* sasa. Naomba Idara ya Mahakama tuharakishe kesi, ziishe, hukumu zitolewe *faster*, mali itaifishwe na yeye yupo, tuisubiri afariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepitisha Mfuko wa Mahakama na tunaomba hela na tutakuja katika Bunge hili safari hii kuwaombea hela za Mfuko wa Mahakama. Kipindi kilichopita, tumeomba Shilingi bilioni 20 ili kupunguza *backlog* ya kesi na sasa hivi tutakuja kwenye Bunge letu Tukufu hili kuomba hela. Tunaomba Mahakama isipunguziwe hela ili haki itendeke. Tukiomba hela Kamati ya Katiba na Sheria, Idara ya Mahakama *DPP*, kwa Mwanasheria Mkuu wapewe, haki itendeke na ile mali itaifishwe na yeye yupo anaiona kabisa, anatia sahihi, kwamba kweli hii iende kuliko kusubiri afariki. Kwa sababu Tanzania tumesaini Mikataba, *Universal Declaration of Human Rights*; Katiba yetu inasema: "*a person is innocent until proved guilty.*" Hivyo vifungu vyote tunavificha wapi? Tutaonekanaje wakati amefariki?

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi ina pande mbili, anayelalamika na anayelalamikiwa. Sasa anayelalamika yupo, anayelalamikiwa amefariki, unasimama dhidi ya nani? Jamani, Watanzania wenzangu Wanasheria *professionals, where are you?* Naomba sana jambo hili tuangalie sisi *Lawyers*, kesho na kesho kutwa wasije wakasema hao *Lawyers* walikuwa ni akina nani? Kwa hiyo, Marehemu anabaki kuwa Marehemu. Tuharakishe kesi, hukumu itoke, na yeye yupo *live*. Kwa hiyo, huo ndiyo mchango wangu, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Pindi Hazara Chana. Waheshimiwa Wabunge, hapa Mheshimiwa Mbunge anachangia. Alitoa rai, na rai hiyo alikuwa amelelekeza kwa Serikali. Lakini upande mwingine alielekeza kwa Bunge hususan katika kuangalia hii Miswada ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali, ile inahusu Kamati za Kisekta kupelekwa kwenye sekta husika. Sasa kwa kuwa tuko na Makatibu wetu, ningewaomba katika lile daftari letu la kuandika matukio ya siku, suala hilo ni muhimu sana likaingia kwenye rekodi, kusudi liweze kufanyiwa kazi kwenye vikao vyetu.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, naomba tuendeleo sasa na mchangiaji anayefuata ambaye nilikwishamtamka, Mheshimiwa

16 APRILI, 2012

Mariam Kasembe. Lakini wakati huo huo nimwombe Mheshimiwa Mustapha Akunaay na yeye ajiandae.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia marekebisho ya sheria mbalimbali ambayo imewasilishwa hapa leo. Naomba kuchangia kwa masikitiko makubwa sana juu ya kuahirishwa Muswada wa Korosho. Tulivyokuwa katika Mkutano wa Nne, tulifanya marekebisho ya Sheria mbalimbali na tulitarajia tutafanya marekebisho ya sheria inayohusu korosho. Lakini siku tunaletewa hapa mawasilisho hayo tuliletewa taarifa kwamba sheria ile haitajadiliwa. Tulipohoji tuliambiwa kwamba marekebisho ya sheria italetwa katika Mkutano huu wa Saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ratiba zetu tulizonazo, nilivyoona kwamba kuna marekebisho ya Sheria mbalimbali, nilikuwa na matumaini makubwa kwamba sheria hii ya korosho safari hii itawasilishwa kwetu na itapata fursa ya kujadiliwa. Lakini kwa masikitiko, tena katika orodha ya sheria zinazorekebisha leo, wakati Mwanasheria Mkuu alipokuwa anatuwasilishia, ametamka kwamba Sheria ya Korosho imeondolewa. Kwa hiyo, kwa leo tena hatupati fursa ya kujadili sheria hii.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *agenda* gani juu ya korosho? Kuna nini ndani ya Korosho? Ni nani anayekwamisha kuletwa kwa sheria hii ndani ya Bunge tukapata fursa ya kujadili? Ni kikundi kipi chenye fursa ya kuweza kukwamisha sheria ambayo tunatarajia kwamba ingeweza kusaidia wakulima wa zao la korosho? Kwa kweli mimi naweza kusema kwamba hatutendewi haki hata kidogo kwenye zao la korosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimesimama hapa kwa masikitiko mazito sana kuhusu malipo ya korosho. Leo hii nilitarajia nitapata faraja kidogo, lakini imezidi kuniongezea machungu pale nilipoona kwamba hata leo Serikali haitaki kutuletea sheria ya korosho tukajadili. Tafadhali namwomba Mwanasheria Mkuu awe wazi, kulikoni huko Serikalini na korosho? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii tumeililia sana. Nashauri ifanyiwe marekebisho kwa sababu fedha ya wakulima ambayo tulikuwa tunaitarajia ingekwenda moja kwa moja katika Halmashauri zetu na kuwasaidia wakulima kwa ajili ya kununua pembejeo. Fedha hii kwa miaka mingi imekuwa ikiishia Bodi ya Korosho. Bodi ya Korosho hawatusaidii lolote katika kuangalia kwamba mkulima anapata pembejeo kwa wakati. Sasa kwa nini hamtaki kuleta sheria hii tukairekebisha ili wananchi wanaolima zao

16 APRILI, 2012

Ia korosho wakanufaika? Tunataka kuacha fedha hii katika Bodi ya Korosho ili kuendelea kunufaika watu wachache. Kulikoni? Tunapokea kwenye vikao vya wadau wa korosho, kwa nini hamtuambii kwamba jamani sheria iliyopo itakuwa kama Msahafu au Biblia, haitabadilishwa milele? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza, sijawahi kusimama hata siku moja nikatamka kwamba sitaunga mkono hoja zilizoko mbele yetu. Leo kwa mara ya kwanza nataka kusema kwamba sitaunga mkono sheria mbalimbali zinazorekebisha hapa mpaka pale AG atakaposimama akaniambia ni kwa nini Sheria hii haitaki kuletwa Bungeni tukaijadili? Namwomba sana, kama kuna anayezuia, awe muwazi. Bungeni ni mahali pa uwazi, atuambie ni nani au kikundi gani ambacho kinatukwamisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita siku ya Jumatano kwa kutambua umuhimu wa jambo hili, Wenyeviti wa Halmashauri walikuja hapa Dodoma kumwona Waziri Mkuu, kuomba kwamba katika Bunge hili tusimalize shughuli zetu bila kuleta marekebisho ya Sheria hii na aliahidi kwamba amewasikia na litafanyiwa kazi. Kumbe kazi iliyofanyiwa ndiyo hiyo ya kutukwamisha tusiletewe hii sheria!

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea kwa uchungu mkubwa na nimesema, sitaunga mkono hoja hii na wala sitakuwa na nafasi tena ya kuchangia sheria mbalimbali tunazorekebisha leo. Hoja yangu ilikuwa ni kutaka kujua, kwa nini sheria hii imekuwa ikipigwa dana dana kila wakati? Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Kasembe.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kasembe amegusa kipengele kimoja tu kinachohusu kuondoa sheria. Iitakiwa iende kubadilisha nadhani maeneo mbalimbali kwenye Sheria ya Bodi ya Korosho, kwa hiyo, yeye ameongelea hiyo moja tu. Sasa kwa maana hiyo, tunaendelea na wachangiaji wengine ambao niliwatamka mwanzo.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha nisimame mbele ya Bunge hili leo kuchangia hoja hii. Pili, naungana na Waheshimiwa Wabunge wengine waliotoa salaam kwa familia mbalimbali zilizofiwa tangu Bunge lililopita hadi leo ambao wametamkwa na mimi, sina sababu ya kurudia ila ni kuwaombea mbele ya Mwenyezi Mungu Roho za Marehemu zipumzike kule ziliko.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza na rai aliyotoa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria ambayo mimi pia ni Mjumbe kwamba mabadiliko ya sheria yoyote ipelekwe kwenye sekta inayohusika kwa sababu muda wa Kamati nyingine zinatumiwa isivyo sahihi. Kwa mfano, Kamati ya Sheria na Katiba ililetewa *Loan Board Amendment* ambayo tuliifanyia kazi, baadaye tukaambiwa imekuwa *withdrawn* kwa sababu haikupitiwa kwenye Kamati ya Ustawi wa Jamii. Sasa tunashauri Kamati zinazohusika zipelekewe sheria hizo zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nianze na eneo la kurekebisha sheria, *The National Prosecution Service Act*. Naunga mkono kwa kuteuliwa kwa *legal officer* kutoka kwenye Serikali za Mitaa na mahali pengine popote pamoja na *private practicing lawyers* au *legal officers* ambao watateuliwa kufanya kazi kwa niaba ya DPP na kufanya *prosecution* kwa ajili ya kusaidia sehemu hiyo, kwa sababu sasa hivi Halmashauri zinashindwa kuendesha kesi zake ambazo zina mithili ya jinai kwa sababu ya kutokupatikana *State Attorneys*. Kwa hiyo, kuajiriwa hapo, Serikali itakuwa imewasaidia wananchi kuondoa *backlog* ya kesi nyingi. (Makofi)

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni kuhusu Sheria ya *Proceeds za Crime* kama walivyosema Wabunge wengine, lazima tuwe waangalifu tusivunje Katiba. Katiba yetu inasema, mtu yeyote anayeshitakiwa, anachukuliwa kwamba hana hatia mpaka hapo atakapothibishwa ana hatia. Kadhalika, mali atakazokuwa anamiliki na ambazo pia wanazo watu wengine ama ni *third part* au ni nani, kama haijathibitika ni ya huyu au kama ni ya jamaa yake, mali hii kama itakamatwa kutokana na sheria hii, mabadiliko yanataka kuonyesha itakuwa kinyume cha sheria ya kimataifa na Sheria ya Katiba ya kwetu. Kwa hiyo, kifungu hiki kitazame Katiba inasemaje juu ya miliki yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwamba hawa watu waliopata mali kwa njia isiyo halali, mali ile wasiifaidi, lakini pia isiwe ni kero kwa mali nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwetu kesi nyingi zinachelewa na washitakiwa wanafia Magereza, wengine wanafia kwenye dhamana. Lakini kama utakuja kukamata kwa sababu huyu amekufa na hajathibitishwa, mali hiyo iko kwenye *third part* na unataka kupiga mnada. Kesi ya jinai katika mfumo wetu wa sheria ni kwamba, ikifa na mambo yake yamekufa. Kwa hiyo, tufuate taratibu hizo hizo kimataifa.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleo sehemu inayofuata ambayo nilikuwa nimejitayarisha, nayo ni sehemu ile ya kuongezwa kifungu cha 25A ya Sheria ya Usalama Barabarani ambayo inaongezea kwenye leseni alama, ambapo mtu akitiwa hatiani atapunguziwa. Sheria yetu iliyoko sasa hivi ya *Traffic Act* inajitosheleza kwamba katika makosa maalum mshitakiwa akitiwa hatiani, leseni yake inafutwa. Sasa hii ya kupeana hapa *point* ambayo inaanza labda kutokea barabarani, kama Waheshimiwa Wabunge wenyewe walivyosema, itakuwa imefungulia uwanja mwingine wa kupeana rushwa. Hiyo ni hatari kubwa! Tusiruhusu kabisa alama hizo zipunguzwe na Polisi, alama hizo ziingie Mahakamani na ziwe kwa shauri maalum na siyo kila shauri. Mtu amekutwa hana *belt*, unaambiwa *point* mbili zinaondoka. Hiyo, tutakuwa tunafanya *kangaroo courts* huko barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono kwamba iende mahakamani ifanyiwe ushahidi na mtu akitiwa hatiani iwe ni shauri maalum kama ilivyo, kwa mfano mtu anapelekwa Mahakamani kwa kosa la kusababisha kifo au amesababisha na *reckless driving* lakini siyo mengine madogo madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, Waziri asiwekewe *regulation*, hii iwe ni sehemu ya

16 APRILI, 2012

Mahakama, tusichukue kazi ya Mahakama na sehemu ya utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pale, kulizungumzwa juu ya Mfuko wa Jimbo. Hii naona Waheshimiwa Wabunge wamewahi, yale yote ni Zanzibar. Ile ya kwetu ikija tutazungumza. Hii sasa hivi tukiizungumza tutakuwa tumechanganya na *Attorney General*, sidhani kama atakuwa na majibu. Lakini sitaki nimjibie, ila yalikuja kwetu tuyazungumzie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda wangu bado upo, naomba nirejee pale kwenye Sheria ya Dawa ya Kulevya. Katika dawa za kulevya kama Wabunge wengine walivyosema kwamba kesi zinapungua, lakini dawa nyingi zinaongezeka kukamatwa. Lakini kingine kikubwa kinachoonekana zaidi ni kwamba huko mjini wale wanaoathirika pia inaelekea wanaongezeka katika miji ya Dar es Salaam, Zanzibar, Arusha na Mwanza. Wale wanaitwa wateja. Sasa hawa askari sielewi wanafanya kazi gani, vijana wetu wameharibikiwa sana, au hii jamii inataka kuangamizwa? Naomba niishie hapo, ya kwangu yamekwisha. Ahsante. *(Makofi)*

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nitoe shukrani

16 APRILI, 2012

kwako kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuzungumza kwa kuchangia mambo machache sana ambayo mengine wenzangu wameyasema, lakini naweza kuyasema kwa msisitizo tofauti.

La kwanza kabisa ni hii sheria ya *Higher Learning Students Loan Board*. Nitazungumza mambo matatu. La kwanza, ni suala la kutathimini nani anastahili kupewa mkopo? *Means test* imeweka vigezo ambavyo ndivyo inavibeba wakati inafikiria nani apewe mkopo. Lakini kuna jambo moja ambalo ni muhimu sana ambalo haigusi. Jambo lenyewe ni la wazazi ambao mmoja amefariki, ambao ni *single parent*. Sheria inazungumza juu ya *orphanage*, lakini ukitazama *orphanage* maana yake, ni aliyefiwa na wazazi wake wote. Lakini ukweli ni kwamba tunaona akina mama wengi wanapata taabu sana hasa baba anapofariki, pale inapokuwa baba ndiye aliyekuwa analipia watoto. Sasa kama sheria hii haimtambui mjane katika *category* ya *single parent* ikampa *score* ya kumpunguzia malipo, basi tutakuwa hatujasaidia. Tutazame kuongeza *single parent* kama sehemu ya *means test* ili isaidie hawa *single parent* kusaidia kulipa malipo. Hilo la kwanza.

La pili ni suala la *priority courses*, hiyo *cap. 178* inampa mamlaka Waziri mhusika wa elimu kubadilisha *list*.

16 APRILI, 2012

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo.

MWENYEKITI: Naomba Dokta uendelee, nitakupa nafasi, ngoja aendelee.

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, inampa Mheshimiwa Waziri mhusika kuto-*vary list* ya *priority courses*. Ninashauri...

TAARIFA YA SPIKA

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa! Dokta naomba ukae.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji anayeendelea kuzungumza anaongelea sheria ambayo haipo, naomba mwongozo wako.

MWENYEKITI: Hebu endelea Dokta, ni kitu gani anachoongelea ambacho hakipo ulicho ki-*notice* hapa?

16 APRILI, 2012

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, anazungumzia masuala ya *The Higher Education Students' Loans Board* ambayo imeondolewa katika Muswada huu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Mgimwa utakapokuwa unaendelea na kuchangia, fanya walichokifanya wenzako, maneno ya utangulizi.

Waheshimiwa Wabunge, unaweza ukagusia kidogo Sheria ambazo zimeondolewa kama alivyofanya Mheshimiwa Mnyika, amezigusia kidogo na wachagiaji wengine wamegusia kwa sababu zimetajwa katika hoja iliyotolewa na mtoa hoja. Kwa sababu hoja hii iliyoletwa na mtoa hoja, haikuanzia tu hewani, yako maeneo ameyataja hapa kama ni maeneo ambayo yameondolewa. Kwa hiyo, kama ni hoja ambayo imeshasemwa kwa namna moja ama nyingine hapa ndani, mtu akiiiongelea kwa utaratibu uleule wa maneno ya awali, yuko sahihi, lakini hatakiwi kuendelea na ndiyo maana hata Mheshimiwa kama angeendelea zaidi ya pale, ingebidi nimwambie aache kuendelea na hoja yake kwa sababu si hoja ya msingi ambayo iko humu ndani lakini aliizungumza kama hoja ya utangulizi kama alivyofanya Mnyika na kama walivyofanya wengine.

16 APRILI, 2012

Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mgimwa kama hoja yako wewe inataka kuzungumzia tu mikopo ya elimu ya juu, hiyo siyo hoja ambayo inatakiwa kujadiliwa kwenye sheria hii lakini kama ni maneno ya utangulizi, maliza utangulizi wako, endelea kwenye hoja ambayo tunaijadili, vinginevyo naomba uelewe mwongozo huu ninaokupa kutoka kwenye Kiti. Mheshimiwa Dkt. Mgimwa naomba uendelee. *(Makofi)*

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hiyo ilikuwa sehemu ya utangulizi kwa sababu imo ndani ya sheria. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba niendelee. Napenda kuongelea *Proceeds of Crime Act, Cap. 256*. Naungana na wenzangu wote kusema kwamba tusikubali utaratibu wa *'satisfied on balance of probabilities'*, iwe sehemu ya kuruhusu *confiscation order* wakati mtuhumiwa amefariki. Hiyo hakuna haki kabisa, wote tuungane suala hilo liondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nyingine ninayopenda kuiongelea ni *The Drugs and Prevention of Illicit Traffic in Drugs Act*. Suala hili kama walivyosema wengine na mimi naunga mkono kabisa wote ambao tunaona kuna wahusika

16 APRILI, 2012

wakubwa ambao wana-*finance importation* au *procurement*, sasa sheria itizame namna ya kuzuia tatizo badala ya ku-*deal* na matokeo. Kuna watu wana-*finance* uingizaji wa madawa ya kulevya, sheria ndiyo ilenge huko, namna gani tutazuia madawa ya kulevya kwa kutibu tatizo sio matokeo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa sababu nimeshasema ya msingi kabisa, naomba niishie hapa, lakini suala la *Loans Board* limesikika. (Makofi/Kicheko)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dokta Mgimwa basi nimegundua mpango wako wa ziada uliokuwa nao kwenye Bunge la leo. (Kicheko)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumsikia Mheshimiwa Dokta Mgimwa, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Moses Joseph Machali, nadhani tutakuja kuendelea jioni muda hautaturuhusu.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwanza kwa kunipa fursa ili kusudi niweze kuchangia hoja hii ya mabadiliko ya sheria mbalimbali. Kimsingi sitakuwa na mambo mengi ya kusema isipokuwa nina kipengele kimoja ambacho naomba wakati Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu atakapokuwa

16 APRILI, 2012

anahitimisha hoja yake, niweze kupata ufafanuzi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niipongeze Serikali kwa kuweza kuondoa hoja iliyokuwa inahusiana na mambo ya mikopo ya elimu ya juu kwa sababu imeonekana kuwa na upungufu ambao ni mkubwa sana kwa mujibu wa matakwa ya Watanzania hususani wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nitazungumzia kidogo kuhusiana na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa maana ya *Constituencies Development Catalyst Fund*. Mheshimiwa Akunaay alipokuwa akichangia amesema kwamba kwa sehemu kubwa imeweza kuangalia upande wa pili wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maana ya Tanzania Visiwani, kule Zanzibar. Yale mambo ambayo wamekuwa wanayapigia kelele, yameweza kufanyiwa mabadiliko, niipongeze Serikali kwa jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuja kwa upande wa Tanzania Bara, sasa hizi ni changamoto ambazo nazileta kwa Serikali, kimsingi sheria hii imekuwa ikilalamikiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Moja ya mambo ambayo yanajitokeza ambayo ni udhaifu katika sheria hii ya *CDCF* ni kama

16 APRILI, 2012

vile kuhusiana na namna ya kuweza kuwapata Wajumbe wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo katika Majimbo yetu. Sheria haijataja wazi nafasi ya Mheshimiwa Mbunge juu ya suala zima la kuweza kupatikana kwa hawa Wajumbe kwa maana ya Madiwani, wale Maafisa Watendaji wa Kata, ni nani hasa ambaye analazimika kuwateua? Je, ni Mheshimiwa Mbunge au ni Mkurugenzi wa Halmashauri au ni Mwenyekiti wa Halmashauri? Sheria haijaweka bayana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, marekebisho ambayo yameletwa, kwa kweli naomba niseme tu kwamba Serikali haijaweza kukidhi haja na matakwa ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, ni imani yangu, Serikali itaharakisha kuangalia namna ya kukidhi matakwa ya Waheshimiwa Wabunge juu ya mambo haya ambayo tulitegemea mtaweza kutuletea mabadiliko ambayo ni makubwa na pengine sasa Bunge liweze kujadili na kuangalia namna gani ya kuweza kufanya ili kuweza kupunguza *contradictions* ambazo tumekuwa tukizi-face tunapokuwa kwenye Majimbo yetu hasa tunaposhughulikia maendeleo ya Majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mdogo, imekuwa ikijitokeza katika Halmashauri mbalimbali, wakati mwingine Wenyeviti wa

16 APRILI, 2012

Halmashauri wamekuwa wakiwateulia Waheshimiwa Wabunge Wajumbe wa Kamati za Maendeleo ya Majimbo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukija kwenye sheria yetu, kwenye suala zima la *composition of the Constituency Development Catalyst Committee*, hakuna mahali ambapo sheria inabainisha Mkurugenzi atamteua nani kuwa Mjumbe wa Kamati hii! Wala Mwenyekiti wa Halmashauri husika atamteua mjumbe fulani labda Mheshimiwa Diwani fulani kuwa mjumbe wa Kamati hii au Afisa Mtendaji wa Kata kuweza kumteua, *no*, Mwenyekiti wa Halmashauri au Mkurugenzi kumteua Afisa Mtendaji wa Kata yoyote kuwa mjumbe wa Kamati ile, lakini haya yamekuwa yakifanyika na matokeo yake Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tunauliza hata maswali hapa, lakini jambo hili halijaweza kupatiwa ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nichukue fursa hii kuishauri Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jambo hili liweze kuharakishwa na pengine ningepomba kama inawezekana, ikishindikana katika Bunge la bajeti inayokuja, basi tuangalie katika Mabunge mengine ambayo yatafuata baadaye. Kwa kweli kuna tatizo, hata Mheshimiwa Mwambu

16 APRILI, 2012

amekuwa akilalamika sana, lakini bado hatujaweza kuona matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme mabadiliko haya ambayo tunafanya leo hii ya sheria mbalimbali, hayajaweza kukidhi matakwa ya Mfuko huu wa Maendeleo ya Jimbo. Wazanzibari nafikiri kilio chao kwa kiasi fulani kimepungua japo hata wao tena iko haja ya kuangalia juu ya vifungu hivi kwa sababu matatizo ambayo yanajitokeza kwa upande wa Tanzania Bara, hata na wao wataendelea ku-*face problem* mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi, tunapojaribu kuiangalia sheria hii, Wabunge kule kwenye Majimbo yetu inaonekana kama vile sio taasisi kamili, bado kwa sehemu kubwa tunaendelea kutegemea watendaji wa Serikali na wakati hii ni mihimili miwili ambayo ni tofauti kabisa. Kwa hiyo, kwa kuangalia sheria hii, twende mbali, ningomba Serikali iende mbali kwa kuweza hata kurejea ile *The National Assembly Administration Act ya 1988*, tukihusianisha na sheria hii ya *Constituencies Development Catalyst Fund*, tuziangalie kwa mapana yake na tulete mabadiliko ambayo yataboresha na hivyo Ofisi za Wabunge ziweze kuonekana kwamba ni taasisi kamili mpaka kule chini, kuliko utaratibu uliopo hivi sasa. (*Makofi*)

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu unakuta Ofisi za Wabunge, hazina wafanyakazi wa kutosha, Mbunge wa Tanzania anaonekana kama ni Dakitari, Mbunge wa Tanzania ni *Financial Institution*, Mbunge wa Tanzania ni Jaji, Mbunge wa Tanzania ni Afisa Kilimo, kwa hiyo Mbunge wa Tanzania ameonekana ni kila kitu. Mbunge wa Tanzania ni *Researcher*, tunafanya kazi katika mazingira magumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuiomba na kuishauri Serikali; kati ya sheria ambazo ni za msingi ili kuweza kuwafanya Wabunge kuwa *effective* na *efficient enough* ni kuhakikisha sheria hizi mbili *next time* zinaangaliwa kwa mapana yake na zisiletwe nusunusu kama ilivyofanyika leo hii, sheria ya *CDCF* bado kuna vipengele vingi ambavyo vina upungufu, sasa sijui wakati mwingine Serikali inapatwa na hofu gani, sielewi. Kwa hiyo, nitaomba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wakati anahitimisha hoja yake alieleze Bunge ni lini sheria hizi zitaweza kuangaliwa kwa mapana yake na kubwa zaidi wajaribu kukusanya na kusikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge ili kuhakikisha kwamba sheria hizi zinaweza kuboreshwa kikamilifu ili kuondoa changamoto hizi ambazo zinakabili ofisi za Wabunge.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niishie hapo, hicho ndicho kipengele ambacho niliona nikigusie kwa kina. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Machali, Mheshimiwa Amina Clement dakika zilizobaki unaweza ukazitumia?

MHE. AMINA A. CLEMENT: Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zilizobakia naona kidogo sana nitachangia jioni.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini?

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, langu ni dogo tu kwamba katika marekebisho ya sheria hii hasa ya *trafficking*, ya usalama barabarani, tatizo kubwa ninaloliona sio upungufu katika sheria. Ukisoma ule ukaguzi wa ufanisi alioutoa CAG, utagundua kwamba asilimia 74 ya ajali ambazo zinatokea barabarani kwa kweli zinasababishwa na uzembe wa madereva na uzembe huu unatokana kwa kiasi kikubwa sana na usimamizi wa sheria iliyopo.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza Matrafiki wetu wanakwenda na vitu vidogo vidogo tu. Juzijuzi mimi nilisimamishwa naulizwa una stika ya *fire*? Mimi nikamuuliza yule Trafiki, cha muhimu ni stika au ni ule mtungi? Mtungi ule ndiyo muhimu zaidi kuliko stika. Kwa hiyo, mimi nadhani hawa wanaosimamia sheria wasimamie sheria vizuri na wawe *serious* katika jambo hili, wanafuatilia vitu vidogovidogo halafu wanaacha yale mambo ya muhimu ambayo yanaweza yakashughulikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nizungumzie hili suala la madawa ya kulevya. Wenzangu wamesema vizuri sana. Sasa hivi ukiangalia katika Miji yote Tanzania mpaka Vijijini, mateja wanaongezeka tu vijiwani, lakini sheria ipo na tumeambiwa hapa kwamba kiwango cha madawa ya kulevya kinaongezeka, sasa unajiuliza yanapitia wapi? Maana yake ni kwamba rushwa imekithiri sana katika maeneo haya mawili, katika usimamizi wa Sheria ya Usalama Barabarani na katika usimamizi na udhibiti wa madawa ya kulevya. Kwa hiyo, kama walivyosema wenzangu, mimi ninachokiona ni kwamba pamoja na hizi sheria kutungwa na adhabu kuwekwa, twende kwenye misingi, kwenye sababu zinazosababisha utekelezaji wa hizi sheria uwe mgumu, tutatue hayo, haya mengine yatakuja kwa ziada.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano amesema Mheshimiwa Mnyika, hivi kipato wanachopata Trafiki wetu kinaendana na maisha wanayoishi? Mtu anasimama barabarani kuanzia asubuhi mpaka jioni, posho shilingi laki moja, hivi kweli inawezekana? Inatuingia akilini kweli? Sasa matokeo yake ni kwamba hizi sheria tutakuwa tunazitunga lakini tunatengeneza mtandao mwingine wa rushwa. Tuangalie, tuwawezeshe wale ambao wanasimamia hizi sheria ili wazisimamie kwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishafunga makabrasha yangu nikijua tunaairisha, ni hayo niliyokumbuka kwa harakaharaka niliyokuwa nimejiandaa. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini nakushukuru sana kwa kuwa mahiri wa kuchangia lakini pia kujali muda na kutusaidia kuongezea hoja ambayo iko mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, naomba labda nitoe tu tangazo moja ambalo lilikuwa limesahaulika. Mheshimiwa Steven Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu alileta ombi lake kupitia Ofisi yetu kwamba tuwatambue wageni wake watatu ambao ni wageni kutoka Jamhuri ya China wakiongozwa na Diwani wa Kata ya Ketale, Ndugu Mramba Simba, sijui kama bado wapo hapa ndani,

16 APRILI, 2012

sasa Mramba Simba ameongozana na Bwana Yong Fang kutoka Jamhuri ya Watu wa China na Bwana Duan Hong kutoka Jamhuri ya Watu wa China. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, sina uhakika kama nimetamka hayo majina vizuri lakini nimejitahidi kwa kadri ya uwezo wangu wote. Kwa hiyo, hawa wageni wetu ni wawekezaji, wamekuja kuona fursa za kuwekeza hapa nchini. Kwa hiyo, kama ni masuala ya uwekezaji basi Mheshimwa Waziri anaweza ku-*network* na Wabunge kuona wanawezaje kujisambaza katika nchi nzima kwa namna itakavyowezekana. Basi inatosha naomba mkae chini. Tunawakaribisha sana Ndugu Yong Fang na Bwana Duan Hong, karibuni sana Tanzania. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji bado ni ndefu, si ndefu sana lakini ninaomba niache nafasi kwa *Presiding Officer* atakayekaa hapa Mezani mchana kuona anaweza akaendeleza agenda hii kwa maana ya uchangiaji kwa kiasi gani, lakini tu nadhani kwa ustaarabu na kwa kusaidia maandalizi mema ya uchangiaji, niwataje angalau wachangiaji wa mwanzo wawili. Atakayeanza saa kumi na moja kamili atakuwa Mheshimiwa Mussa Haji Kombo na atakayefuatia atakuwa Amina Clement ambaye amesema anajiandaa kutumia dakika kumi na tano. Kwa hiyo,

16 APRILI, 2012

naomba hawa wajiandae na kuna orodha ya wachangiaji wanaofuata, tunaweza kuwapa nafasi kwa mujibu wa Kiti, kiongozi atakayekuwa amekaa Mezani.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, basi naomba nitishe shughuli za Bunge kwa asubuhi, tutaonana saa kumi na moja jioni.

(Saa 06.57 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa (Mhe. Sylvester M. Mabumba) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Naomba niwataje wachangiaji, tutaanza na Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Clement, baadaye Mheshimiwa Felix Mkosamali na Gosbert Blandes ajiandae. Naona Mheshimiwa Kombo hayupo, basi nimwite Mheshimiwa Mkosamali.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili na mimi niweze kuchangia mambo machache kwenye Muswada huu.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo napenda kuchangia ni kwamba tunapofanya marekebisho ya Miswada mbalimbali kama hii, tunapaswa kufanya *intensive amendment*, marekebisho makubwa. Ukiangalia Sheria ambazo zinaletwa, zimekuwa zinalalamikiwa katika maeneo mengi. Kwa mfano Sheria ya Mfuko wa Jimbo, imeletwa kufanyiwa *amendment* kwenye eneo dogo lakini malalamiko ni makubwa sana kwenye eneo hili. Kwa hiyo, tunapofanya *amendment* leo, *miscellaneous* ndogo, kesho *miscellaneous* ndogo, hata *Tanganyika Law Society* wameshauri hili wanapokuja kwenye Kamati zetu kwamba tufanye *intensive amendment* siyo leo kitu kidogo kwenye *amendment* hii, kesho kwenye *amendment* nyingine, inakuwa siyo utaratibu mzuri wa utungaji wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa nina mambo machache ambayo napenda kuchangia kwenye Muswada huu. Moja, ni kuhusu Sheria ya Usalama Barabarani (*The Road Traffic Act*). Tunataka tuingize mfumo ambapo *point* zitakuwa zinapunguzwa na ma-*Traffic* barabarani. Hili siyo jambo la kuingia kichwani kirahisi rahisi, siyo jambo la kuingia kichwa. Pia tunapitisha Sheria halafu tunamwachia Waziri akatunge *regulations* za makosa hayo, sisi hapa Bungeni hatujui yatakuwa ni

16 APRILI, 2012

makosa gani ambayo ukifanya watazi-*deduct* zile *point* za mtu. Makosa hatuyajui, yeye aende akayaweke kule, tunampa mamlaka makubwa ambayo ilitakiwa kuwe na *schedule* kwenye sheria inayoonesha makosa hayo ili sisi hapa wawakilishi wa wananchi tuyaone siyo Waziri ndio aende huko apange makosa yake, tutakuwa tumempa mamlaka makubwa ya ku-*legislate* wakati hiyo ni kazi ya Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri hatuwezi tukampa mamlaka ya kwenda kutengeneza *offenses*, kwenda kutengeneza makosa. Halafu watu wenyewe tunaowapa, angalia takwimu za *Legal and Human Rights Centre*, zimeonyesha kabisa hali ya rushwa ilivyojaa katika Jeshi la Polisi katika ku-*control* ajali za barabarani na vitu vingine, *issue* kubwa ni hiyo. Leo umwambie Polisi awe ana-*deduct point* kwenye leseni ya mtu, mtu anatoka Dar es Salaam mpaka kufika mpakani Rwanda anasimamishwa na ma-*traffic* 50, sasa hii leseni ikiwa na *point* 50 si itakuwa *deducted within one day*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima vitu hivi tuviangalie kwa makini na tuangalie tunawapa nguvu hizi akina nani na watu wa namna gani? Ninashauri kifungu hiki tusikipitisha, *we have to investigate on this* ndiyo tuweze kukipitisha. Tusiende

16 APRILI, 2012

tu kwa mkumbo, tumesikia nchi fulani, maana matatizo ya nchi zetu ambazo hazina falsafa za Sheria (*jurisprudence*) ni ku-*paste-paste* tu, tukisikiasikia India sijui wametunga Muswada gani na sisi tunaleta. Ukisikia Kenya sijui wapi, tunaleta huku, sheria hii kwa Tanzania bado. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napenda kuchangia juu ya Sheria nyingine ambayo tunaifanyia marekebisho. Sheria inayopendekeza *confiscation* kwamba mtu akifa mali yake iweze kuwa *confiscated*, tunakiuka misingi ya Sheria, Ibara ya 13(6)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kama ilivyofanyiwa marekebisho, inaeleza kwamba mtu akituhumiwa kwa kosa la jinai, asionekane au asihukumiwe kwa kosa lile mpaka Mahakama imthibitisha. Leo tunasema mtu akifa, *Attorney General* ata-*apply Order* mali ziwe *confiscated*. Hii *issue* ni pana sana. Mmeichunguza kwa upana wake mpaka mlete mabadiliko haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu watakufa ambao mali zao ni *co-ownership*, zinamilikiwa na mtu zaidi ya mmoja. Alikuwa na kesi Mahakamani, hamjaweka *provision* za kutuonyesha *circumstance* kama hizi, itakuwaje? Nyumba inamilikiwa na mke na mume, Sheria ya Ardhi, kifungu cha 69, imeleeza. Hamjaleleza *circumstances* kama hii zitakuwaje?

16 APRILI, 2012

Mmeeleza mtu atakwenda ku-*apply order* lakini hamjaeleza *Administration of Estate Act* itaathirika vipi na mabadiliko haya? Mtu ameshachaguliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi, *Order* imetoka, mazingira yatakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mabadiliko makubwa sana lakini pia yamekwenda kinyume na utaratibu wa Sheria. Mnasema baada ya pale mtakapo-*prove* itakuwa *beyond reasonable doubt*. Hiyo haipo, Katiba inatambua makosa yote jina ni ku-*prove beyond reasonable doubt* siyo *on balance of probability*. Sasa hiyo mmeitoa wapi wakati Katiba imeeleza waziwazi hivyo, je, hii Sheria haikiuki Ibara ya 13(6)(b)? Nataka majibu ya Serikali kwa sababu hiyo *crime* sasa unapokwenda ku-*transfer* kuifanya kama *civil*, umeitoa wapi hiyo *principle* wakati Katiba yetu bado iko vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nahitaji majibu sahihi marekebisha haya yanalenga nini na mazingira kama hayo yatakuwaje. Mazingira ya mali ambazo zinamilikiwa na watu wengine, mazingira ya kukiuka Ibara ya 13 na kadhalika. Nahitaji majibu sahihi kutoka kwa Serikali ili niweze kuunga mkono Muswada huu, nisipopata majibu, siungi mkono kabisakabisa. (Makofi)

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napenda kuchangia juu ya *amendment* zinazofanywa kwenye Sheria ya Madawa ya Kulevya Sheria, *Cap. 95*. Tumekuwa tunahudhuria semina nzuri sana za madawa ya kulevya na watu wa madawa ya kulevya wamekuwa wanakuja kwenye Kamati yetu ya Katiba na Sheria, wameeleza waziwazi tatizo siyo haya mabadiliko kwamba ndiyo yata-*cure* tatizo hili la madawa ya kulevya ni *system* nzima iliyopo pale. Angalia kesi ngapi zimeisha Mahakamani na kuwahukumu watu kufungwa au kutuhumiwa, hakuna!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii *amendment* bado ni ndogo. Tunahitaji *amendment* kubwa ambayo itatengeneza mfumo wa kudhibiti suala hili. Suala hili la madawa ya kulevya siyo kitu cha kitoto, watu wanao-*deal* na biashara hii ni ya vigogo kwa lugha nyingine, siyo kwamba ni watu wa kawaida kawaida, ndiyo maana tunatakiwa tufanye *amendment* ambazo zitatufanya tuweze kutatua tatizo hili si kufanya *amendment* ambayo inaacha *gaps* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Muswada huu nilikuwa nimejipanga kuchangia kwenye maeneo hayo. Nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii lakini nahitaji majibu sahihi katika maeneo hayo ambayo nimehoji Serikalini.

16 APRILI, 2012

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa nimwite Mheshimiwa Amina Clement, kama hayupo nimwite Mheshimiwa Moses Joseph Machali, basi nimwite Mheshimiwa Pauline Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache katika Muswada ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kukipongeza Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo CHADEMA kwa kuweza kushinda katika uchaguzi wa Arumeru. Hakika lile zoezi halikuwa jepesi, lilikuwa zito lakini wananchi wa Arumeru wameweza kututunza na hatimaye wameweza kutupatia Mbunge wa Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Chama changu kuendelea kukilaani kitendo ambacho kiliwapata Wabunge wenzetu wawili wa CHADEMA katika Mkoa wa Mwanza ambao waliweza kukatwa mapanga. Wabunge hao walitakiwa kuwepo katika kipindi hiki cha Bunge lakini kwa matatizo yaliyowapata, hawajaweza kufika katika Mkutano huu wa Saba.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuliomba Jeshi la Polisi na Serikali kwa ujumla waendeleo na uchunguzi haraka ili haki iweze kutendeka kwa sababu kama inafikia hatua viongozi wanaweza kukatwa mapanga kwa kiasi kile sijui sasa kwa wananchi inakuwaje? Mimi naomba wafanye uchunguzi wa kina lakini bila kujali itikadi za vyama, wajue wale ni viongozi na hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niwape pole wale ambao wamefiwa katika kipindi hiki na wapendwa wao. Mungu aendeleo kuweka roho za marehemu mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye Muswada huu. Napenda kuchangia katika maeneo mawili. Eneo la kwanza ni eneo la adhabu hizi ambazo zinakwenda kutolewa kwa wale ambao wanafanya makosa barabarani. Katika Muswada huu tunaona kwamba tunakwenda kukazia sasa adhabu kwa wale madereva ambao wanasababisha vifo vya wananchi wengi lakini ni katika Bunge lililopita tu tulipitisha faini kwa wale madereva ambao wanafanya makosa, kwa makosa yale ya barabarani tukapandisha toka faini ya shilingi 20,000 mpaka 30,000. Faini hiyo haijatekelezwa vizuri, leo tunakuja na adhabu nyingine.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ripoti iliyotolewa ya makosa ya barabarani, tumeona kwamba makosa mengi yanasababishwa na madereva kutofuata taratibu zile za barabarani lakini tunapokuja na adhabu nyingine pamoja na kwamba wamechajiwa faini tunakwenda ku-*deduct point* kwenye leseni. Ni sawa, lakini Serikali imefanya utafiti ili kujua kwamba ni kwa kiasi gani huu ndiyo utakuwa mwarobaini wa kwenda kukomesha makosa haya ya barabarani, tunakwenda sasa kuokoa vifo ambavyo vinatokea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe Serikali, ni kweli Sheria tunapitisha lakini utekelezaji ni jambo lingine. Waziri anayehusika na Idara hii, Waziri wa Mambo ya Ndani, ni vizuri akawa karibu na wale watumiaji wa barabara ili wajue ni sababu zipi zinasababisha ajali nyingi kutokea katika barabara zetu. Ukiangalia barabarani, madereva wanaendesha lakini kinachosababisha ajali magari mengine ni mabovu lakini yanapita. Utaona kila kituo kondakta lazima ateremke, aonane na ma-*traffic*, hili hatulisemi, tutakuja na *amendment* mbalimbali, tutaleta kupunguza *point* kwenye leseni, sawa lakini *how effectively?* Itafanya kazi kwa kiasi gani? Kama tuliongeza faini kutoka shilingi 20,000 mpaka shilingi 30,000 na bado ajali zikaendelea, ni suala la nchi kukaa chini na kutafakari. Je,

16 APRILI, 2012

tunaendelea kurekebisha hizi Sheria mpaka lini wakati katika utekelezaji kuna tofauti kubwa sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi niseme kwamba, ni vizuri utendaji ukaboreshwa, tutapitisha Sheria sisi kama Wabunge lakini ukiangalia hata zile leseni tu ambazo zimepitishwa hazina hata mwaka, zile leseni mpya, kuna taratibu ambazo zilisemwa kwamba unapohitaji leseni mpya ambazo zina hizo *point*, ni vizuri hao madereva wetu wakaenda shule au wakaenda kwenye Vyuo vya VETA waweze kupewa mafunzo wajue ni taratibu zipi wanazifuata wanapokuwa barabarani lakini ukiangalia jinsi ambavyo leseni hizo zinavyotolewa, utaratibu ule ambao ulitakiwa haufuatwi. Tumeshasema katika zoezi hili la leseni kuna harafu za rushwa, taratibu hazifuatwi. Dereva yeyote anaweza akakurupuka akapata leseni lakini Sheria inataka aende kwenye mafunzo, ni kwa kiasi gani tunawasimamia hawa madereva ili waende kwenye Vyuo vya VETA, kuhakikisha kwamba wanakwenda kwenye vyuo stahiki wapate hizo leseni baada ya kufuzu yale mafunzo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hili liangaliwe. Serikali iangalie ni wapi imekosea. Matibabu matibabu ya matatizo haya ya barabarani siyo kuleta *amendments* kila Bunge tukarekebisha Sheria hizi lakini wakati huohuo

16 APRILI, 2012

matatizo yanatokea. Mimi nishauri, Wizara husika waangalie, inawezekana sisi viongozi tunapanda magari yetu mazuri VX, tunakaa kwenye magari yenye viyoyozzi, hatupandi mabasi, hebu Idara husika ijaribu kupanda mabasi, wakatathmini suala zima la rushwa. Unapokuwa umepanda basi la abiria, utajifunza mengi na sisi viongozi hizo ni *public transport* tupande ili tuone yanayoendelea barabarani na kuelewa ni kwa kiasi gani hizi rushwa ambazo zinalalamikiwa zipo, ukipanda kwenye basi ndiyo utajua, lakini ukiwa na gari lako umepeperusha bendera huwezi hata siku moja ukajua kwamba kuna rushwa barabarani. Mimi niombe Serikali iangalie badala ya kuleta haya marekebisho mara kwa mara, wajaribu kutathmini tatizo ni nini, ni rushwa iliyokithiri, magari hayakaguliwi au ni kweli kwamba tunahitaji kuzisimamia hizi Sheria zetu na kuziboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kwamba katika Muswada baada ya sisi kupitisha, Waziri atakwenda kuangalia kanuni. Wenzangu waliotangulia wamezungumza kwamba ni vizuri makosa hayo yakabainishwa. Ni makosa ya namna gani pale ambapo leseni yako inakwenda kutolewa *point*? Wengine wamefika mbali kushauri kwamba Maaskari hao wasitumike katika kupunguza zile *point* katika leseni za madereva, hizi kesi ikiwezekana ziende katika Mahakama za Wilaya lakini kwenye

16 APRILI, 2012

Mahakama hizo twende mbele zaidi, tuna kesi ngapi zimerundikana kwa sababu tunaposema kwamba tumepitisha sheria, *point* zinakwenda kupunguzwa hatujaeleza *specifically* ni nani anakwenda kupunguza hizo *point*, pia ni tatizo. Ni sawa tunapitisha Muswada huu, lakini kwa upande mwingine mimi binafsi naweza nikasema kwamba hiki kipengele hakijajitosheleza, hakiko wazi kwamba hizo *point* nani anakwenda ku-*deduct*. Je, ni kosa gani? Hujafunga mkanda, *point* inakwenda kuondolewa au umesababisha ajali *point* gani inakwenda kuondolewa? Tahadhari hiyo izingatiwe kwa sababu mwisho wa siku ni kweli kama tutaweka tu makosa yote, dereva anayetoka pale Arusha kufika Dar es Salaam anafika mwisho wa safari leseni yake hiyo ime-*expire* kwa sababu amesababisha makosa mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie pia kwenye kifungu cha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Mimi niwapongeze ndugu zetu wa Zanzibar sasa mambo yao yameanza kuwa mazuri kuhusu huu Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Ni kwa muda mrefu walikuwa wakilalamikia suala hili na mimi kama Waziri Kivuli wa Muungano napongeza kwa sababu hili linatokea pia upande wa Zanzibar. Kwa upande mwingine, Sheria hii ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Wabunge tumepiga sana kelele hususan Wabunge wa Viti Maalum kwamba ni kwa nini tunatengwa

16 APRILI, 2012

katika Mfuko huu wa Maendeleo ya Jimbo hata kusimamia tu. Mimi napata shida sana kwamba Diwani wa Viti Maalum anaweza akaingia akasimamia ule Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo lakini Mbunge wa Viti Maalum ukanyimwa, Sheria haikuruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia hii Sheria Mama ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo inaeleza *composition* ya wale Wajumbe. Wameeleza pale, wamethubutu, kwenye kipengele (f) cha Sheria Mama cha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wameeleza kwamba hata *NGO* ambayo inapatikana katika lile Jimbo au *organization* zao za *NGO*, wanaweza wakatuma mwakilishi lakini Wabunge wa Viti Maalum, katika Halmashauri, wanaweza wakawepo wawili au mmoja, asiruhusiwe kwenda kusimamia zile pesa kwa ajili ya maendeleo ya Jimbo, mimi hili linanishangaza sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu alitujibu katika Bunge hili na Mheshimiwa Mwanri alitujibu, ninaomba TAMISEMI walifanyie kazi na Mwanasheria Mkuu, atuletee *amendment* kuhusu kipengele hiki. Kweli Wabunge wa Viti Maalum tumepiga sana kelele kwamba na sisi tunahitaji tusimamie hizo pesa. Sio kwamba tunahitaji tuzisimamie kama Wenyeviti, katika *composition* kwenye Kanuni ile ya 10 ya Sheria Mama wameeleza, yeye ndio Mwenyekiti wa ule Mfuko lakini inabidi walete *amendment*, Sheria inasema

16 APRILI, 2012

kwamba, wasizidi wale wajumbe saba katika Kamati ile ya Mfuko wa Jimbo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamsihi Mwanasheria Mkuu, aharakishe *amendment* hii kwa sababu, huu ni ubaguzi wa hali ya juu kwa Wabunge wa Viti Maalum. Inaonekana kwamba, hawana uwezo, wakati hawa Wabunge ndio wanaochapa kazi, ndio wanaosimamia, ndio wanaopambania maendeleo katika Mikoa. Hata hivyo, wameaminiwa kwa kiasi kikubwa, kama wanathubutu kusimamia na kutunza Mikoa, sembuse Jimbo? Ni kwa nini Wabunge hawa hawaruhusiwi kuingia katika Kamati ile walao hata kuona zile pesa zinagawanywa vipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linatusikitisha sana. Niliombe Bunge lako Tukufu, Mwanasheria anatusikiliza, Wabunge haturidhishwi na ubaguzi huu na tunaomba usianzie katika ngazi hii ya Taifa. Kama kule chini Halmashauri *representatives wa NGOs* wanaingia, kuna tatizo gani? Wabunge wanaume, acheni hofu na akina mama; mturuhusu tusimame tuweze kutetea kama zile pesa zinatumika vizuri au hazitumiki vizuri, lengo ni kuwaletea wananchi maendeleo, mwisho wa siku hizi pesa ziwe zimetumika vizuri. Hili ni la msingi, ninaamini katika *amendment* watakwenda kuzingatia hili. (*Makofi*)

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hilo la Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, nimeona kwamba, Sheria hii inarekebishwa kwa upande wa Zanzibar pamoja na kwamba, wanapelekewa sasa hizi pesa za Jimbo, kuna suala zima la ma-*signatories*. Katika Sheria Mama kwa huku upande wa Bara inaonekana kwamba, Mkurugenzi na Wahasibu wake ndio wanahusika kuwa *signatories* wa kwenda kusaini kutoa zile pesa, Madiwani huku hawahusiki. Ukiangalia katika Muswada tulioletewa tunaona upande wa Zanzibar, wanaingiza sehemu ya Diwani, kwamba Diwani na yeye aweze kushiriki. Mimi nilipenda kupata ufafanuzi kwamba, ni kwa nini katika Sheria Mama huku Madiwani wao wanasimamia tu na watendaji hawahusiki katika suala zima la kusaini, lakini upande wa Zanzibar, Madiwani hawa wameeleza katika Muswada kwamba, anaweza akaingia katika kile kipengele cha ma-*signatories*. Nimwombe Mwanasheria Mkuu, anapokwenda kujibu hili aweze kutupatia ufafanuzi wa ujumla kwamba je, ndio *amendments* zimeanza taratibu, ameanzia Zanzibar, upande wa Bara atarekebisha kihivyo au basi imewekwa kimakosa mahali hapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu. (*Makofi*)

16 APRILI, 2012

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia Muswada uliokuwa mbele yetu mchana huu wa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, pia napenda kutoa pole kwa wapigakura wangu ambapo Mwenyekiti wangu wa Kata amefiwa na mkwe, Mzee wa Nguinyaga, Mwenyezi Mungu amuweke mahali pema peponi, amina. Hali kadhalika dereva wangu amefiwa na dada yake, mchana huu ni mazishi. Basi niwatakie kila la kheri washiriki salama katika mazishi hayo na mimi Mbunge wao tuko pamoja katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza nimefarijika kuja kwa Muswada huu leo tena lakini kuja kwake umekuja na baadhi ya vipengele na vipengele vingine vimeachwa. Mimi kwanza, kwa kweli nimepatwa na huzuni kubwa sana; huzuni yangu kubwa ni kutokana na maeneo mawili ambayo yameachwa katika Muswada huu ambapo pale awali tulipokuwa tunaujadili kwa mara ya kwanza kabla hatujaurejesha Serikalini, kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho, vilikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha kwanza ilikuwa ni suala zima la Sheria ya Korosho.

16 APRILI, 2012

Mwenzangu Mheshimiwa Mariam Kasembe, amechangia hapa, lakini sisi watu wa Ukanda wa Pwani ambao korosho ni zao la biashara, kwa kweli tuna huzuni kubwa sana katika hili. Katika hili mpaka tunapata wasiwasi au kuna baadhi ya watu wana ajenda binafsi? Kwa sababu, haiwezekani korosho ndio zao la uchumi katika Mikoa ya Pwani, ukianza Mkoa wa Pwani wenyewe, Lindi, Mtwara, Ruvuma na tatizo kubwa lilikuwa ni suala zima la ule Mfuko. Leo hii inaonekana kwamba, Sheria ile bado tena imerudishwa nyuma na hatujui ni lini tena itakuja? Tunajua Wakuu wa Mikoa wamesafiri mara nyingi na Wakuu wa Wilaya, katika kuhakikisha kwamba Sheria hii inaweka utaratibu ili mradi kila Halmashauri iweze kupata fungu lake. Hivi kigugumizi hiki kinatoka wapi mpaka Serikali leo imeshindwa kuleta Muswada huu katika Bunge hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa hili tunapata huzuni, tunajua kwamba inawezekana kuna ajenda nyingine binafsi katika suala zima la uchumi wa zao la korosho. Nipende kuwaeleza kwamba, kutokana na hili kuna watu wengi, vijana wengi, wataathirika hasa katika Ukanda wa pwani. Kwa hiyo, sasa nimwombe Mwanasheria Mkuu wetu kuhakikisha kwamba, suala hili linafanywa haraka, kama leo halikuja basi tupate majibu ni lini Muswada huu utakuja ili mradi tuweze kuujadili kwa ajili ya wananchi wetu wanaolima zao la korosho. *(Makofi)*

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la mikopo ya wanafunzi na huu nao vilevile haukuja. Hili ni tatizo kubwa sana, sisi Wabunge wote tuliokuwa humu Bungeni ni mashahidi vijana wetu wanapata shida kubwa sana katika suala la Bodi ya Mikopo na matarajio yetu ni kwamba, Muswada huu ungekuja hapa leo tungepata uwanja mpana wa kuujadili kwa ajili ya mustakabali wa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wanafunzi wanatutazama nao walikuwa wanatarajia hiki kitu kitakuja lakini hakijaja. Naiomba sana Serikali iharakishe suala zima la Sheria ya Bodi ya Mikopo ili mradi tuweze kuwapatia vijana wa Kitanzania mikopo kwa sababu wengine mwaka huu hawakwenda Vyuoni kwa ajili ya kukosa mikopo. Tunajua kuna changamoto kubwa sana katika suala zima la Bodi ya Mikopo. Naiomba sana Serikali itupe majibu ya haraka ni lini Muswada huo utakuja ili tuweze kuujadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeeenda moja kwa moja katika vifungu vya Muswada, hasa nataka nizungumzie suala zima la Sheria ya *Traffic*. Bahati nzuri wenzangu wote wamechangia vizuri zaidi, lakini ningependa kuzungumzia *points* zitakazopunguzwa katika leseni za watu ambao wataonekana wamekutwa na makosa. Tatizo sheria

16 APRILI, 2012

haijatoa kigezo kwamba ni kosa gani mtu huyo atapunguziwa *points* ili hatimaye leseni yake ifutwe. Siku zote tunalalamikia tatizo la rushwa. Naomba niwaambie, kama hatutaweka vizuri kipengele hiki, tutakuwa tumeongeza kwa kiwango kikubwa kiwango cha rushwa kwa ma-*traffic* na kwa watu wetu ambapo madereva wenyewe ni watu hali ya choka mbaya kabisa. Namwomba AG akija kufafanua eneo hili, atueleze ni jinsi gani sasa hizi *points* zitawekwa ili kuweka wazi suala hili. Isije kuwa ni kwa makosa madogo ukakuta mtu ndani ya mwezi mmoja, leseni yake imeshakufa. Kwa hili, tutakuwa hatujatenda haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lilikuwa ni suala zima la kufilisi kwa mtu anayeonekana kwamba ametenda makosa ya kijinai. Mimi napendekeza sana, ni kweli kwa watu waliofanya ubadhirifu katika Taifa hili ni lazima wachukuliwe hatua za Kisheria. Hatuwezi kukubali kwamba watu wanafanya ubadhirifu na wanaiba pesa za wananchi halafu wanaangaliwa hivi hivi lakini siifikiani na utaratibu wa mtu hata hajafikishwa katika vyombo vya kutoa hukumu, mali zake zinataifishwa. Namshukuru ndugu yangu Mheshimiwa Mkosamali na wengine wameligusia suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana mwingine mali zake yuko *share* na mtu mwingine,

16 APRILI, 2012

sasa utataifishaje? Pia kuna suala zima la mirathi kwa sababu kila dini ina utaratibu wake wa mambo ya mirathi, kwa mujibu wa Sheria hii tutakuja kusababisha haki za watoto na yatima zikapotea. Namwomba AG anapokuja hapa atueleze jinsi gani Sheria hii itaenda sambamba ili kuhakikisha haki za watu wengine katika zile mali zinalindwa. Maana kama mtu hajahukumiwa na Mahakama, leo hii unasema mali zake zitaifishwe, inawezekana mali hizo amechuma na mke wake kwa utaratibu halali, je, tunachunguza vipi, kuna *investigation* gani itagundua mali hii ndio mali ya ubadhirifu na mali hii sio ya ubadhirifu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaambie ndugu zangu, mwanadamu yeyote anapokufa kitu kitakachobakia ni mirathi na mirathi sio haki ya aliyekufa ni haki ya watu waliochwa pale duniani na inagawanywa kwa mujibu wa taratibu na sheria zake. Kwa hiyo, namwomba sana AG atakapokuja hapa, utoe ufafanuzi wa kina katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la udhibiti wa dawa za kulevya. Ukiangalia tatizo la dawa za kulevya katika nchi yetu ni kubwa sana. Mimi siamini kwamba ni tatizo la kisheria, hapana, hili tatizo ni mtambuka. Kwanza, kuna tatizo la maadili katika Dunia kwa ujumla. Tatizo la maadili kwanza ni ajenda ya kwanza lakini maadili haya yana-*cross*

16 APRILI, 2012

cut sehemu nyingi. Jambo la kwanza hata uadilifu katika vyombo tulivyoviweka kwa ajili ya kusimamia haki, tumepata rekodi kwamba kesi nyingi zimepelekwa Mahakamani, je, ni ngapi watu wamehukumiwa? Kwa nini kila siku mateja wanaongezeka Dar-es-Salaam na miji mingine? Inaonekana sio tatizo la Sheria, kuna jambo lingine na hasahasa ni suala la rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa imani yangu ninavyoamini, bila kujipanga kama Taifa kutatua tatizo la rushwa, hatutaweza kutatua tatizo la dawa za kulevya katika nchi yetu. Watu ambao saa nyingine wanapelekwa Mahakamani ni watu wasiokuwa na nguvu kabisa, ni watu madhalili kabisa lakini *importers* wakubwa wa madawa ya kulevya tunawaacha na kila siku wanatamba na mabenzi yao barabarani. Jambo hili sio haki, Sheria iangalie ni jinsi gani ile *source* ya watu ku-*import* dawa za kulevya inapatikana na tunawabainisha vizuri. Tunaweza tukatunga Sheria, lakini kila siku watu wanajipanga na vyombo mbalimbali vimeeleza watu wanaohusika na biashara hii wengine ni viongozi wa sehemu muhimu na kada mbalimbali, hii ni hatari. Kuna watu wenye nguvu wanaohusika na suala hili na bahati mbaya wanaoathirika ni vijana wenzetu. Sasa hivi ukitembea katika miji yote, vijana wanatia huzuni, mtu anatemeka bila kutetemeshwa, hata ile

16 APRILI, 2012

kusema ukinywa *Coca-Cola* unatetemeka, mtu anatemeka hivi hivi, ni hatari kubwa sana. Tunapongea hapa maana yake tunazungumzia uchumi wa Taifa, ina maana baada ya miaka 10 ijayo Taifa letu litaingia katika janga kubwa sana, kama hatutafanya jitihada za kuhakikisha tunadhibiti *source* ya dawa za kulevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Sheria imekuja lakini ni lazima katika suala hili zima tuangalie ni jinsi gani tutaweza kudhibiti *ma-importers*, hili ni tatizo. Watu wengi wanaokimbilia dawa za kulevyo ndio maisha yao yako hatarini. Yako hatarini kwa sababu kuna watu wenye nguvu wanaotumia mikono yao na nguvu zao zote za kifedha kuhakikisha kwamba suala la dawa za kulevyo linaendelea kwa sababu linawanufaisha katika maisha yao. Kwa hiyo, ndio maana nimesema suala la dawa za kulevyo ni suala mtambuka, ni pana sana. Vilevile Viongozi wetu wa Dini nao watusaidie sana kwa sababu suala zima la dawa za kulevyo ni suala la maadili. Kama kuna watu ambao wanaona utajiri ndio ajenda pekee bila kujua kwamba siku atafariki, Mwenyezi Mungu ataenda kumhoji katika hilo, kama watu hao wapo na wanaendelea kutamba basi ni mtihani mkubwa katika Taifa letu. Kwa hiyo, tuna kazi kubwa ya kuwekeza katika maeneo hayo. (*Makofi*)

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala zima la majengo, biashara ilipofanyikia, hii ni *relative term*, sijajua wale waheshimiwa wanaokuwa wamefikia katika mahoteli yetu ya kitalii ambao wanafanya biashara hii ya dawa za kulevya na hao wenye hoteli ina maana tuwachukulie hatua? Ni lazima tuangalie tutafanyaje katika hili kwa ajili ya kidhibiti suala hili la dawa za kulevya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesimama mchana wangu huu wa leo, yangu ni hayo machache. Kubwa zaidi ni kushukuru sana kwa kunipa fursa hii kwa mjadala huu mpana. Baada ya kupata majibu mazuri ya Mheshimiwa AG, basi mwishowe naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (Makofi)

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nizungumzie suala hili la dawa za kulevya. Mie kwa *interest*, ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Idara hii iko chini ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wa Idara hii watu wanaowatafuta ni matajiri sana, wana uwezo wa kufanya lolote kwao lakini inasikitisha sana wanavyotunzwa, wanavyowekwa, kama Mkurugenzi wao anaishi hata Askari wa Mgambo anayemlinda hana wakati anaongoza Idara ngumu

16 APRILI, 2012

kama hii. Achilia mbali kwamba tutasema tunampa tamaa ya kuwa apokee rushwa, lakini pia kwa maisha yake na kwa Idara yenyewe hali ilivyo, mimi ningeiomba Serikali, haidhuru Serikali inaunda Tume au Kamati ya pamoja kulishughulikia suala hili, lakini hawa viongozi wao wanahitaji kutunzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la kukamata au kuzuia dawa za kulevya zisiingie nchini mwetu ziko njia nyingi, njia ya ndege, njia za meli, njia za vyombo vya baharini, magari ya nchi kwa nchi lakini leo maboti au vyombo ambavyo ni vya bahari vinaleta dawa hizi kwetu. Bahati mbaya sana uwezo wa kuvizuia vile vyombo au wa kuvifuata vile vyombo kwa uwezo wa vile vyombo ulivyo na uwezo wa nchi yetu ulivyo, kukamata dawa ni kwa bahati tu. Kwanza, hatuna uwezo wa kuzuia vile vyombo kuingia nchini kwa uwezo wa nguvu zake na hata mwelekeo wao ni tatizo; tunahitaji kuisaidia Idara hii, kuwapa vyombo vya kisasa ambavyo vitawasaidia kuweza kuzuia tatizo hili. Ikiwa tutaifanya Idara hii sawasawa na wale wanaokula ule unga wanasinzia saa 24, haitatusaidia. Ni lazima tujitahidi kuwaokoa vijana wetu katika matatizo kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Mfuko wa Mikopo ya Wanafunzi. Bahati mbaya mwenzangu ananiambia hauji lakini ninataka

16 APRILI, 2012

niseme athari zake za kuuzuia usije, ni athari kubwa sana. Ninachopenda kukuambia kwa sababu wewe ni Mbunge wa Jimbo, maombi tunayoyapata sisi Wabunge kwa wanafunzi hawa basi ni zaidi ya mishahara yetu ya mwezi au miezi miwili kwa mara moja. Ni lazima tuwe wa kweli, watoto wetu wa kike wanavyoharibika kwa sababu ya kukosa mkopo huu na hamkuwa *serious*, hamjafanya utafiti mkaangalia hali halisi ilivyo, bado tunataka kuwafanya watoto wetu waendeleo kuharibika na kupata maradhi, bado mnataka kutuongezea mzigo ambao hatuwezi kuukataa kwa watoto ambao wanatoka kwenye Majimbo yetu? Ninaomba sana Mwanasheria Mkuu, alitizame hili kwa manufaa ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumza sana hapa, hasa hii *CDCF* na suala hili la Viti Maalum. Wakati wa uhuru nchi hii, hasa tutazungumzia Zanzibar, wakati wa uchaguzi, Vyama vikuu *Afro-Shiraz*, *ZNP*, *ZPP*, mtu ambaye wanaona huyu ana uwezo wa kutusaidia katika Bunge, alikuwa hatizamwi anatoka wapi, wanatizama huyu tukimsimamisha hapa akishinda, uwezo wake utakisaidia chama chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema vyama vyetu vina demokrasia na vinasimamia demokrasia, hawa akinamama wapo wengine wana uwezo

16 APRILI, 2012

mzuri sana wa kuisaidia nchini, wanahitajika vile vyama vyetu ingekuwa bado utaratibu wa kupata viongozi wetu wa kugombania katika Ubunge. Vyama hivi vinapewa *seats* wanajua kiti hiki mgombea wangu akisimama anakipata basi tungekuwa tuna uwezo mzuri wa kuwapeleka hawa akinamama ili wakaweze nao watakapoingia ndani ya Bunge kama ni Mbunge wa Jimbo kama wale wengine wakaweza kusaidia nchi yetu demokrasia, tuache, mimi nafikiri tumefikia mahali tuachane na ukiritimba huu wa kuonekana katika vyama vyetu basi mtu atokaye kwenye jimbo hili basi huyo huyo ndiyo agombee, tutapata matatizo makubwa, tuwasaidieni hawa akinamama kwenye vyama vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwapeni nguvu, tutizame majimbo ambayo tunaweza tukawapeleka wakapata nafasi wakawa Wabunge, wakipata hawa Wabunge wa majimbo watakuwa na kiburi na jeuri kwamba yeye hakuchaguliwa na mkoa wala jimbo lake hiyo peke yake ni fursa moja nzuri lakini ni jambo la msingi sana vyama vya siasa ambavyo vinaleta Wabunge katika Bunge, wabadilisha utaratibu huu wa kura za maoni kutoka kwenye matawi kwa mtu aliyetoka katika jimbo lile kuna watu wengine wazuri hawawezi kupatikana kwenye majimbo mengine, lakini kwa sababu chama kile ni *seat* yake, ni *sure seat* akipelekwa atasaidia nchi,

16 APRILI, 2012

tuwape nafasi hiyo wananchi hasa akinamama na wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko huu wa *CDCF*, umezungumzwa sana hasa kwa Wabunge wanaotoka Zanzibar, ulikuwa una matatizo makubwa sana na bahati mbaya Sheria ya Muungano na Sheria ya Zanzibar ni mambo mawili tofauti. Lakini kwa muundo wa leo kutoka kwa Makamu wa Rais kwenda moja kwa moja kwenye ofisi ya Bunge itatusaidia sana kuondoa matatizo ambayo yamekuwepo, naungana sana na masahisho hayo. Lakini jambo ambalo linanisikitisha ni moja, tunauchukua huu mfuko kama unyanyasaji wa Kikatiba wa Zanzibar ulivyo. Tunahesabu *population wise*, jimbo la Mheshimiwa Mnyika lile lina kura ngapi sijui, lina kura laki nne, mwenyewe Mheshimiwa Mnyika huwa anasema lina kura zaidi ya *population* ya Zanzibar jimbo lile moja, sasa tunalichukua unapokuja unasema nahesabu kura anazopata Mbunge, hutizami kama ni *two steps* Mbunge wa Zanzibar kashinda kapata kura 5,000 nyingi, unauchukua mfuko ule unauhesabu na Mbunge wa Dodoma Mjini mwenye laki tano au TMK anakura laki sita, unatazama mfuko huo wa jimbo ambalo lina kura nyingi sana 4,000, kwa hivyo hata ule mchango tunawapa wananchi wetu wa maendeleo ni sawa sawa na zile kura tulizonazo.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wengine watasema tusibiri labda mabadiliko ya Katiba wengine watasema vipi lakini nilikuwa nikitaka niulize hili kwamba tunahitaji kuongezwa Bunge moja linapata milioni 70, jimbo, jimbo langu ninapata milioni 15 au 20 na tunaambiwa tuko haki Wabunge wote sawa sawa, Ubunge huo sawa sawa uko wapi? Naomba sana jibu hili lizungumzwe kwa wazi sana otherwise mie nitazuia kidogo siku hizi shilingi hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu korosho, sisi Zanzibar hasa Pemba tulianza kampeni ya kupanda korosho, ardhi ya Kaskazini Pemba inalingana sana na ardhi hii ya baharini Mtwara, Lindi, Rufiji, Kilwa na maisha yetu kule kwetu Pemba, korosho itakuwa kama ni tunatafuna tu, tunachoma na nini basi lakini maisha makubwa ni karafu, ukiwa huna karafu kule uraia wako una wasiwasi.

Sasa je, tunategemea kuwa wanasiasa zaidi kuliko kuangalia maisha ya watu wetu? Juzi watu wa Lindi walifanya maandamano makubwa sana ya kuomba haki zao juu ya korosho walipwe. Watu tunawakampeni limeni, tunapeleka dawa fanyeni hivi uzalishaji unakuwa mkubwa, unatushinda kununua tunawapa matatizo wananchi wetu. Na kwa sababu wanashida wewe unaweka bei shilingi 1,000 huiunui yule atakayekuja na shilingi 200

16 APRILI, 2012

atanunua, atauza umemsaidia nini mkulima yule zaidi ya kumdhalilisha na kumnyanyasa?

Naomba sana tulitazame suala hili, hili suala ni uti wa mgongo kwa maisha yao watu wa Kusini, nina *interest* sana ya Kusini kuelezea hivi kwa sababu ambayo watu wengi wanajua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga hoja mkono. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed na huyu ndiyo atakuwa mchangiaji wa mwisho.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mambo madogo yaliyo kidogo lakini yenye maana kubwa lakini nahitaji tafakari ya nguvu. Naanza na suala la dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue fursa hii kuwapongeza wale wote wanaotumia dawa za kulevya katika Kisiwa cha Pemba ambao kwa makusudi tu wameamua kuachana na shughuli hii na wameamua kuunda vikundi vyao kwa ajili ya kuelimisha wenzao. Wilaya ya Mkoani wanacho kikundi chao cha Soba, Wilaya ya Chakechake

16 APRILI, 2012

wanacho kikundi chao cha Soba na Wilaya ya Wete
wanacho kikundi chao kinaitwa Soba. (*Makofi*)

Lengo la vikundi hivi ni kuwatafuta wale ambao bado wanaendelea na kadhia hii na wakaweka sawa kwa kweli nawapongeza sana. Sasa tunapofikia mahali leo unaona kwamba kuna sheria nyingine zinazidi kuletwa kidogo inaanza kutupa wasiwasi kwa sababu sheria hii katika nchi hii zipo, sheria zimeundwa lakini sheria hazifuatwi. Leo baadhi ya vijana wameanza kujiweka sawa tunaanza kupanga tena masheria mengine. Mimi nilikuwa nashauri hebu tujaribu kuangalia kama ambavyo wenzangu walizungumza hapa kwamba tutazame ile mianja au mianya ambayo hizi dawa zinaingia katika nchi yetu. Tutakapoweza kuzidhibiti hizi njia za panya au njia zozote ambazo wanapitisha hawa watu hizi dawa hapo tutafanikiwa bila ya kutafuta sheria nyingine, lakini bila ya hivyo kila mwaka tutakaa hapa na tutaunda sheria nyingine. Lakini kinachonishangaza zaidi na huwa nakaa najiuliza hivyo Mwanasheria Mkuu na watu wake wanakaa wanaunda sheria kama hizi wakati sheria ndogo tu hapa inatushinda kutekeleza? Uvutaji wa sigara wa hadharani dogo linatushinda, watu wanavuta sigara wanavyopenda, wanavuta maeneo wanayopenda wanaangaliwa tu hivi hivi.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaanza kutunga masheria makali makali kwa ajili ya wavuta unga, hawa wavuta unga wameanzia kwa kuvuta sigara, hapa ndiyo ambapo wameanzia anamwambia mwenzake kishwea anapewa hapo ndiyo ambapo anaanzia. Sasa hebu kwanza tujaribu hizi sheria ambazo tunazo hebu tuzifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la leseni, tumezungumza sana katika Bunge hili kuhusu ajali za barabarani, tumetunga sheria mwaka jana hapa tumeipitisha kuhusu adhabu ya madereva leo hii tunaweka tena adhabu nyingine, adhabu ambayo itatokana na alama za leseni, ninachokisema ni kwamba tuna mamlaka Tanzania, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Majini na Nchi Kavu (*SUMATRA*) wana sheria nyingi tu, hebu tuipeni nguvu hii *SUMATRA* na wanafanya kazi vizuri sana *SUMATRA* na ni wa kupigiwa mfano kwa kweli. Hebu tuwapeni nguvu hiki kitengo ambacho tumekiunda ili tuweze kufanya hii kazi. Serikali tunapokaa, mnapokaa mkaunda tu sheria kwa kweli hii italetu usongo wa mawazo kwa hawa ambao tunawatungia hizi sheria. Kwa hiyo, nafikiri tukaeni tuangalie hebu tuipeni nguvu *SUMATRA* tuone namna gani itaweza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala la sheria hii ya polisi, kwa kweli tulitegemea

16 APRILI, 2012

kwamba sheria ile ingekuzwa na ikaenda mbali zaidi, lakini kipengele kilicholetwa ni kidogo mno, tunachosema sheria ambazo polisi wanazitumia nyingi zimepitwa na wakati, ni sheria ambazo tumezirithi kutoka kwa wakoloni. Hebu ziletwe tuziangalie upya tusidokoe kidogo kidogo kwa sababu kawaida ya sheria inakuwa ni kitu kama *link*, sasa tusinyofoe hapa kati tukaacha huku nyuma. Sheria nyingi tulizonazo tumezirithi kutoka kwa wakoloni na nyingine tumezichukua kutoka India. Nafikiri wakati umefika kwa Mwanasheria Mkuu sasa hivi kuziangalia sheria zote zinazoambatana na masuala ambayo wanafanyiwa na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia mimi nataka nizungumzie mfuko wa *CDCF*, niipongeze sana Serikali kwa kusikia kilio chetu hasa sisi Wabunge ambao tunatoka Zanzibar na kuweza kutuletea sheria hii. Mpangilio ambao wameuleta unaridhisha na unakubalika. Sasa kwa vile mfuko utaanzia katika Ofisi Ndogo ya Bunge iliyoko Zanzibar, na wewe ni shahidi kwamba bado Ofisi yetu ya Bunge Zanzibar haijafanya shughuli zake kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefika wakati sasa hivi kwa Ofisi ya Bunge kuhakikisha kwamba inaipa kila nyenzo, inaipa kila msaada na inawatengea fedha nzuri watendaji wa Ofisi Ndogo ya Bunge

16 APRILI, 2012

iliyopo Zanzibar ili kusije kukatokea matatizo wakati wa kushughulikia masuala haya ya mfuko huu kwa Wabunge. Tuna hofu fedha hizi zisije zikaingia pale halafu tena tukaanza kutafutwa ngoja aonekane Spika, hebu ngoja apatikane Naibu Spika, hapo itakuja kuwa vurugu mechi kidogo.

Kwa hiyo, tunaiomba sana Ofisi ya Bunge ihakikishe kwamba Ofisi Ndogo ya Bunge Zanzibar inafanya kazi kama ambavyo inafanya kazi Ofisi iliyopo Dar es Salaam ya Bunge na hii iliyopo hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache nakushukuru ahsante. *(Makofi)*

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu.

Pia napenda kutumia fursa hii kutoa maoni yangu kuhusiana na Sheria ya Mapato yanayopatikana kwa njia ya uhalifu. Naunga mkono mapendekezo hapa kwa asilimia mia moja. Kipengele hiki kinahusiana na ufilisi wa mali ya mtuhumiwa anayepelelezwana anapotoroka na inasaidia kuondoa mashitaka pale itakapotokea

16 APRILI, 2012

mtuhumiwa anayepelelezwa aliyeshtakiwa ambaye hukumu haijatolewa, pindi anapofariki, Mahakama iweze kutoa amri ya kufilisi mali ya mtuhumiwa huyo.

Kwa kufanya hivyo, itasaidia wale ambao wanafanya uhalifu wasiendeleo na vitendo vyao kwani imekuwa kama tabia na watu wanaofanya uhalifu wanapata sifa na wamekuwa wanapata mapato makubwa kutokana na vitendo hivi viovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wanaotetea haki za Kikatiba lakini tunatambua kwamba Ibara ya 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayotoa haki ya kumiliki mali, Ibara ya Katiba haiwezi kuruhusu haki ya kumiliki mali ambayo si halali. Haiwezekani mtuhumiwa leo aibe mali yake halafu ikatokea shitaka linaendelea mahakamani, muathirika (*victim*) haki yake ikoje, mtuhumiwa anapofariki. Hata siku moja, Katiba haiwezi kukumbatia uhalifu. Haiwezekani familia/mtu wa karibu na mtuhumiwa aliyefariki, akakaa na mali ambayo hakuipata kihalali. Kwa kuruhusu hili tutazidi kushamirisha ufisadi na wote tumekuwa tukipigia kelele ufisadi. Kwa kweli ni nyema mapendekezo haya ya Serikali yakapitishwa na Bunge lako Tukufu. Tusipopitisha mapendekezo haya wahalifu wataendelea kuwa tishio katika jamii na wahalifu wataendelea kuwa tishio kwa maendeleo ya

16 APRILI, 2012

uchumi wa Taifa letu na dhana hii itazidi kujengeka kwamba uhalifu ndiyo unaolipa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapotekeleza mapendekezo haya, hatutakuwa peke yetu kwani nchi kama Zambia, Namibia na Uingereza pia wanatekeleza. Wengi wanahofu kwamba haki haitatendeka, lakini vifungu vya 351 na 352 vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai vinaipa mamlaka Mahakama kufilisi mali iliyotumika katika kutenda makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa ufilisi wa mali iliyopatikana kwa uhalifu huwa unaanza kwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupeleka maombi katika Mahakama kwamba anahitaji kufilisi mali ya mtuhumiwa ambayo ilipatikana kwa makosa ya kesi ya jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na marekebisho ya Sheria za Usalama Barabarani ikiwa ni pamoja na marekebisho hayo bado askari wa usalama barabarani hawajabadilika kitabia. Bado askari wanakumbatia rushwa na vitisho kwa madereva barabarani. Weledi wa askari wa barabarani ni

16 APRILI, 2012

tatizo kubwa. Kisingizio cha mshahara na maslahi madogo ya askari polisi kisiwe ndio chanzo au sababu ya kuvunja maadili ya kazi yao.

Nashauri sheria itungwe ili kuwadhhibiti kwa kiasi kikubwa kwa askari wanaochukua rushwa barabarani ili kuondokana na vifo vingi vinavyotokea barabarani. Naunga mkono hoja.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwa kuipongeza Serikali kuleta Marekebisho ya Sheria Mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia sehemu inayohusu mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani.

Kuhusu kuwadhhibiti madereva wanaosababisha ajali kwa mujibu wa marekebisho yanayopendekezwa na Ibara ya 29 ambayo ina lengo la kurekebisha kifungu cha 25 cha sheria sura ya 168.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza mambo yafuatayo:-

Kwa kuwa msingi wa marekebisho haya ni kuweka utaratibu wa leseni za udereva kupewa alama maalum kwa namba pale mwenye leseni

16 APRILI, 2012

anapotenda kosa, basi alama hizo zitakuwa zikipunguzwa, ni vyema marekebisho yakatamka kuwa iwapo alama hizo zitapungua hadi kiwango kadhaa, hatua zipi zitachukuliwa dhidi ya dereva husika na pia iwapo mtu anaweza kupoteza sifa za udereva kwa alama zake kushuka katika kiwango kipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho haya lazima yaweke utaratibu tofauti wa madereva ambao wanaendesha magari ambayo kimsingi si ya hapa Tanzania, kwa mfano madereva wa Kenya, Uganda, *DRC* na kwingineko ambao huwa kwa namna moja au nyingine wanatumia barabara za hapa Tanzania, mfano ni vyema kufikiri zaidi kwenye kutoa faini kwa madereva hawa na si kutumia utaratibu wa kupewa alama maalum za namba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuchangia sehemu inayohusu mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma za Polisi. Ni vyema Muswada kuweka wazi kuwa amri zitolewazo na Inspekta Jenerali wa Polisi zitakuwa na nguvu sawa mbele ya sheria bila kujali amri hizo zimeshapishwa au hazijachapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya (ix) inayohusu mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria

16 APRILI, 2012

ya Uendeshaji wa Mashitaka. Ibara ya 24 unapendekeza marekebisho ya kifungu cha 18 cha Sheria namba 18(b)4 inaeleza; *"The orders, guidelines and instructions issued under this section may be published in the Gazette."*

Pendekezo langu ni vyema Muswada kuweka wazi kuwa amri, mwongozo na maelezo yaliyotolewa na Mkurugenzi wa Mashtaka yatakuwa na nguvu sawa mbele ya sheria bila kujali kuwa amri, mwongozo na maelezo yanayotolewa na DPP yamechapishwa kwenye Gazeti la Serikali au la.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba nichukue nafasi hii kuiomba Serikali ilete huo Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, ni muhimu sana huu Muswada na unasubiriwa sana. Ahsante.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuleta Muswada huu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu uliletwa hapa Bungeni katika Bunge lililopita na ukarudishwa kwa kuwa marekebisho yaliyokuwa

16 APRILI, 2012

yanapendekezwa hayakukidhi haja na Serikali iliahidi kwenda kuyaboresha na kuyarudisha Bungeni. Ajabu na kinyume cha matarajio ya Bunge hili Tukufu sehemu zote hizo hasa zinazohusu Bodi ya Mikopo zimeondolewa bila ya maelezo na sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikopo ya wanafunzi ni bomu linalotembea na wakati wowote linaweza kulipuka. Hivi ni kwa nini Serikali haijaleta mabadiliko katika sehemu hii ya Bodi ya Mikopo? Nashauri Serikali iletea mabadiliko hayo haraka sana ili kutatua matatizo ya Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kipengele cha Sheria ya Usalama Barabarani yaani *Amendment of the Road Traffic Act*, mapendekezo haya hayajaeleza ni makosa yapi yanayostahili kuondolewa alama za leseni. Ni vizuri sheria hii ikaeleza kwa ufasaha hata kwenye jedwali (*schedules*) aina ya makosa husika.

Pia kifungu hiki hakijawa wazi ni wakati gani mtuhumiwa anastahili kupunguziwa alama zake kwani maneno yaliyotumika ni "*commits or is convicted of an offence under this Act.*" Nashauri neno *commits* liondolewe libaki *is convicted of an offence.*

16 APRILI, 2012

Kuhusu kifungu cha 39 kinachoongeza 13A kuhusu kutaifisha mali za marehemu aliyekuwa anashitakiwa kabla ya kuhukumiwa na kutiwa hatiani, inawezekana Serikali ina nia nzuri katika suala hili lakini linapingana na Katiba ya nchi yetu, *presumption of innocence*, "every person is presumed to be innocent until proved guilty."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo katika misingi ya Sheria hakuna Sheria iliyo juu ya Katiba. Serikali iangalie uwezekano wa Sheria hii kupingwa Mahakamani kwa kuwa ni kinyume cha Katiba ya nchi.

MHE. AMINA ANDREW CLEMENT: Mheshimwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kubadili mfumo mzima wa marekebisho wa Sheria hii kwani kulikuwa na mlolongo mrefu mpaka hizo fedha kufikia kwenye sehemu husika.

Lakini masikitiko yangu ni pale pesa zinapofika Halmashauri tunapata usumbufu mkubwa sana wakati wa kutekelezwa miradi ambayo tumeiandaa Jimboni.

Ushauri wangu ni kwamba naomba yule afisa wa Halmashauri anayeshughulikia majImbo yote yaliyo kwenye Halmashauri husika anakua na majukumu mengi. Ombi langu naomba huyu afisa

16 APRILI, 2012

mipango mmoja kwa majimbo matatu hatoshi ni bora kwa hili kila jimbo awepo afisa wa kushughulikia mfuko na miradi ya jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati kabisa jinsi ambavyo amekuwa akifanya marekebisho kwa baadhi ya Sheria za Fedha ili kuonyesha na kurejesha nidhamu ya fedha za umma, ni sisi Wabunge nikiwemo mimi tuliomba sheria ziwe kali ili kuwezesha fedha iliyoibwa kurejeshwa, anachokifanya sasa hivi ndicho hicho tulichokiomba. Hongera sana!

Hata hivyo, kuna baadhi ya vifungu vingi vinavyohitaji marekebisho ili kuwezesha rasilimali iliyoibiwa na watendaji wasio waaminifu kurejeshwa Serikali (*stolen asset recovery*) kwa nini hujaleta marekebisho na lini utazileta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *DPP* awe na uhuru kamili kama ilivyo Kenya, Rwanda na hata Uingereza.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru

16 APRILI, 2012

Mungu. Moja kwa moja nianze kuchangia mada iliyo mbele yetu. Kwanza, naipongeza Serikali kwa kuondoa marekebisho ya Sheria ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwani marekebisho hayo yalikuwa yanakwenda kuendeleza ubaguzi na madaraja baina ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia sehemu ya 11, katika kifungu cha 25, chenye marekebisho cha Sheria ya Usalama Barabarani. Tatizo kubwa la ajali za barabarani si kwa sababu ya kukosa leseni bali kuna vyanzo vingi vinavyosababisha ajali za barabarani ikiwemo:-

- (a) Kukosa maadili ya udereva kwa madereva.
- (b) Kutozingatia Sheria za barabara kwa watumiaji wa magari barabarani.
- (c) Rushwa kwa Askari wa Usalama Barabarani iliyokithiri.
- (d) Barabara kukosa vibao vya alama za tahadhari.
- (e) Magari kutokukaguliwa kabla ya kuanza safari na mengineyo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuiomba Serikali ni bora kwanza kuzuia vyanzo hivi vya ajali ndipo tujadili kuweka alama kwenye leseni

16 APRILI, 2012

za madereva kama madhumuni ya kifungu hiki kinavyoeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye sehemu ya 16, inayopendekeza marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kusafirisha Madawa ya Kulevya. Tunapoongelea marekebisho ya kifungu hiki, tunatakiwa kwanza kuelezwa na Serikali mpaka sasa ni washtakiwa wangapi wa kesi ya madawa ya kulevya walioshtakiwa na kuchukuliwa hatua na ni wangapi walioachwa huru na ni wangapi kesi zao zinaendelea? Naomba majibu kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa tulilionalo hapa nchini kwetu, tumezoea kuangalia zaidi tulipoangukia na si tulipojikwaa. Tatizo hili tutaliondoa iwapo Serikali itawazuia na kuwakamata *super dealers* na siyo kuhangaika na watumiaji wadogo wadogo na wakulima wa mimea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii katika mchango wangu kumwuliza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kwamba; kama nchi yetu ina mipaka na mipaka hii inalindwa na mali zinazolingia na kutoka nchini zinakaguliwa; je, madawa ya kulevya yanaingilia wapi?

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba kuunga mkono hoja hii na kuipongeza Serikali kwa kuleta tena Muswada huu baada ya kuufanyia marekebisho upya na kuondoa Muswada unaohusu mikopo kwa wanafunzi, nikiamini ya kwamba, Serikali inahitaji muda wa ziada kuufanyia kazi ili haki za kiutendaji ziwe zimezingatiwa na tuweze kupata Sheria iliyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho ya leseni za madereva, naomba Serikali katika kutekeleza Sheria hii ni vyema kwanza kuangalia Sheria zilizopo ambazo zipo na ambazo hazina meno. *SUMATRA* ni Taasisi ambayo inasimamia mwenendo mzima na inadhibiti matumizi yote ya usafirishaji barabarani. Taasisi hii ina sheria nyingi ambazo hazitekelezwi; ni mategemeo yangu kwamba, uletwaji wa marekebisho haya yameendana na Sheria za *SUMATRA*. Bila hivyo tutawaletea wananchi wetu matatizo ambayo si ya lazima. Ili Serikali isije ikaingia katika mgogoro na madereva ni vyema kuoanisha Sheria za *SUMATRA* kwani Sheria zilizopo zinajitosheleza ila hazitumiki. Ni vyema Sheria hii ipelekwe Mahakamani na siyo polisi au kitengo fulani kutumia adhabu hii kwa kuwahukumu madereva kwani kufanya hivyo ni

16 APRILI, 2012

kutoa fursa nyingine kwa Watendaji wasio waaminifu kuchukua rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea katika Muswada huu, Serikali italeti marekebisha ya Sheria nyingi ambazo zimepitwa na wakati, ambazo tumezirithi wakati wa ukoloni na zinazotoka India. Kwa hiyo, kipengele hiki kimoja tu cha Jeshi la Polisi hakitaweza kuwa na meno bila ya kuangalia kwanza Sheria za Urithi tulizonazo, Sheria ambazo nyingi haziendani na wakati uliopo sasa.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kuleta Muswada huu Bungeni kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutoa pongezi na shukurani za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria na Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa ushauri kwa Serikali, ambao umesaidia sana Serikali kuweka mambo yake sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu nitachangia maeneo yafuatayo: Utaratibu wa kuweka alama kwa madereva; mtuhumiwa aliyefanya kosa na mali kutaifishwa; na Sheria ya Kuzuia Ugaidi.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na utaratibu wa madereva kuwekewa alama pale wanapofanya ajali. Mtindo huo ni mzuri na unaweza ukawa mzuri iwapo misingi ya haki itatendeka kwa kuwekwa wazi utaratibu mzima wa utoaji wa alama. Mkoa wa Dar es Salaam umekuwa na ajali nyingi ambazo zinasababisha vifo kwa wakazi wa Mkoa wetu ambazo zinasababishwa na madereva wa daladala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuweka alama kwa wale ambao watakuwa wanajirudia rudia basi adhabu kali itolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtuhumiwa anapofanya kosa mali zake kutaifishwa ni kweli na nakubaliana na marekebisho ya Serikali ya kutaka kutaifisha kwa mali. Pia ni sahihi kuwa watu wengine wanaiba au kudhulumu mali za watu, lakini wakati kesi inaendelea mtuhumiwa anakufa na mali ile inabaki katika familia ya mtuhumiwa, jambo ambalo siyo haki.

Ninaungana na mapendekezo ya Serikali katika kupitisha Sheria ya Kuzuia Magaidi kwa maslahi ya Watanzania ili na sisi Watanzania tufanye kazi zetu kwa amani na utulivu.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

MHE. SAID R. BWANAMDOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nina hoja chache zifuatazo:-

Kwanza, iwepo au iletwe Sheria ya Bodi ya Mikopo, itakayotoa utaratibu mzuri wa mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Pili, kuna tatizo kubwa sana la madawa ya kulevya hususan kwa vijana wetu. Mara nyingi waathirika wakubwa ni vijana wasio na uwezo na kwa bahati mbaya sana wahusika na biashara hii ni matajiri wakubwa sana.

Tatu, utaratibu wa sasa wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo uendeleo kwani kugawa fedha kwa misingi ya usawa baina ya Majimbo ya Zanzibar na Bara siyo sahihi sana. Hoja ya msingi ni kuongeza fedha katika Mfuko huu na wala siyo kugawa fedha kwa kufanana baina ya Majimbo yaliyopo Zanzibar na Bara.

Nne, Sheria ya Madini iletwe tuiipitie upya kwani ina upungufu sana.

16 APRILI, 2012

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa uhai na afya yangu.

Pili, naomba kuchangia juu ya Sheria zifuatazo:-

Sura ya 168, Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo. Nielewavyo mimi ni kuwa, Mfuko wa Kuchochea Mfuko wa Jimbo umekuwepo kwa ajili ya matumizi ya Wabunge wa Majimbo tu, kwa vile ilipokuwa inatungwa, Wabunge wa Viti Maalum utaratibu huo haukuwepo. Hivi sasa utaratibu huo wa Wabunge wa Viti Maalum upo na kupatikana kwao ni kupitia Kata na Matawi yote ya mkoa husika, wakijinadi wakitoa ahadi ni nini watawafanyia wanawake kwa mkoa mzima kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake ndio huhitaji maendeleo tena makubwa, wao ndiyo walezi wa familia ikiwa ni baba, watoto na makundi mengine. Katika nchi hii na nchi nyingine hapa duniani ndiyo wapiga kura; hivyo, wanawake hawa wanahitaji kukumbukwa sana na kusaidiwa kusukumwa katika kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Wabunge wa Viti Maalum ndiyo wawakilishi wa wanawake

16 APRILI, 2012

ambao ndio wajasiriamali na wainuaji wa uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu kuwa Serikali inapowafikiria Wabunge wa Majimbo kwa kuwa-*support* na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, basi na Wabunge wa Viti Maalum nao wafikiriwe ili Mfuko huo uwapunguzie umaskini wanawake na familia zao. Tukumbuke kuwa mwanamke ndiyo mleta maendeleo na ndiyo muihua uchumi wa nchi hii.

Sura ya 200, Sheria ya Kuzuia Biashara ya Dawa za Kulevya; ni rai yangu kuiomba Serikali iangalie kwa undani watu wote; wakubwa kwa wadogo, wanaoingiza madawa ya kulevya kwa ajili ya biashara, wakamatwe na Sheria ichukue mkondo wake kwa sababu ni wabinafsi, wauaji, wanajali maslahi yao binafsi na hawajali ustawi wa nchi yetu. Tanzania ndiyo maana idadi kubwa ya vijana wanaotumia madawa hayo hawazalishi, tena wanakuwa mazezeta, hawachangii katika uchumi wa nchi wanakufa. Naomba Serikali iweke *control*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia ingeweka *good control* hata kwa madawa ya hospitali kama vile *morphine, pethidine largacti valium* na *phenobarbiton*, kwa sababu haya mara nyingine

16 APRILI, 2012

hayatumiki ipasavyo, yanaibiwa yanauzwa na kutumiwa kama madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja na kushauri yafuatayo:-

Kuhusu Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, napendekeza Mfuko huu uimarishwe zaidi na ikiwezekana uhusike moja kwa moja na kuwekwa kwenye Mfuko huu, rasilimali za kujenga na kuendesha Ofisi za Wabunge ambazo zimezorota na kumwacha Mbunge akikosa hadhi ya nafasi anayosimamia. Vilevile sijaona umuhimu wa Wabunge wa Viti Maalum kupewa fedha hii kwani hawana jimbo; watachochea jimbo gani? Muhimu ni ushirikiano.

Leseni za madereva; napendekeza eneo hili liangaliwe kwa makini kwa vile ni eneo linalolalamikiwa kwa kukithiri kwa vitendo vya rushwa. Pamoja na mapendekezo yanayowekwa kwa kutumia mahakama, bado mahakamani hapo lipo tatizo la rushwa. Pia ningeshauri yabainishwe makosa ambayo yatahusika moja kwa moja na kunyanyasa dereva kuanza kupoteza hadhi na hatimaye kunyang'anywa leseni yake na kama

16 APRILI, 2012

lazima mahakama itumike, iwe katika ngazi ya Hakimu Mkazi na Mahakama za Mwanzo zisipewe hadhi hiyo.

Sehemu ya kumi na tatu ya Muswada iliyoletwa na Serikali namna ya kukabiliana na mkosaji aliyefariki au kutoroka. Hii ni kukiuka misingi ya katiba na haki za binadamu ambayo nchi yetu imeridhia, pia ni kinyume na dhana ya utawala bora, mahakama ndiyo chombo pekee cha kumtia mtu hatiani.

Udhibiti wa dawa za kulevya ni tatizo kubwa, mwarobaini wake bado haujapatikana na inawezekana viongozi mbalimbali wanahusika na kwa sababu ya uzito wa wahusika, hapajapatikana mwarobaini. Ninashauri jambo hili liwe mtambuka na viongozi wote katika jamii mama, madhehebu ya dini na viongozi wa kisiasa, tusaidie jambo hili lina nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napongeza kwa kuleta mapendekezo mbalimbali ya sheria zilizotolewa. Kuhusu suala la mikopo, liangaliwe kwa kina hasa kwa wasimamizi wa mikopo hiyo. Bodi ya Mikopo itoe urasimu uliopo kwani eneo hili lina matatizo

16 APRILI, 2012

makubwa sana. Ninaishauri Serikali iweke mipango mizuri ya usimamizi wa kutekeleza Sera ya Mikopo na kuwawajibisha viongozi wote wanaosababisha kushindwa kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la sheria barabarani, naomba sana Serikali ichukue hatua kali juu kudhibiti Watumishi wa Mambo ya Ndani, Askari Polisi na *Traffic*, wanaoruhusu vitendo vya ukiukwaji wa Sheria za Usalama Barabarani wafukuzwe kazi. Askari wa Usalama Barabarani wamekuwa ni chanzo cha kusababisha ajali nyingi zinazotokea mara kwa mara kwa uzembe wa kuruhusu magari mabovu, mwendo kasi na madereva kuendesha magari au pikipiki wakiwa wamelewa na kuruhusiwa na Askari wa Usalama Barabarani kwa kupewa rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la madawa ya kulevya bado halijapewa nguvu ya kutosha na Serikali, kwani vijana wengi wanaongezeka kuyatumia kuliko huko nyuma. Serikali idhibiti maeneo muhimu yanayoingiza madawa ya kulevya kama *Airport*, Bandarini na Vituo vya Mipakani, kuwe na udhibiti kuingiza madawa hayo ambayo yanapitishwa kwa makusudi na wasimamizi wakiruhusu kuyaingiza kwa kupewa rushwa.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali haijafanya kile ambacho kinatarajiwa na wananchi. Wanaleta madawa ya kulevya, Serikali inawafahamu lakini hatua kali zichukuliwe juu ya hao wanaoleta madawa hayo. Tunaiomba Serikali vigogo wote wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. GOODLUCK JOSEPH OLE-MEDEYE:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kuwasilisha mapendekezo haya ya marekebisho ya sheria mbalimbali. Marekebisho haya yataboresha sheria zinazohusika ili haki itendeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (*CDCF*), imeelekeza kuwa Mfuko uwe na akaunti yake benki. Hata hivyo, katika Jimbo la Arumeru Magharibi hadi leo Akaunti ya Mfuko wa Jimbo haijafunguliwa kwa maelezo ya *DED* kuwa Hazina imezuia akaunti isifunguliwe. Kwa kuwa lengo la kuwa na Akaunti ya Mfuko ni kwa ajili ya kuongeza udhibiti wa fedha, naomba maelezo ya sababu zipi zimefanya Wizara ya Fedha izuie ufunguaji wa akaunti kinyume cha sheria.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. AUGUSTINE M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja yenye kufanya marekebisho kama inavyoletwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unalenga katika kuboresha Sheria zilizopo za barabarani, kudhibiti dawa za kulevya na kadhalika. Napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta marekebisho haya kwa wakati muafaka. Hata hivyo, kuwepo kwa kiwango kikubwa cha adhabu katika sheria huku vyombo vinavyohusika na usimamizi wa michakato ya kuwatia hatiani wahalifu vinaonesha udhaifu katika kuharakisha upatikanaji wa haki bila upotoshaji.

Kwanza, Jeshi la Polisi ndilo hasa chanzo cha utekelezaji mzima wa sheria zote nchini kwa kuanzia upelelezi, ukamataji na kushtaki wahalifu Mahakamani. Panapokuwa na udhaifu katika Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa Sheria mbalimbali nchini hasa inapotokea kunakuwepo na tuhuma za rushwa katika Jeshi la Polisi ambapo Polisi wasiokuwa waaminifu hupokea rushwa na hivyo kutofikishwa Mahakamani ambako ndiko hasa haki hupatikana.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Tanzania ndicho chombo pekee kinachoweza kuleta mabadiliko katika nchi hii iwapo kitafanya kazi kwa uadilifu. Bila kuwa na Mahakama inayosimamia sheria na utekelezaji wake basi sheria zote zinazotungwa na Bunge hili hazitakuwa na maana yoyote hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ilianganalie kwa makini suala la ongezeko la dawa za kulevya nchini. Bila kupatikana hatia kwa watuhumiwa wa dawa za kulevya, kunaonesha dawa zinaathiri kwa kiwango kikubwa. Bila kuwatia hatiani na kuwaadhibu wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya tutakuwa na Taifa lenye watu wengi walioathiriwa na dawa za kulevya na mwisho wake fedha nyingi za Serikali zitatumika kuwatibu wale wanaoathirika na dawa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuapisha Tume iliyoundwa kwa Sheria tuliyopitisha wenyewe hapa Bungeni ya kukusanya maoni ya Katiba Mpya. Pia nampongeza Mwenyekiti na Wajumbe wote walioteuliwa.

16 APRILI, 2012

Naomba nianze na utangulizi wa ushauri wa kurekebisha mfumo wa kuleta marekebisho mbalimbali ya mabadiliko (*amendments*) ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri kwamba, kila *amendment* iwe inapita kwenye Kamati Mama, Kamati husika na jambo ambalo Sheria hiyo inahusu. Mfano, kama ni Sheria ya *Loans Board*, basi Kanuni za Bunge zielekeze bayana kwamba Kamati husika ambayo ilihusika na Sheria mama, inahusika. Hivyo utaratibu wa kuleta Marekebisho ya Sheria tofauti 16 katika Muswada mmoja wa *Miscellaneous amendment* usiwepo, uangalie upya. Hii itafanya mabadiliko ya Sheria mbalimbali yapitie Kamati husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 25 cha Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168 (*The Road Traffic Act*). Marekebisho yanashauri kwamba kila dereva atawekewa *points* katika leseni yake na atakapotenda kosa basi pointi zile zitapunguzwa, wazo ni jema. Naomba ufafanuzi wa kupunguza hizo *points*. Je, zinapunguzwa barabarani au Mahakamani? Maana kwa mujibu wa Katiba Mahakama ndiyo inatafsiri sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri kwamba yawepo makosa ya aina fulani fulani *categories* za makosa. Vitu kama *fire extinguisher*,

16 APRILI, 2012

reflector, vipewe adhabu kama ilivyo kwenye sheria na sio kupunguza *points*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho kwenye Sheria ya Mapato kwa Njia ya Uhalifu (*Amendment of the Proceeds of Crime Act*). Marekebisho yanapendekeza mtuhumiwa anapotoroka au kufariki, Mahakama iweze kutaifisha mali yaani kutoa amri ya kufilisi mali ya mtuhumiwa huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni zuri sana, lakini anapofariki kabla ya kuthibitisha kwamba ana hatia lazima suala hili liangaliwe. Anapotoroka inabidi Sheria ya masuala ya dhamana iboreshwe ili anapopewa dhamana ielezwe wazi kuwa akitoroka hata kabla ya kutiwa hatiani basi mali inayohusika itaifishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo mtuhumiwa atafariki naomba tuangalie kwani *Universal Declaration on Human Rights* inaeleza *rules of natural justice*. Katiba yetu pia inaeleza *a person is not guilty until proved guilty*. Mbona jambo hili linapingana? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni marekebisho katika Sheria ya Kuzuia na Kusafirisha Dawa za Kulevya. Maoni ya Kamati ni kwamba, napendekeza kuwepo na *minimum sentence*.

16 APRILI, 2012

Naungana na mapendekezo mengine yote ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuchangia machache katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Serikali kwa kuleta Muswada wa Sheria ya Usalama Barabarani, kwa sababu kumekuwepo na ongezeko kubwa la ajali za barabarani hususan katika mabasi ya abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashuhudia ajali nyingi za mabasi ya abiria ambazo zinasababisha familia nyingi kupoteza Wazazi ambao ndio nguzo muhimu za familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri na maoni katika Muswada wa Sheria ya Usalama Barabarani kipengele cha 25 (a):-

- Mamlaka kwa Waziri ni mapana, yaangaliwe upya na kwa ufanisi zaidi;

16 APRILI, 2012

- Utekelezaji wa sheria usisitizwe, sio tu kuishia kupitisha Sheria ambayo haitekelezwi; na
- Kupunguza *points* kwenye leseni za udereva, ni sahihi lakini liangaliwe kwa kina zaidi hasa kwa makosa ya kizembe kama kuendesha huku ukiwa umelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni marekebisho ya Sheria kuhusu dawa za kulevya. Vijana wengi wa Tanzania wanazidi kuteketea kutokana na matumizi ya dawa za kulevya, hivyo nasikitika sana kupata taarifa kuwa uingizaji wa dawa za kulevya nchini Tanzania unaongezeka kwani kiwango cha dawa za kulevya kinaongezeka, lakini cha kusikitisha pia watuhumiwa wa dawa za kulevya wanapungua. Kulikoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri au kutoa maoni katika Sheria inayohusu dawa za kulevya kama ifuatavyo:-

- Tume ya Kuratibu udhibiti wa dawa za kulevya nchini inafanya kazi nzuri lakini inakwamishwa katika baadhi ya mambo. Kwa mfano, kuna baadhi ya watuhumiwa wakubwa wanakamatwa na dawa za kulevya lakini wakifikishwa Mahakamani

16 APRILI, 2012

wanapewa dhamana kinyume na taratibu za kisheria. Je, hii si rushwa?

- Kuongeza adhabu kwa watuhumiwa wa dawa za kulevya si tija kama hakuna utekelezaji wa sheria kwa wakosaji hao hasa wale wanaoingiza dawa hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na timu yake yote kuandaa Muswada huu na kuuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya *Road Traffic Act*. Kipengele cha 25A(1) cha Muswada kinaeleza kutolewa kwa leseni za madereva zenye *points* ambazo zinakuwa zinapunguzwa kila dreva atakapotenda kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza sheria hii iainishe idadi ya hizo *points* zitakazowekwa kwenye leseni na kuainisha pia vigezo vitakavyotumika kupata hizo *points*. Sheria hii ioneshe au kuainisha ni makosa gani hayo yatakayosababisha *point* kuondolewa makosa hayo yaelezwe wazi na Watanzania wote waelewe ili

16 APRILI, 2012

yeyote atakayepunguziwa *point* kwenye leseni yake asilalamike kuonewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua tatizo kubwa la rushwa barabarani. Trafiki waliopo barabarani hawatekelezi wajibu wao ipasavyo na wengi wanakula rushwa na hivyo kuruhusu madereva wazembe, magari mabovu na matokeo yake ni Watanzania wengi kupoteza maisha kwa ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa *points* hazitaoanishwa na aina ya kosa linalostahili kupewa adhabu ya kuondoa *points* kuwekwa wazi kuna wasiwasi wa kuongezeka kwa rushwa au watu/dereva kupewa adhabu kali kwa sababu tu hakuna rushwa/hana pesa.

Kifungu 25A(2) – neno “*May make regulation*” kinatia *option* Waziri kuweka *regulation* au kutoweka *regulation*. Hili ni tatizo kwani tumekuwa tunatunga sheria hapa, zinachukua muda wa miaka miwili hadi mitatu bila kuwa na *regulation* na hivyo kusababisha sheria kutotekelezwa kikamilifu. Hivyo, napendekeza badala ya “*May*” litumike neno “*Shall*”. Pia Waziri anapewa mamlaka makubwa sana, akiwa siyo mtendaji mzuri mambo hayaendi.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu marekebisho ya Sheria ya Madawa ya Kulevya (*Cap. 95*). Tatizo la dawa za kulevya ni tatizo kubwa sana hapa nchini. Nguvu kubwa ya Taifa imeharibika, vijana wengi ambao wangeweza kuliletea Taifa hili uwezo mkubwa kiuchumi, kijamii na nyanja zote wamejitumbukiza kwenye kuvuta madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara hii ina mtandao mkubwa na wanaojihusisha na biashara hii ni watu wenye uwezo mkubwa na wengine ni viongozi kwenye ngazi mbalimbali za Serikali. Athari kubwa wanaoathirika vijana na wengi wao wanapoteza kabisa mwelekeo wa maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu inayotolewa kwenye sheria hii kwa wale wanaokutwa na madawa ya kulevya ni ndogo sana (faini ya Tsh. 10,000,000) *is just a peanut*) haitoi somo hata kidogo kwa walengwa. Nchi nyingine wanawanyonga wale wote wanaokutwa na madawa ya kulevya, hapa kwetu tunatoa adhabu ndogo na ndiyo maana tatizo linaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina nia ya dhati ya kupambana na biashara hii ya kulevya hapa nchini. Hivyo, ni vizuri tuweke adhabu kali zaidi

16 APRILI, 2012

hata ya kuwanyonga hasa wale wanaoendesha mtandao huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kipengele 13A(1) na (2). Naunga mkono mapendekezo ya Serikali kuhusu kukamata mali zote zilizopatikana kwa njia ya wizi na zisizo halali kwa manufaa ya umma. Ikiwa vielelezo vyote vitaonesha kweli na haki itendeke kutokumwonea mtu au familia yake ikiwa mtu huyo atakuwa hayupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri uchunguzi ufanyike vizuri sana na tahadhari zote zichukuliwe ili kuondoa mazingira yote ya uonevu na watu kutoonewa kwa kubandikiwa kesi zisizostahili.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria itamke ushiriki wa Wabunge wa Viti Maalum kuwa Wajumbe halali katika Mfuko huo wa Jimbo.

Sheria iweke mkazo kwa Wajumbe halali tu ndio waweze kushiriki vikao vya Mfuko wa Jimbo, kwa kuwa baadhi ya maeneo, Wenyeviti wa Halmashauri wanaingia katika vikao hivyo ili hali wao si wajumbe.

Sheria iongeze uwakilishi wa asasi za kiraia na Mashirika ya Dini katika maeneo husika.

16 APRILI, 2012

Sheria iweke mkazo wa taarifa za Mfuko wa Jimbo ili uweze kupitiwa na Mabaraza ya Madiwani kabla ya fedha husika kupelekwa kwenye miradi husika.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu marekebisho katika kifungu cha 25 cha Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168. Madhumuni ya marekebisho haya yanalenga kuanzisha kifungu kipya ndani ya sheria hii cha kushughulikia na kusimamia leseni za udereva kupewa alama maalum kwa namba na pale mwenye leseni anapotenda kosa, basi alama hizo zitakuwa zikipunguzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri leseni za udereva kupewa alama maalum kwa namba na pale kwenye leseni anapotenda kosa kufanyike Mahakamani ili kuweka uwazi zaidi na kupunguza mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kushauri ikitokea dereva kawekewa alama na akakaa kwa kipindi cha miaka zaidi ya miwili bila makosa afutiwe adhabu zile za mwanzo maana kukaa muda wa zaidi ya miaka miwili bila makosa inamaanisha dereva atakuwa amejirekebisha, kwa hiyo ni vizuri suala hili likaangaliwa kwa kina.

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri alama zitakazopelekea kuwekwa kwenye leseni si kila kosa ustahili alama, yawe baadhi tu ya makosa.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo (CDCF), Sheria iyangaliwe ili Wabunge wa Viti Maalum waweze kushirikishwa kwa kumshirikisha Mbunge wa Jimbo katika maamuzi. Hii itaondoa uwezekano wa fikra na maamuzi kinzani baina ya Mbunge wa Jimbo na wa Viti Maalum hususan kama Mbunge wa Viti Maalum atatumia fursa hiyo kujjenga ili mara uchaguzi ufikapo amuengue Mbunge wa Jimbo ingawaje ni haki yake ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa zinazopatikana kwa ubadhirifu au madawa ya kulevya ni muhimu zitozwe kodi kama kipato halafu kesi iendelee. Utaratibu huo uko Marekani, kipato halali na haramu vyote lazima vitozwe kodi.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu Bungeni. Napenda kutoa maoni yangu katika maeneo yafuatayo:-

16 APRILI, 2012

Moja, Serikali iangalie vema suala la kuweka alama kwa leseni za madereva walioleta makosa. Naomba alama hizo ziwekwe kwa makosa maalum yaliyotolewa hukumu na Mahakama.

Pili, kutoa amri ya kufilisi mali za watuhumiwa waliofariki. Naomba ithibitike dhahiri kwamba mtuhumiwa ametenda kosa kweli na kuhukumu kwa mujibu wa Sheria ili kuhakikisha haki za warithi zinalindwa.

Tatu, mwenye jengo kuingizwa hatiani, ni sawa, lakini ithibitike wazi kwamba mwenye jengo amehusika, la sivyo wataingia hata wamiliki wa hoteli ambao wanapangisha wageni wanaofanya biashara za madawa ya kulevya bila wenye majengo au hoteli za kupangisha wageni kujua.

MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Mfuko wa Jimbo zisipitie Halmashauri, ni usumbufu na urasimu mkubwa, zimalizikie ofisi ya Bunge Zanzibar.

MHE. NEEMA M. HAMID:

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kuchangia Muswada huu kwa kuanzia suala zima la Wabunge wa Viti Maalum kupata Mfuko wa Jimbo na kushiriki katika kuangalia ni jinsi gani pesa za maendeleo ya wananchi zinavyotumika. Kwa kuwa Wabunge

16 APRILI, 2012

hawa wa Viti Maalum wapo kikatiba, hivyo basi, kuna umuhimu kwa Wabunge hawa kuwekwa kwenye mchakato huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, napenda nizungumzie suala zima la madawa ya kulevya sababu wahanga wakubwa wa madawa haya ya kulevya ni vijana. Napenda kusema kwamba tatizo kubwa la madawa ya kulevya ni tatizo la maadili. Uadilifu katika vyombo vya kusimamia haki, hivyo basi, tatizo si Sheria, tatizo kubwa ni rushwa, naomba sana tudhibiti uingizaji wa madawa ya kulevya, vijana wa Kitanzania wanakwisha na Taifa linaangamia kwa kuwa nguvu kazi inapotea.

MHE. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nachukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi na timu ya wafanyakazi wako Wizarani kwa kazi yenu nzuri. Baada ya utangulizi huu sasa naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Kwanza, *Means Testing, section 17*, utaratibu wa *means test* umeweka vigezo vya kuingiza katika kufikiria mkopo. Hata hivyo, kuna jambo moja kubwa la mzazi mjane (*single parent*) halijaingizwa kama moja ya vigezo. Kuna sababu moja kubwa kwamba kama baba amefariki na alikuwa ndiye chanzo kikubwa cha fedha za malipo ya ada kwa

16 APRILI, 2012

watoto, basi mama au mjane ni vigumu kuwa na uwezo wa kuwalipia watoto.

Pili, *priority courses*, utaratibu huu pamoja na uzuri wake tusiruhusu Waziri awe na mamlaka yeye peke yake kubadilisha *priority courses*. Kuna sababu kubwa moja ya kuzingatia hofu hii. Inaweza ikatokea Mheshimiwa Waziri akashawishika kusaidia watu fulani wanaochukua *course* ambazo hazimo kwenye *list* ya *priority* na kwa mwanya huu akaruhusu.

Tatu, *budget for Loans Board*, Serikali inaweza kuondokana na tatizo hili kwa kujiwekea utaratibu wa kukopa fedha kabla ya kufungua shule. *Public borrowing to the time of the required amount*. Serikali inaweza ku-raise *issue TB's or Treasury Bond of two, three et cetera maturities* kama inavyofanya kwa kukopea matumizi mengine. Fedha hiyo ilipwe *lumpsum* ili kuwaondolea kero watoto, vijana wetu mashuleni.

MHE. SUSAN A. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne iliyokuwa XI kuhusu usalama barabarani yaani *Road Traffic Act, Cap 168*. Nakubaliana na mabadiliko haya kwani kumekuwa na ongezeko kubwa sana la ajali barabarani kutokana na uzembe wa madereva na wengine kutokuwa na leseni. Pia uwepo wa *points* katika

16 APRILI, 2012

leseni hizi zitasaidia sana umakini wa madereva kama ilivyo kwa nchi zilizoendelea ambapo kila kosa linapunguza *points* na kufikia hata kufutiwa leseni. Hii itasaidia sana kwa makosa ya uzembe kupungua na kukoma. Nchi kama Marekani wamefanya hivyo na tunaona ni jinsi gani *drivers* wanavyokuwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano iliyokuwa XII kuhusu fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Kila mara suala hili limekuwa likizungumzwa hasa kuhusiana na jinsi gani Wabunge wa Viti Maalum watashiriki katika Mfuko huu. Wote kujua ni jinsi gani wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, ni vema basi suala hili liangaliwe nao waweze kushiriki au kupatiwa fungu lingine waweze kuwasaidia wapiga kura wao ambao kimsingi lina mahitaji sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita iliyokuwa ya XIII *amendment of the Proceeds of Crime Act Cap. 256*, nchi yetu ni nchi inayofuata haki na taratibu, ni jambo la kushangaza kuona kwamba sasa mtuhumiwa hajahukumiwa lakini anafilisiwa. Hivi toka lini mtuhumiwa, bado hajawa *convicted* ahukumiwe, huku ni kukiuka haki za mtuhumiwa na haki na warithi wa marehemu. Ni vema tuzingatie utawala wa sheria na haki za binadamu.

16 APRILI, 2012

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali. Nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi yake nzuri pamoja na wasaidizi wake wote waliofanikisha kuletwa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii ya marekebisho ya sheria imeletwa wakati muafaka kwa sababu Taifa limepita na kukumbana na changamoto nyingi zihusuzo umuhimu wa marekebisho ya sheria mbalimbali zihusuzo umuhimu wa marekebisho ya sheria mbalimbali na kwamba sheria hizi zimeletwa lakini bado kuna sheria nyingi ambazo zinahitajika kurekebishwa, zingine zinahitaji kutiwa nguvu katika utekelezaji:-

Kwanza, Sheria ya Mtu Kuvuta Sigara Hadharani, sheria hiyo inatakiwa kuwekewa msukumo wa kutisha kwa sababu haitiliwi maanani, watu wanavuta sigara holela bila kujali watu wasiovuta sigara ambao mwisho wake inawaletea madhara makubwa.

Pili, sehemu ya kumi na moja ya Muswada huu ambao unalenga kufanya marekebisho katika Sheria Ya Usalama Barabarani, naiomba Serikali

16 APRILI, 2012

kufanya utafiti zaidi kwamba chanzo kikubwa cha ajali zinazotokea nchini ni nini?

Pia uwekaji wa alama barabarani uende sambamba na sheria hizi kwani siku hizi barabara zote zimejaa matuta ili kuzuia uendeshaji mbovu wa madereva. Kwa kweli huu siyo ufumbuzi, lakini ni muhimu kuweka sheria kali ili kuzuia ajali kwa ujumla.

Tatu, sehemu ya 15 ya Muswada huu, Sura ya 95 inayolenga kurekebisha Sheria ya Kuzuia na Kusafirisha Madawa ya Kulevya inatakiwa kufanyiwa utafiti wa kutosha kwa sababu tatizo hilo ni tatizo la nchi zote maana hata nchi zilizoendelea ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maoni yangu machache kwenye marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Biashara ya Dawa za Kulevya, Sura 95 ya Sheria za Tanzania. Ni jambo la wazi kabisa kuwa njia kuu ya kuingia nchini dawa za kulevya na biashara zingine haramu ni vibandari visivyo rasmi kwenye pwani ya Bahari ya Hindi. Vibandari vyenyewe ni Ununio, Bagamoyo – Bandari ya zamani na Mlingotini, Pangani na kwingineko. Naiomba sana Serikali

16 APRILI, 2012

iziaangalie bandari hizi na kuzidisha doria na Polisi na hata Jeshi la Wananchi. Bila kufanya hivi, nchi yetu itaendelea kuwa njia kuu ya kupitisha dawa za kulevya kwenda nchi nyingine. Pia biashara zingine haramu zinaikosesha Serikali mapato makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuleta Muswada huu ili upitishwe uwe sheria hasa kwa sababu unagusa mambo ambayo kwa muda huu (enzi ya utandawazi, teknolojia kubwa) ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Serikali katika Sheria ya Mapato kwa njia ya Uhalifu, Sura 256. Mtu mwizi au fisadi anayejiipatia fedha kwa njia ya udanganyifu atakuwa ana historia hiyo na kama hana hatia, hamna sababu ya kutoroka. Akifariki mtu huyu, *background* ya tabia yake itaangaliwa, biashara anayofanya itachunguzwa. Ikijulikana anajipatia fedha kinyume na taratibu afilisiwe. Kusubiri mpaka Mahakama ku-*prove beyond resonable doubt* ni kutoa mwanya wa rushwa na ushahidi kupotezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Serikali katika mapendekezo ya sehemu ya 16 ya Muswada

16 APRILI, 2012

kuhusiana na Sheria ya Kuzuia na Kusafirisha Dawa za Kulevya, Sura ya 95. Mapendekezo ya kifungu cha 51, nashauri yaangaliwe upya lakini adhabu isiwe chini ya miaka mitano (5) na isiwe na *parole* hata kama mtu amepatikana na gramu 10. Hii ni kwa sababu inawezekana aliyekamatwa siku hiyo na gramu 10, kuna siku nyingine anakuwa na mzigo wa kilo moja au zaidi. Kwa vile taarifa zilizopo ni kuwa wanaokamatwa na mizigo kamwe hawawataji *masters* wao, sheria ikiwa kali itawafanya wanaotumiwa waogope/wakatae kutumwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kifungu cha 52, kinachoongeza kifungu kipya cha 17A.(c), neno "owner" libadilishwe. Naungana na maoni ya Kamati. Hii ni kwa sababu Watanzania wengi mapato yao ni pamoja na mapato yanayotokana na nyumba za kupangisha/kulala wageni. Desturi iliyopo, mwananchi anajenga nyumba Kimara, yeye anaishi Mikocheni. Yeye anadai kodi ya mwaka mzima au miezi sita (6) na anaweza mwaka mzima asifike katika nyumba hiyo hasa kama wapangaji wake ni wastaarabu, yatakayofanyika katika nyumba yake ni vigumu sana kuyafahamu. Naishauri Serikali iweke utaratibu wa kutaka nyumba zilizopangishwa wapangaji wachache *identity* zao mara tu wanapoingia, taarifa ambayo mwenye

16 APRILI, 2012

nyumba atatakiwa kui-*submit* katika vyombo vya Dola mara itakapotokea mashaka/tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la fedha chafu inaelekea ni kubwa nchini. Ninaomba ufafanuzi, Serikali haina fedha lakini miji mingi nchini majengo marefu yanaota kama uyoga, ukata wa maisha ambao kila mtu analalamika, kuporomoka kwa uchumi wa dunia wa nchi kama Marekani – inaelekea uchumi unaporomoka tu kwa Serikali ya Tanzania. Wananchi wa Marekani walifikia hatua wakashindwa kulipa *mortgage* za nyumba zao, lakini Tanzania nyumba zinajengwa na viwanja kununuliwa kwa bei za juu karibu maeneo yote ya Jiji la Dar es Salaam/Arusha. Fedha hizi Watanzania hawa wanazipata wapi? Je, hakuna fedha chafu katika hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ufafanuzi, napenda kuunga mkono hoja.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Sheria na Katiba, Mheshimiwa Celina Kombani, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Werema, Katibu Mkuu wa Wizara ya Sheria na Katiba pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Muswada huu wa marekebisho ya sheria mbalimbali kwani itasaidia

16 APRILI, 2012

sana kuzifanyia marekebisho sheria ambao hazitendi haki kwa Watanzania hasa wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya Mahakama kwa watuhumiwa wa makosa mbalimbali kukaa mahabusu muda mrefu. Yapo matatizo ya mahabusu kukaa rumande muda mrefu bila ya kesi kutajwa Mahakamani matokeo yake mahabusu hukaa rumande muda mrefu bila kujua jambo linaloendelea dhidi yake. Hivyo, naomba kupendekeza kuwa ni vema kuwepo na muda maalum wa upelelezi na hatimaye kesi ianze kusikilizwa hususani kesi za mauaji kwani sio watuhumiwa wote huwa wanahusika na mauaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mfuko wa Jimbo. Napenda kutoa masikitiko yangu kuona Sheria ya Mfuko wa Jimbo inatoa haki kwa Wabunge wa Jimbo na kuwabagua Wabunge wa Viti Maalum wakati wote ni Wabunge na majukumu yao yanafanana. Ninaomba sheria hii iangaliwe upya ili iweze kutoa huduma zinazofanana, Wabunge wa Viti Maalum wawe wajumbe wa Kamati ya kugawa mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usalama Barabarani. Pamoja na sheria kutungwa na adhabu kuwekwa bado suala la usalama barabarani ni duni sana. Napeda sheria hii iende sambamba na

16 APRILI, 2012

kuboresha maslahi ya Askari kwani rushwa inafanya sheria hizi zisifanye kazi ipasavyo. Hivyo ni vema suala la maslahi liangaliwe upya ili kusaidia Sheria za Usalama Barabarani kutekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumalizia kuungana na Wabunge wenzangu kuomba Muswada wa Sheria ya Korosho kuletwa haraka Bungeni kwani wananchi wanapata kero sana kwani soko la korosho linapunguza sana imani ya wananchi na Serikali yao. Vilevile ninaomba sheria ambazo zimepitwa na wakati zifanyiwe marekebisho ili ziweze kwenda na wakati kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumaliza kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia na ninawatakia utekelezaji wenye tija.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mchango wangu juu ya Muswada wa Sheria hii, ni kuhusu ucheleweshaji wa mirathi. Kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa wa mirathi jambo ambalo hufanya hata familia ya marehemu kufikia hatua ya kukata tamaa hatimaye mali au mirathi kupotea, familia ya marehemu kuendelea kupata shida, watoto wa marehemu kushindwa kudumu gharama mbalimbali hizi za kimaisha kama vile elimu, matibabu na kadhalika.

16 APRILI, 2012

Hivyo kuwe na muda maalum, kuwe na chombo cha kuratibu muda tokeq marehemu amefariki hadi muda wa kutoa mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utoaji wa *point* kwenye leseni kwa madereva. Sheria nyingi zimetungwa katika nchi hii kutaka kudhibiti uhalifu wa aina mbalimbali. Tatizo tulilionalo ni kutokuwa na usimamizi mzuri, ukosefu wa uadilifu, rushwa, ufuatiliaji dhaifu, upendeleo na kujuana. Hivyo, ili kudhibiti suala hili ni kuondokana na mambo niliyoandika hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Jimbo madhumuni yake mkubwa ni kuchochea maendeleo ya Jimbo, Mbunge wa Viti Maalum ni Mbunge wa eneo lote la Mkoa na *mandate* ya uchaguzi wake amechaguliwa na akina mama wenzie bila kuhusisha wanaume. Hivyo Wabunge wa Viti Maalum kama wanataka kuhusika na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, waende wakagombee Majimboni, hakuna anayewakataza, ni haki yao na tunakubaliana kuwa akina mama wanaweza, waende wakagombee Majimboni, huo ndio ukweli wenyewe, wasipende kujishusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

16 APRILI, 2012

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ndiyo ufunguo wa maisha na hapa Bungeni tumekuwa mara nyingi tukisikia taarifa za migomo ya wanafunzi na mizozo inayoendelea kila siku kati ya wanafunzi na Vyuho Vikuu na Bodi ya Mikopo. Ni wakati muafaka sana wa kujadili jambo hili lakini kwa masikitiko makubwa Muswada huu umeondolewa na huku mahitaji kwa wanafunzi wetu bado ni tatizo kubwa kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la madawa ya kulevya, tatizo hili halitamalizika tu kirahisi bila kushughulikiwa kwa dhati na wale ambao wanaingiza madawa hayo hapa nchini. Serikali kwa tafsiri nyingine inawaonea vijana ambao wamekosa kazi mitaani na wameingia katika biashara hii haramu na kuwaacha lakini bila kuwashughulikia wale ambao wanaingiza madawa haya hapa nchini. Vijana wote wanaokamatwa na kufikishwa Mahakamni kwa kiwango kikubwa ni wale wanaosinzia mitaani na ambao wanajidunga sindano kuongeza (stimu) na ambao wanauza (wauzaji wadogo) humu mitaani, lakini wanaopitisha kwa makilo katika viwanja vya ndege na bandari zote, hufanya mapato na watendaji katika vituo hivyo, mzigo unapitishwa chini ya ulinzi ukiwa salama na hakuna hatua. Napendekeza ili kukomesha jambo hili ni vyema tukatoa adhabu ya kunyongwa kwa wale ambao wanakamatwa na pia kuwafanyia

16 APRILI, 2012

mabadiliko wale wenye mamlaka ya kuandaa na kuendesha mashtaka juu ya wahusika hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *CDCF*, jambo hili mimi kama Mbunge wa Zanzibar inanisikitisha sana juu ya namna utaratibu wa mfuko huu wa maendeleo ya Jimbo langu namna ambavyo inatupatia usumbufu mkubwa katika kuweza kupanga matumizi yaliyokusudiwa katika Majimbo yetu. Kwa Zanzibar utaratibu wa mfuko huu unadhalilisha sana Mbunge kwa namna ambavyo Halmashauri zinajiona kama kwamba wao ndio wenye mfuko na Mbunge anaomba kwao, jambo ambalo sio sahihi. Ushauri wangu katika jambo hili ni kwamba katika mfuko huu kwa Zanzibar usimamiwe na Ofisi ya Bunge na Afisa wa Bunge awe ndiye mdhibiti na msimamizi katika mchakato wa fedha za mfuko, lakini pia Diwani naye awe katika wale watia saina Benki katika fedha hii na asiwe Afisa Mipango wa Halmashauri pekee, jambo hili ni pamoja na sababu za Halmashauri kuwa na kiburi juu ya mfuko huu. Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika Muswada huu hususani katika mambo mkuu mawili. Kwanza katika kifungu cha 29, kifungu cha 25(1), Sheria haijaainisha ni kwa *grade* zipi za udereva leseni

16 APRILI, 2012

zitakuwa zinatolewa kwa kuzingatia *point* gani? Kwa maana nina *Class E* na mwingine *Class C*, je, hawa wanaadhibiwa kwa upungufu wa *point* zao kwa kuzingatia adhabu au *grade* ya *class* zao za leseni? Pili, je, mafunzo thabiti yametolewa kwa madereva wote kuhusiana na ingizo jipya la adhabu katika kundi lile la adhabu? Hivi sasa ni tozo ya fedha lakini tunashuhudia ni kwa kiasi gani sheria haifuatwi badala yake inaishia kuwafaidisha traffic polisi ambao huona ni bora wampe kati ya fedha ya tsh 2000 hadi 10,000/=. Je, tumejiandaa na chombo kipi kuhakikisha kuwa utoaji wa adhabu hii unatumika kama inavyokusudiwa maana isije ikawa ni ulaji wa watu wachache. Je, hao ma-traffic wamefundishwa? Je, kuna chombo mahsusi? Je, watumiaji wa barabara wameelimishwa? Naomba haya yaingizwe

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madawa ya kulevya, naomba wale waingizaji wa madawa haya wachukuliwe hatua na si kuwaonea watu wasio na kipato ambao hutumika kama wasafirishaji au wasambazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi hili suala la Wabunge wa Viti Maalum kuwa kama *subordinates* wa Wabunge wa

16 APRILI, 2012

Majimbo, litarekebishwa lini? Maana Mbunge wa Viti Maalum, yeye ni Mjumbe tu kwenye kikao cha kujadili namna ya kutumia pesa za Mfuko wa Jimbo, lakini hawa Wabunge hawana ratiba maalum ya pamoja juu ya matumizi ya Mfuko huo, ukizingatia kuwa Mwenyekiti wake ni Mbunge wa Jimbo. Nadhani eneo hilo inabidi liangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa AG atasema na Wabunge wa Viti Maalum nao wakagombea Majimbo? Hapana. Viti Maalum lazima vijazwe mpaka hapo Sheria itakaporekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi watoe adhabu hapo hapo kwa kosa la wazi ili kutoa mwamko na kupunguza kesi za Mahakamani, hata Ulaya wanafanya hivyo. Naunga mkono hoja.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kikao cha Nne, tulitarajia marekebisho ya Sheria ya Korosho utawasilishwa. Lakini kwa masikitiko makubwa, tuliambiwa marekebisho hayo yameondolewa kwenye Kamati, yatawasilishwa katika Mkutano wa Tano na ilikuwa ni kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Leo hii Sheria haijaletwa: Je, ni nani anazuia Sheria hii isiwasilishwe katika Mkutano huu? Je, kuna ajenda ipi katika zao

16 APRILI, 2012

la korosho? Kwani kadiri tunavyojitahidi kutafuta ufumbuzi wa kuweka utaratibu mzuri inashindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa korosho ni sehemu ya Watanzania ambao wanapaswa kusikilizwa na kuwekewa utaratibu mzuri wa kupata haki zao ili kuboresha maslahi yao na Taifa kwa ujumla. Kwa nini kuwe na watu wachache bila kutumia utaratibu, waweze kukwamisha suala zima la kurekebisha Sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipatiwe jibu la uhakika juu ya kukwama kwa marekebisho haya. Ahsante.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii nitoe mchango wangu juu ya marekebisho ya Sheria mbalimbali. Suala zima la makosa ya barabarani ambayo yanasababishwa na madereva wazembe na kusababisha ajali za mauaji na ama vilema, zinasababishwa na rushwa zinazofanyika baina ya dereva na Polisi au baina ya Kampuni na Polisi ambaye amehudhuria katika eneo la tukio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauaji ya barabarani yameongezeka na sasa limekuwa ni jambo la kawaida kwa nchi yetu ya Tanzania. Hivyo, Sheria hii kufanyiwa marekebisho itasaidia sana kutoa haki

16 APRILI, 2012

kwa Watanzania ambao haki zao za kuishi zilikuwa au zinaendelea kuvunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama zina wajibu wa kuchukua na kuyachunguza makosa ambayo yanasababishwa na madereva. Kuna wajibu wa Mahakama kuliangalia kosa kwa kufuata Sheria na siyo kuangalia aliyefanya kosa ana uwezo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna haja ya kuwaangalia *Traffic* juu ya uwajibikaji wao. Je, uwajibikaji wao ni halali na unazingatia Sheria za nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la dawa za kulevya pamoja na kuundiwa Sheria, lakini tuna wajibu wa kuliangalia suala hili kwa upana wake. Hivyo ni kweli kwamba, Serikali hii haina vyombo ambavyo vinaweza kuwakamata waingizaji wa dawa za kulevya? Je, hawako ambao wana mamlaka ya kiulinzi ambao wanatumiwa katika kuingiza dawa hizo? Je, hao hawana hisa zinazotokana na dawa hizo? Kwa nini pamoja na Sheria hii ambayo imefanyiwa marekebisho iwe suala hili linaendelea, hali ya kuwa Kitengo cha Udhhibiti wa Dawa za Kulevya kipo? Je, kinafanya kazi gani? Kwa nini Serikali haijachukua hatua za nidhamu ikawawajibisha wao kwanza?

16 APRILI, 2012

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa marekebisho, uwepo wa Sheria hi,i basi ni muhimu kuunda kikosi kazi kitakachodhibiti hali hii. Kama siyo hivyo, nchi itaenea vichaa na vibaka wasioweza kuijenga nchi katika maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa *CDCF*, pamoja na marekebisho yaliyofanywa katika Sheria, yakiidhinishwa toka Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Muungano) na kupelekwa moja kwa moja kwenda Ofisi ya Bunge Zanzibar na kuidhinisha kuingizwa katika Halmashauri husika, lakini ni bora pia, Mheshimiwa Mbunge husika wa Jimbo, apewe nafasi ya kusaini ndipo pesa hiyo itolewe. Kwani mantiki ya kumtoa Mbunge katika upatikanaji wa fedha hizi, sioni na sijui malengo yake ni yapi. Suala la kusaini liwahusu Wabunge wote Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi Diwani wangu na Mwenyekiti wa Halmashauri wa Wilaya yangu, alithubutu kusema kwamba, fedha zile ni za wananchi na hazihusiani kabisa na Mbunge. Hivyo, Mbunge akitaka kusaidia atoe pesa zake za mshahara. Sasa nitamwomba Mwanasheria Mkuu, atutolee ufafanuzi. Je, Mfuko huu unatuhusu Wabunge au la? Kama unatuhusu kwa ajili ya kuamsha ari katika kuchangia maendeleo ya watu

16 APRILI, 2012

wetu, basi ielezwe kwenye Bunge hili. Tusiondoke hapa, watu baadaye wakapelekewa Sheria nyingine wakaitumia katika kutudhalilisha sisi Wabunge. Ikiwa sisi Wabunge kutoka Majimboni hautuhusu, kwa nini Wabunge wa Viti Maalum, hawaingiziwi fedha za *CDCF*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sina fadhila kama sikuunga mkono marekebisho ya Sheria hii, kwani ni ufumbuzi wa matatizo ya kulinda haki ya raia kwa nchi yao, usalama wao na maisha na mali zao. Nashukuru sana.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono uamuzi wa Serikali kuondoa marekebisho yote yaliyohusiana na mikopo ya elimu ya juu katika Muswada huu wa marekebisho ya sheria mbalimbali. Marekebisho yaliyotolewa yanakiuka katiba ya nchi kwa kuongeza ubaguzi na kuchochea migogoro katika elimu ya juu. Aidha, marekebisho hayo yameandaliwa bila wadau ikiwemo wanafunzi wa elimu ya juu na wahitimu wa Vyuho na Vyuho Vikuu kuhusishwa kwa ukamilifu wake. Aidha, marekebisho hayo yaliletwa Bungeni wakati ambapo ripoti ya Tume iliyoundwa na Rais kuhusu mikopo elimu ya juu na migogoro iliyopo vyuoni haijawasilisha taarifa Bungeni. Hivyo ni muhimu kabla ya Serikali kuleta marekebisho kuhusu mikopo ya elimu ya juu, itoe

16 APRILI, 2012

Bungeni ripoti ya uchunguzi husika na pia Kamati zinazosimamia sekta husika na wadau kwa ujumla kuhusiana na ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sehemu ya 10 ya marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Polisi, (*Cap. 322*, Marekebisho yaliyoletwa ni madogo sana ukilinganisha na ahadi ambayo Serikali iliitoa Bungeni nilipouliza swali la nyongeza kuhusu umuhimu wa Sheria ya Jeshi la Polisi kufanyiwa marekebisho makubwa kwa kuzingatia Mikataba ya Kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia. Seriali itoe kauli ni lini Sheria ya Jeshi la Polisi itafanyiwa marekebisho makubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani (*Cap 168*), Mamlaka ya Waziri yawekwe udhibiti kwa kuwekwa pia jedwali la makosa yanayohusika. Aidha, Serikali ipitie ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ufanisi wa ukaguzi barabarani (*A performance Audit Report on the Management of Traffic Inspections and Speed Limit in Tanzania*) ya mwezi Marchi, 2012. Kutokana na mapendekezo ya ripoti hiyo, Serikali iwasilishe marekebisho zaidi kwa lengo la kuwezesha ufanisi katika ukaguzi, kudhibiti ufasidi katika masuala ya usalama barabarani, kuwezesha vifaa stahiki kuweza kupatikana kwa ajili

16 APRILI, 2012

ya Askari wa Usalama Barabarani na kuwezesha usimamizi thabiti wa utawala wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo *Cap 96*, Serikali ilete mapendekezo mengine ya nyongeza ya jedwali la marekebisho ya sheria kuwezesha Wabunge wa Viti Maalum kuingia katika Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Maelezo kwamba marekebisho haya yanahusu Zanzibar pekee hayajibu hoja ya msingi ya ahadi ya Waziri Mkuu kuwa kifungu husika kingeletwa kwenye marekebisho ya sheria mbalimbali. Pia Serikali itoe kauli kuhusu hatua iliyofikiwa ya kesi iliyoko Mahakamani ya kupinga sheria husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Dawa za Kulevya *Cap 95*, pamoja na kuleta marekebisho ya sheria kwa kwa kuongeza adhabu, Serikali itoe ahadi ya kuleta marekebisho ya kuiongeza mamlaka na uhuru kwa Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka (*DPP*) katika kufanya uchunguzi na kuendesha mashitaka ya dawa za kulevya. Pia marekebisho mengine ya sheria yaletwe kwa ajili ya kuweka mfumo wa kisheria wa kuwahudumia waathirika wa dawa za kulevya (*mandatory rehabilitation*).

16 APRILI, 2012

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuwashukuru Wabunge wote waliochangia katika Muswada huu ambao una mambo mengi mazito na mambo ambayo yanahitaji utulivu katika kuyashughulikia. Kwa kweli ninafarijika kwamba Wabunge waliozungumza 16 wametoa maelezo yenye busara katika kuboresha Muswada wetu na pia maoni ambayo tunadhani yanatusaidia kuboresha si sheria hizi tu bali pia zitakazoshughulikia mambo yetu ya sheria siku za usoni. Wabunge waliochangia kwa mdomo ni Wabunge 16 ninaomba kuwatambua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa kwanza alikuwa Mheshimiwa John Paul Lwanji aliyesoma taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, aliyesoma taarifa ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwenye eneo hili, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Pindi Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Mariam Kasembe, amesema kwa uchungu sana kuhusu suala hili la korosho na kwa kweli dada yangu Kasembe nakuhakikishia kwamba hakuna *agenda* wala siri ya kutaka kuhujumu Watanzania wenzetu wanaotegemea kilimo cha korosho. Na kwa kweli hakuna kikundi

16 APRILI, 2012

kinachohusika kinachoweza kunishawishi mimi kuhujumu watu wanaolima korosho. *(Makofi)*

Mchangiaji wa nane, alikuwa Mheshimiwa Mustapha Akunaay, simuoni, Mheshimiwa William Mgimwa, Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa njia ya maandishi jumla yao 35, Mheshimiwa Catherine Magige, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Kepteni John Komba, Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa William Mgimwa, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Karuthum Mchuchuli, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa

16 APRILI, 2012

Betty Machangu, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa *Engineer* Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Luhanga Mpina, Mheshimiwa Neema Hamid, Mheshimiwa Amina Mwidau, Mheshimiwa Said Bwanamdogo na Mheshimiwa Esther Matiko.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao ya mdomo na ya maandishi.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo waliotoa maoni kwa zile sheria tulizoziondoa, narudia tena kutoa taarifa kwamba Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inahitaji kufanyiwa marekebisho makubwa na kwa kweli tunahitaji kuwahusisha wadau sawasawa. Kwa hiyo, *report* hiyo baada ya utaratibu huo tunategemea kwamba itawasilishwa hapa Bungeni na pengine kama tukipata ruhusa katika Bunge bila kutegemea Bunge la mwezi wa sita kama tutaweza.

